ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Mhe. Pandu Ameir Kificho	-	SPIKA
1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi		- MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini		- MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary		-MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad		-MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban		-MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji		-MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed		-MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa

12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	-MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	-MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	-MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	-MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	-MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	-MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	-MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	- Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	-Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	- Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	-Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	-Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	-Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	- Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	- Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	- Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	- Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	- Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	- Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	- Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	- Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	- Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Ashura Sharif Ali	- Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	- Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Farida Amour Mohammed	- Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Fatma Mbarouk Said - Jimbo la Amani

41.Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura

42.Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani

43.Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani

44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe

45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Muyuni

46.Mhe. Kazija Khamis Kona - Nafasi za Wanawake

47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Jimbo la Kikwajuni

48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Jimbo la Kitope

49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Jimbo la Mkwajuni

50.Mhe. Mgeni Hassan Juma - Nafasi za Wanawake

51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Jimbo la Bumbwini

52.Mhe. Mohammed Haji Khalid - Jimbo la Mtambile

53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi - Jimbo la Chambani

54.Mhe. Mohammed Said Mohammed - Jimbo la Mpendae

55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Nafasi za Wanawake

56.Mhe. Mussa Ali Hassan - Jimbo la Koani

57. Mhe. Mussa Khamis Silima - Jimbo la Uzini

58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Rahaleo

61.Mhe. Omar Ali Shehe - Jimbo la Chake-Chake

62.Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Rashid Seif Suleiman - Jimbo la Ziwani

64.Mhe. Raya Suleiman Hamad - Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rufai Said Rufai - Jimbo la Tumbe

66.Mhe. Saleh Nassor Juma - Jimbo la Wawi

67.Mhe. Salim Abdalla Hamad - Jimbo la Mtambwe

68.Mhe. Salma Mohammed Ali - Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Salma Mussa Bilali - Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salmin Awadh Salmin - Jimbo la Magomeni

71.Mhe. Salum Amour Mtondoo - Jimbo la Bububu

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan - Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki - Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai - Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim - KATIBU

Kikao cha Tatu – Tarehe 21 Januari, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 53

Utoaji wa Elimu wa Mfumo Mpya wa Serikali

Mhe. Ussi Jecha Simai - Aliuliza:-

Ingawa wananchi wa Zanzibar walikubali kuanzishwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa asilimia 66.4 na Serikali ilifanya Marekebisho ya 10 ya Katiba ya Zanzibar ya 1984 ili iendane na mfumo huo. Hata hivyo, imebainika kwamba wananchi walio wengi hawaufahamu mfumo huu mpya wa Serikali.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaelimisha zaidi wananchi ili wauelewe mfumo huo.

Mhe.Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 53 lakini kwanza naomba nitoe maelezo mafupi kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Awamu ya Saba yenye muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, inawapongeza wananchi wote wa Unguja na Pemba kwa kuitumia haki yao ya Demokrasia, wakati wa kura ya maoni juu ya mfumo gani utumike mara baada ya Uchaguzi Mkuu wa tarehe 31 Oktoba, 2010.

Mhe. Spika, uamuzi wa wananchi wa kutaka kuanzishwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa asilimia 66.4 haukuwa wa kubahatisha na leo hii sisi sote ni mashahidi wa namna nchi yetu ilivyokuwa na amani, utulivu, umoja na mshikamano.

Kwa mnasaba huo, naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza Viongozi wetu Waasisi wa mabadiliko haya, Rais Mstaafu wa Zanzibar wa Awamu ya Sita Mhe. Amani Abeid Karume na Katibu Mkuu wa CUF ambaye

ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Maalim Seif Sharif Hamad pamoja na viongozi na wananchi wote wa Zanzibar.
Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ina mpango wa kutoa elimu zaidi kwa umma juu ya muundo mpya wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa pamoja na kueleza mafanikio yaliyopatikana tangu kuwepo madarakani kwa Serikali ya Mapinduzi ya Awamu ya Saba yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa.

Aidha, napenda niwahakikishie Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuwa Serikali ilishaanza kuchukua jitihada za kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vyetu vya habari, mikutano ya hadhara, midahalo mbali mbali na makongamano pamoja na kufanya mikutano ya ndani kupitia vyama vyetu vya siasa kuwaelezea muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Spika, kutokana na jitihada hizo ndio maana zoezi la Kura ya Maoni kuhusu Serikali ya Umoja wa Kitaifa limefanyika vizuri kwa amani na utulivu mkubwa na matokeo yake ndio chanzo cha Marekebisho ya Kumi ya Katiba yetu yaliyopelekea kuanzishwa kwa muundo huu mpya wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa swali mama liliuliza kuhusu uelewa wa wananchi juu ya utaratibu wa uendeshaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Sisi tulipata taarifa kupitia vyombo vya habari mbali mbali kabla ya uchaguzi kwamba ile Tume ya Wawakilishi Sita waliowakilisha vyama vyetu viwili kushughulikia mchakato ule wa kura ya maoni na kupatikana kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ilipata safari ya kwenda nje na kujifunza mambo mengi. Lakini taaluma waliyoipata kule haijatufikia sisi wala wengine.

Je, ziara ile ilikuwa ni ya bure kwenda haikuwa na maana au ilionekana kwamba basi walikwenda kutembea. Kama si hivyo, kuna utaratibu gani wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kuitumia tume ile na taaluma yao ili na sisi kutujulisha nini walichokivuna katika ziara hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ni nia ya serikali kupitia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kukaa na tume ile itusaidie mawazo mbali mbali waliyojifunza huko nje ili yasaidie katika kutoa elimu kwa umma.

Hivi sasa tuna mpango wa kupeleka warka maalum serikali juu ya jambo hili ili tulifanye kwa kuwashirikisha wadau wote na wananchi wapate elimu ya kutosha kwenye jambo hili kubwa. Kwa sababu Mhe. Spika, kuuenzi na kuuendeleza umoja huu ndio chanzo kikuu cha amani na utulivu katika nchi yetu na upendo wa Wazanzibari.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Mhe. Waziri wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais naomba kuongezea jibu la nyongeza kuhusu swali lililoulizwa na Mhe. Rashid Seif Suleiman Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Ziwani.

Mhe. Spika, kwanza Baraza lako tukufu lielewe kwamba kazi ya kuwaelimisha wananchi juu ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa ilifanywa na Kamati ya Watu Sita ya Baraza la Wawakilishi kabla ya uchaguzi wa kuchagua mfumo gani ufuatwe Zanzibar. Kazi hiyo ilifanyika kabla ya kwenda nje ya nchi kwa kamati hiyo. Kazi hiyo ilifanyika kwa uadilifu mkubwa katika kamati kupita katika kila wilaya kukutana na watu mbali mbali kuweza kutoa taaluma hiyo. Ndio maana wananchi wa Zanzibar wakachagua mfumo huu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Kwa hiyo, suala la kwenda nje halikuwa juu ya suala la taaluma juu ya kuchagua mfumo. Suala la kwenda nje lilikuwa ni kwenda kujifunza baada ya huo uchaguzi wa kuchagua mfumo, serikali ambazo zinafuata mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa zinaendeshwaje. Kazi hiyo ilifanyika kwa kwenda katika nchi ya Uingereza na Ujerumani. Kamati iliporudi iliandaa ripoti na ripoti hiyo ikaletwa kwako Mhe. Spika, hatimae ripoti hiyo ikapelekwa kwa Mhe. Rais.

Ndio maana baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 serikali iliopo madarakani ya Awamu ya Saba imeunda serikali kwa kufuata ushauri ambao umetolewa na kamati kulingana na Katiba ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza nawapongeza mawaziri wote wawili kwa jawabu zao nzuri. Lakini Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora ameeleza kwamba kamati ile ya watu sita ilikwenda nchi za Uingereza na Ujerumani kwenda kujifunza ni namna gani ya kuendesha Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Lakini ninavyojua mimi muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya Uingereza na Ujerumani ni tofauti. Kwa sababu kwa bahati nzuri Mhe. Spika,

hata na mimi uliwahi kunipa nafasi nikenda Uingereza pengine kujifunza mambo haya haya. *(Makofi)*

Sasa mfumo wa wenzetu ni tofauti na wa Zanzibar. Zanzibar mfumo wake wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni wa aina yake haujawahi kutokea duniani. Je, tunaoanisha vipi mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa wa Ujerumani na huu wa Zanzibar. Kwa sababu matokeo ya uchaguzi ya nchi zile na ya Zanzibar ni tofauti.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ni kweli mfumo huu ni mfumo wa aina yake ulimwenguni. Mhe. Spika, nataka nichukue fursa hii nilipongeze Baraza lako tukufu lililokwisha kwa kufanya maamuzi makubwa ya kubadilisha katiba na kupata muundo huu mpya. Kwa kweli wamefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Wazanzibari kiutamaduni ni watu wamoja, wenye tabia moja, wenye mwenendo mmoja na ndio maana tukafikia muundo wetu huu na nina kila sababu ya kusema kwamba muundo huu utaendelea vizuri katika kuliendesha taifa letu.

Mhe. Spika, hiyo mifumo mingine katika nchi nyengine imetusaidia kujifunza ili kuweza kuwa na muundo huu wa aina yake ambao ulimwengu mzima wanatusifu kwa namna tulivyouunda na namna tunavyoutekeleza. Mhe. Spika, nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba tutauenzi na kuuendeleza. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri amekiri kwamba muundo huu ni tofauti na ule wa Ujerumani na Uingereza. Kwa kuwa Baraza la Wawakilishi hutoa nafasi ya kutembelea nchi za nje. Kwa kuwa sisi ni wawakilishi wa wananchi wa Zanzibar. Je, Mhe. Waziri haoni haja ya kutoa mafunzo maalum kwa wawakilishi wote ili kutupa tofauti ya Zanzibar, Ujerumani na Uingereza. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Waziri unaona unavyozungukwa zungukwa hivi. *(Kicheko)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza napenda nikiri kwamba Mhe. Hija Hassan Hija hii ni mara ya mwanzo kukusikia vizuri kutokana na spika yako.

Mhe. Spika, nia ya serikali ni kutoa elimu kwa umma na inaamini kwamba Waheshimiwa Wawakilishi wanayo nafasi kubwa katika kutoa elimu hiyo katika majimbo yao. Mwenyezi Mungu akitujaalia uwezo ukiwa mzuri hatua

kwa hatua tutajitahidi kuchukua nafasi hiyo na kuwapa nafasi Waheshimiwa Wawakilishi kwenda kujifunza katika nchi mbali mbali ulimwenguni.

Mhe. Spika: Sijui kama umefika pahala? Anachouliza Mhe. Hija Hassan Hija je, unaweza ukaandaa utaratibu wa kutoa mafunzo kuhusu hayo yaliyokwenda kusomwa. Ndio nikakwambia anakuzunguka zunguka yule. Ofisi yako itafanya hivyo kutoa mafunzo. *(Kicheko)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa tayari umejibu swali lenyewe hatuna shaka yoyote kuheshimu mawazo yako na tutachukua hatua kama Mhe. Mwakilishi alivyosema kutokana na hali itakavyoruhusu. *(Makofi)*

Nam. 57

Meli Kumwaga Maji Baharini

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Aliuliza:-

Kwa kawaida meli hutolewa maji kabla ya kupakia abiria na mizigo. Kwa kuwa katika bahari yetu ya mwambao hufunga nanga pia meli zinazotoka nchi za ng'ambo.

Je, Mhe. Waziri maji ya bahari ya nchi mbili hizi (mwambao na ng'ambo) yakichanganyika pamoja hayana madhara yoyote kwa viumbe vya baharini.
Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais - Alijibu:

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 57 naomba nitoe maelezo yafuatayo:-
Mhe. Spika, naomba kwanza nikubaliane nae kwamba ni kweli baadhi ya meli huingizwa maji ya bahari ili kuweka usawa wa meli *(ballast water)* na inapofika safari yake maji hayo hutolewa kwa kumwagwa baharini.
Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba nijibu swali la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:

Maji ya bahari ya nchi mbili yanapochanganyika yanaweza kusababisha madhara kwa viumbe vya bahari endapo:

Maji yaliyochukuliwa yatabeba viumbe vamizi wa bahari *(marine invasive species)* ambao watafanya ushindani wa chakula dhidi ya viumbe asili *(marine indigenous species)* au kuwala hao viumbe asili madhara ambayo yatapelekea kupungua kwa viumbe vya bahari nyengine.

Iwapo maji yaliyochukuliwa yatakuwa yamechafuka *(polluted)* ambayo yataweza kusababisha madhara kwa viumbe kwenye bahari nyengine.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri ataweza kutufahamisha kwamba wizara yake imejipanga vipi kwa wale watu wanaokuja kutumia bahari yetu na vyombo vyao kuweza kumwaga maji katika bahari hii na kuweza kuathiri viumbe. Je, kuna gharama au kitu chochote ambacho wanatakiwa kufanya.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, ingawa hakuna uchunguzi wa kina bado ambao unathibitisha kuwa maji ya bahari yetu yamepata madhara kutokana na meli hizo ambazo hubeba *ballast water*.

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kupitia wadau wake wote wa bahari ilikaa pamoja na kupanga mikakati ifuatayo ili kukabiliana na tatizo hilo.

a. Kuongeza ufahamu wa tishio la viumbe vamizi baharini *(marine invasive species);*

b. Kuainisha viumbe vya bahari vilivyo hatarini kutoweka;

c. Kueleza wajibu wa sekta ya usafiri wa meli pamoja na hatua za kimataifa katika kukabiliana na hali hiyo;

d. Kushughulikia tatizo la meli zenye kutumia mfumo wa *ballast water* na kuhamisha viumbe kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine.

Nam. 11

Ongezeko la Nafasi za Wanawake Kupitia Udiwani

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Aliuliza:-

Napenda kuipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuongeza asilimia ya Nafasi za Wanawake katika Baraza la Wawakilishi kutoka asilimia 30 hadi 40. Ongezeko hilo limefanywa kupitia Marekebisho ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar ya 1984.

(a) Je, ni sababu zipi zilizopelekea kutokuongezwa kwa nafasi za Udiwani kupitia viti maalum na kubakia asilimia ile ile 30.

(b) Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iko katika mstari wa mbele kutetea wanawake. Je, ni lini inatarajia kuifanyia marekebisho Sheria Nam. 3 na Sheria Nam. 4 ya mwaka 1995 ili kutoa fursa kwa Madiwani viti maalum nao kufikia asilimia 40.

(c) Iwapo Serikali itazifanyia marekebisho sheria hizo na kuruhusu Madiwani viti maalum kuwa asilimia 40. Je, utekelezaji wake utaanza lini.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 11 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, sababu zilizopelekea kutokuongezwa kwa nafasi maalum za Udiwani na kubaki asilimia ile ile 30 ni kutokana na kutokufanyiwa marekebisho kwa vipengele vya Sheria Nam. 3 kifungu Nam. 4 (1) kwa Baraza la Manispaa na Halmashauri za Wilaya. Pia Sheria Nam. 4 ya mwaka 1995 kifungu Nam. 9 A (1) kwa Mabaraza ya Miji. Vifungu vyote hivi vya sheria vimezungumza juu ya ongezeko la Madiwani kwa asilimia 30.

(b) Mhe. Spika, ni kweli kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iko mstari wa mbele katika kutetea wanawake na ndio maana inajitahidi kuhakikisha kwamba haki, fursa na kila analostahili mwanamke kulipata basi analipata. Hali hiyo hiyo, ndio iliyoipelekea ofisi yangu kuanza mchakato wa kubadilisha Sheria Nam. 3 na 4 ili kuifanya idadi ya madiwani wanawake kufikia asilimia 40. Mswada wa marekebisho hayo unatarajiwa kufika katika Baraza lako tukufu mapema katika kikao kijacho.

(c) Mhe. Spika, utekelezaji wa marekebisho ya sheria hizo kwa kuongeza fursa ya madiwani wa viti maalum kufikia asilimia 40 utafanyika mara baada ya mabadiliko ya sheria kupitishwa kama ambavyo nimeeleza katika jibu (b).

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wanawake kila siku wanadai kuongezwa nafasi za viti maalum leo asilimia 40, kesho asilimia 50 na kesho kutwa asilimia 60.

Kwa kuwa wanawake wakiwezeshwa wanaweza. Kwa kuwa wanawake wanaweza wakavitawala hivi vyombo vya kutunga sheria likiwemo Bunge na Baraza la Wawakilishi pamoja na hizi ofisi za Halmashauri za Wilaya na Mabaraza ya Miji jambo ambalo wanaweza wakatawala maamuzi katika vyombo hivyo. Kwa kuwa serikali kila wakidai asilimia wanaongezwa. Je, isingekuwa vyema vikaanzishwa viti maalum vya wanaume. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, pili ili kuwajenga uwezo na kwa kuwa wakiwezeshwa wanaweza isingekuwa vyema hao akinamama wakaja majimboni wakawania viti vya majimbo kuliko kuendelea kung'ang'ania hivi viti vya kuteuliwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Labda nitoe muongozo kidogo. Hili suala la viti maalum vya wanaume hebu litafutiwe utaratibu wa kuuliza swali la msingi. Suala liliopo linahusu mambo ya viti maalum vya wanawake, kwa hiyo litafutiwe utaratibu wa kuuliza swali la msingi. Swali (b) Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, hili swali (b) sikulipata vizuri.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, kimsingi katika swali langu nilijenga hoja kwamba kwa kuhofia akinamama kutawala maamuzi katika vyombo hivi. Ili ku-*stabilize decision* ndani ya vyombo hivi yaani Mabaraza yasijekuwa *bias* katika maamuzi yakaegemea wanawake wakitaka jambo likawa linapita na wanawake tu. Ndio nikaomba kwamba serikali nayo ingeanzisha hivi viti maalum vya wanaume kwa makusudi ya ku-*balance decision within this house.*

Mhe. Spika, pili nilijenga hoja kwamba kwa sababu wanawake wakiwezeshwa wanaweza na kwa sababu wana nguvu, wana akili na wana maarifa ya kuweza kuwanasihi wananchi kuwachagua. Kwa mantiki hiyo, nadhani ili wasije wakadumaa kimawazo, kimaarifa na kwa nguvu, basi wangekwenda kwenye majimbo tukapambana nao ili kuweza kutunisha misuli nao kupambana na wanaume. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwanza nampongeza sana Mhe. Mwakilishi kuwa mtetezi mzuri sana wa wanaume. Lakini madhumuni makubwa ya marekebisho haya ni kuona kwamba kinamama ambao huko nyuma tumekuwa hatuwapi nafasi sasa tuwape nafasi.

Sababu kubwa sana tumegundua kwamba wana uwezo wakiwezeshwa kama ulivyosema. Wanaume ni kawaida kwamba tumekuwa tunawezeshana ndio maana tunaweza vizuri sana. Lakini ilikuwa hatuwawezeshi kinamama sasa serikali imegundua kwamba kuna vipaji vizuri sana hebu tuwape fursa. Sasa

hayo uliyoulizia yote ya uwiano mimi nafikiri uwiano upo tukiwawezesha wanawake tukiwanyanyua.

Moh'd Mbwana Hamad: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa madiwani ni miongoni mwa viongozi waliochaguliwa na wananchi kwa kura halali. Kwa kuwa madiwani wanafanya kazi katika wadi zao bila ya kuchoka asubuhi na jioni. Je, kuna sababu gani za msingi zilizopelekea kutokulipwa mshahara madiwani.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, suala hili serikali imekuwa ikilizingatia kwa kipindi sasa kuona namna gani tunaweza kuwasaidia Madiwani kimshahara. Bado tunalifanyia kazi nahisi tupe nafasi kidogo tulifanyie kazi tuone hatma yake kwa sababu hizi ni serikali zinazojitegemea. Sasa hili suala la kuwalipa mishahara naona tulitizame uwezekano wake ni namna gani tunaweza kulishughulikia, ahsante.

Nam. 29

Huduma za Wanafunzi Wanaolipiwa na Serikali

Mhe. Salmin Awadh Salmin – Aliuliza:-

Serikali imekuwa na utaratibu wa kuwalipia ada ya masomo wanafunzi wanaofaulu vizuri mitihani yao na kubahatika kuendelea na elimu ya juu ndani na nje ya nchi. Kwa kuwa Wizara yako imeomba kuingiziwa Tshs. 4.5 billioni katika mwaka huu wa fedha 2010/2011 kwa ajili hiyo, lakini hadi sasa fedha zilizoingizwa ni Tshs. 2.5 billioni tu.

(a) Kwa kuwa fedha zilizoingizwa ni karibu ya nusu ya zile zilizoombwa, Wizara yako imejipanga vipi kukabiliana na upungufu huo.

(b) Ni wanafunzi wangapi ambao wanalipiwa na Serikali kupitia utaratibu huo.

(c) Je, Wizara yako huwasiliana vipi na wanafunzi waliopo nje ya nchi ili kuelewa usumbufu wanaoupata ikiwa ni pamoja na kukosa kulipiwa ada kwa wakati.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 29 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

Kwanza napenda kutoa maelezo ya ufafanuzi kama hivi ifuatavyo.
Ni kweli kuwa serikali kwa kupitia mfuko wa elimu ya juu wa Zanzibar umekuwa ukiwapatia mikopo wanafunzi wanaosoma katika vyuo vya elimu ya juu. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011 bodi ya mfuko wa elimu ya juu iliomba kutengewa Shs. 4.5 bilion ili iweze kuwahudumia wanafunzi wote walioomba mikopo.

Hata hivyo, ni Shs. 2.5 bilioni ndizo zilizopitishwa na kutengwa kwa ajili ya utoaji wa mikopo, fedha hizo ni kasoro kwa Shs. 2.00 bilion na hazitoshi kuwahudumia wanafunzi wote.

Baada ya maelezo ya ufafanuzi Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo.

a) Fedha zilizoingizwa ni shillingi billioni 1.19 ambazo ni sawa na asilimia 47.6 ya fedha zote. Kama nilivyotangulia kusema fedha zilizoidhinishwa hazitoshi kuwahudumia wanafunzi wote. Hata hivyo Wizara yangu inafanya mazungumzo na Wizara ya Nchi (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kuangalia uwezekano wa kupatiwa fedha hizo za ziada.

b) Wanafunzi wote waliopatiwa udhamini wa serikali ni wanafunzi 1,349 kati yao 604 ni wanawake na 745 ni wanaume.

c) Wizara yangu inafanya mawasiliano ya mara kwa mara na uongozi wa vyuo vya nje ambavyo wanafunzi wetu tumewapeleka kusoma. Pia kupitia balozi zetu katika nchi za nje kufuatilia matatizo wanayoyapata wanafunzi wetu. Vile vile wanafunzi wenyewe hututumia barua pepe au hata kupiga simu pale wanapopata matatizo makubwa.

Napenda kutoa wito kwa wazazi wote wenye watoto wao katika vyuo vya elimu ya juu vya ndani na nje ya nchi, waendelee kushirikiana na serikali katika kuwapatia huduma vijana wetu ili waweze kusoma kwa utulivu. Ahsante.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri

Mhe. Spika: Ndio sababu ya kusema simu zizimwe kwa sababu ya tatizo hili, tujitahidi tufuate kanuni hiyo ya kuzima simu ili zisitutaabishe katika mawasiliano ndani ya ukumbi. Mhe. Ismail Jussa endelea.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo.

Naomba kusaidiwa kwamba wanafunzi wanaopatiwa mikopo hii ya elimu ya juu wanaosoma katika vyuo viliopo hapa Zanzibar wanakuwa hawapatiwi fedha kwa ajili ya makaazi kwa maana ya a*ccommodation,* usafiri na kwa ajili ya kununulia vitabu na vifaa kama hivyo, wakati wenzao wanaosoma vyuo viliopo Bara na kwengine wanapatiwa. Nilitaka kujua sababu ya kwa nini kunakuwa na tofauti katika kutolewa fedha hizi.

Kumekuwa na madai Mhe. Spika, katika nchi juu ya kuwepo kwa harufu ya rushwa katika bodi ya mikopo ya elimu ya juu, na kwamba mara nyengine hata taratibu hazifuatwi ipasavyo. Sijui wizara inalizungumziaje suala hili na kama lipo je, wizara ina mpango gani wa kufanya uchunguzi ili kukomesha tabia hii kama ipo, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli kwamba wanafunzi ambao wanaomba mikopo kwa vyuo vyetu vikuu vya Zanzibar huwa hatuwapatii fedha za makaazi na chakula.

(a) Mhe. Spika, hii inatokana na hali halisi ya uwezo wetu wa wizara kimikopo hiyo. Mahitaji yaliyokuwa ndani ya nchi Mhe. Spika, ni tofauti na mahitaji ya mwanafunzi aliyekuweko nje ya nchi, hana mjomba, shangazi wala hana kwa kwenda kuomba kule aliko.

(b) Mhe. Spika, sina uhakika na suala ambalo kalizungumza Mhe. Mwakilishi lakini popote pale panapofanywa kazi na wanaofanyakazi ni binadamu, na binadamu ana mapungufu yake. Inawezekana Mhe. Mwakilishi ikawa anazo taarifa zozote juu ya suala hili. Kwa hivyo, tunaomba ashirikiane na sisi, na tuna ahidi kwamba hatutolifungia macho wala hatutolionea haya suala hili, tutampeleka mtu mahakamani kama kweli atathibitika anafanya rushwa katika suala hili, ahsante sana.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya kutaka kukomesha rushwa aliyoyaahidi Mhe. Naibu Waziri, naomba kumuuliza swali moja dogo tu la nyongeza. Kuna tetesi pia kwamba wanaopatiwa mikopo hii ni wale wanafunzi wanaotoka katika skuli za serikali pekee. Wanafunzi wanaosoma katika skuli binafsi huwa hawapatiwi mikopo hiyo. Sasa nauliza je, ni kweli na kama ni kweli hawapatiwi ni kwa sababu gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, sio kweli. Wizara yangu inatoa mikopo kwa wanafunzi wote wanaohitaji mikopo hiyo.

Nam. 8

Hatua Zinazochukuliwa kwa Waajiri Wanaokiuka Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Sheria za nchi zimeweka masharti kwa wafanyakazi wote wa Serikali na Sekta Binafsi kujiunga na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa lengo la kuwasaidia pale watakapostaafu.

(a) Je, Wizara imechukua hatua gani kwa taasisi zinazoshindwa kufuata matakwa hayo ya kisheria kama vile Mashamba ya Mpira ya Kichwele, Mfenesini Selem na taasisi nyenginezo.

(b) Kwa kuwa wafanyakazi hao wa mashamba ya mpira wamekuwa wakisumbuliwa sana katika kupata haki zao, Wizara itawasaidia vipi wafanyakazi hao ili waweze kupata haki zao ikiwa ni pamoja na kupata mishahara na stahiki zao nyengine kwa wakati.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa heshima naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 8 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, kifungu nambari 18 cha Sheria ya Mfumo wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*) kinamtaka kila mwajiri kumsajili mfanyakazi wake katika kipindi cha siku 14 tokea kuanzishwa kwa taasisi hiyo. Aidha, Sheria ya *ZSSF* inamtaka mwaajiri kumkata mwaajiriwa wake asilimia 5 ya mshahara wa mwezi na mwaajiri kumchangia asilimia 10 ya mshahara wa mfanyakazi na kuuwasilisha mchango huo kila mwisho wa mwezi husika.

Mhe. Spika, kutomsajili mfanyakazi na kutowasilisha michango ni kosa kwa mujibu wa sheria na hupaswa kuchukuliwa hatua. Taasisi zinazoshindwa kutekeleza matakwa hayo ya kisheria, hatua zifuatazo huchukuliwa dhidi ya taasisi hizo.

(i) Kuifanyia ukaguzi (*audit*) taasisi husika ili kubaini idadi ya watumishi, tarehe walipoajiriwa, mishahara yao na mwenendo wa uwasilishaji wa michango yao kwa *ZSSF*.

(ii) Kuwaelimisha waajiri juu ya umuhimu wa michango ya waajiriwa wao na hatua zinazopaswa kuchukuliwa kwa mujibu wa sheria pale wanaposhindwa kuwasilisha michango yao.

(iii) Kuwajuulisha waajiri kimaandishi makosa yao na kuwataka wayarekebishe ikiwa ni pamoja na kulipa michango yote kwa mujibu wa sheria.

(iv) Kushitakiwa Mahakamani, pale muajiri anapokaidi kurekebisha kasoro zilizojitokeza.

Mhe. Spika, kwa upande wa shamba la mpira la Kichwele na Mfenesini Selem, hatua za ukaguzi na kuujulisha uongozi kasoro zilizobainika zimeshachukuliwa na uongozi wa *ZSSF* unafuatilia utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa.

(b) Mhe. Spika, kitendo cha kuwasumbua wafanyakazi wakati wa kuwapatia haki zao za msingi kama vile mshahara na stahili nyengine, hakiwezi kuleta tija katika uzalishaji kwa taasisi yoyote ile. Hivyo, serikali inapiga vita vitendo vya aina hiyo kwa faida ya wananchi na nchi yetu.

Kwa mnasaba huo sheria imeweka utaratibu wa kufuatwa na wafanyakazi pale wanapokosa haki zao kutoka kwa waajiri wao. Iwapo imeshindikana kupata ufumbuzi wa matatizo hayo, kupitia vikao vya uongozi na wafanyakazi au chama chao, wafanyakazi wanapaswa kuyawasilisha malalamiko yao Kamisheni ya Kazi ambayo ndio yenye jukumu la kusimamia utekelezaji wa sheria ya kazi, ikiwemo haki za wafanyakazi.

Mhe. Spika, napenda kumuomba Mhe. Mwakilishi, kuelewa kwamba jukumu la kusimamia moja kwa moja haki za wafanyakazi halipo katika Afisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Aidha, nawaomba pia wafanyakazi wa mashamba ya mpira na wengine wenye matatizo kama hayo, kufuata utaratibu huo ili kwa umoja wetu tuweze kuyapatia ufumbuzi matatizo yao. Hata hivyo, nawaomba waajiri nao wawe wanaheshimu haki za wafanyakazi wao kwa lengo la kuimarisha ufanisi mahali pa kazi na kuepusha migogoro isiyokuwa ya lazima.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja la nyongeza kwa Mhe. Waziri. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

Baadhi ya taasisi zinawakata wafanyakazi kima hicho katika mishahara yao, lakini wakati wa kupeleka katika mfuko wanapeleka baadhi ya miezi na baadhi ya miezi hawapeleki. Sasa mfanyakazi anapotimiza muda, akienda kufanyiwa hesabu zake inakuwa kuna kasoro kubwa.

(a) Je, suala hili ni nani wakufuatilia ili mtu aweze kupata haki zake sawa sawa.

(b) Sheria uliyoitaja ambayo inahusika na mfuko huu, kwa serikali mikataba yake ina muda maalum, mtu anastaafu miaka 55 ama 56, lakini taasisi nyengine watu wanajaza mikataba midogo midogo ya mwaka au miaka miwili anaachishwa kazi. Je, mtu kama huyu haki zake atazipataje wakati sheria ni mpaka ufike miaka 55, huoni kama inataka marekebisho.

(c) Umesema kwamba baadhi ya taasisi zisizofanya kikawaida kufuata sheria kulipa haki za wafanyakazi inapobidi, huwa inapata adhabu ili kuweza kujirekebisha na makosa yao. Je, ni taasisi ngapi zilizokuwa hazikutekeleza na zimepewa adhabu, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:

(a) Mhe. Spika, kwanza nataka nimuhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba wale ambao wanapeleka michango ya watumishi wao kwa vipolo, kwa maana mwezi huu wanapeleka na mwezi mwengine hawapeleki basi wako katika kosa kubwa sana kwa mujibu wa sheria. Taasisi hizo zinapaswa kuelimishwa na wanapaswa kulipa miezi yote ambayo watumishi wao walikuwepo kazini, kushindwa kufanya hivyo maana yake ni kupelekwa mahakamani.

(b) Mfanyakazi yeyote ambaye anaajiriwa kwa mikataba midogo midogo, yaani miezi sita baadae anakuwa hana kazi, baadae anakuwa anaajiriwa tena. Taasisi zinazomuajiri zinapaswa vile vile kupeleka michango yake. Pale ambapo wanapositisha uajiri, mfanyakazi na taasisi husika wanapaswa kuiandikia *ZSSF* kusema kwamba huyu sasa hivi sio muajiri wangu na yeye anapaswa kusema kwamba mimi sasa hivi sina ajira. Michango yake itasimama kwa kipindi kile na akipata ajira basi michango yake itaendelea.

Mhe. Spika, mwisho wa mwaka lengo la michango hii ni kumsaidia mfanyakazi pale ambapo atakapofikia miaka 55 au 60, pale atakaposema kwamba nastaafu kwa hiyari au nastaafu kwa lazima ili michango hii iweze kumsaidia. Kwa sababu tunaelewa unaweza ukawakuta watumishi wengine, sio lazima wapate ajira kwa kipindi chote cha maisha yake, anaweza akapata ajira kwa vipindi lakini michango yake kwa mujibu wa sheria inapaswa kuwasilishwa *ZSSF*.

(c) Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi ametaka kujua idadi ya taasisi. Nataka nimwambie tu kwa wakati huu kwa sababu ametaka takwimu sina, lakini ninaahidi nitampatia idadi ya taasisi hizo kama zipo.

Nam. 18

Ukataji wa Viungo kwa Wagonjwa wa Kisukari

Mhe. Salmin Awadh Salmin - Aliuliza :-

Kwa kuwa wagonjwa wa kisukari baadhi yao hulazimika kukatwa sehemu za viungo vyao kama vidole vya miguu au miguu yenyewe kutokana na matatizo ya vidonda vinavyosadikika kuwa na sumu. Kwa kuwa wengi wa wagonjwa wanaofanyiwa hivyo baada ya muda mfupi hufariki dunia.

(a) Je, Mhe. Waziri ni kwanini wagonjwa wa aina hii baada ya muda mfupi hufariki dunia.

(b) Katika kipindi cha mwaka 2009–2010 ni wagonjwa wangapi walikatwa viungo vyao kutokana na matatizo kama hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 18 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, maradhi yasioambukiza (*Non communicable diseases*) kisukari ikiwa ni moja wapo kwa sasa yanaathiri watu wengi hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, mwaka 2009 jumla ya wagonjwa wa kisukari 3,286 walionekana katika kliniki zetu Unguja na Pemba kati ya hao wagonjwa 464 walikuwa wapya.

Tatizo kubwa ni uelewa mdogo wa wananchi kuhusu tatizo hili, wagonjwa mara nyingi huchelewa kufika hospitali kiasi kwamba wakati mwengine uamuzi wa kukata kiungo unapofikiwa sumu huwa imeshasambaa mwilini.

Hivyo basi, matokeo mazuri ya upasuaji yatategemea namna mgonjwa anavyoidhibiti sukari yake na kuwahi hospotali atapoona dalili ya matatizo.

Mwaka 2009 hadi Novemba mwaka 2010, jumla ya wagonjwa 62 wamekatwa viungo kutokana na matatizo ya sukari. Kati ya hao wagonjwa 24 walifariki.

Mwaka:	**Wanawake:**	**Wanaume:**	**Jumla:**
Julai-Dise, 2009	2	3	5
Jan-Dise, 2010	12	7	19
Jumla:	**14**	**10**	**24**

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kwa kuwa baadhi ya wagonjwa au idadi kubwa ya wagonjwa huwa wanafariki pale wanapofanyiwa upasuaji wa kukatwa viungo vyao, upasuaji unaofanyika hapa Zanzibar. Lakini uzoefu unaonyesha kwamba kwa wale wenye nafasi za kutoka nje kufanyiwa upasuaji wa aina hii wao huwa hawafariki dunia.

Je, Mhe. Naibu Waziri huoni kuwa iko haja ya kufanya utafiti wa kina ili kuona kwamba upasuaji unaofanyika hapa pengine una matatizo kuliko ule upasuaji unaofanywa nje.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, sidhani kama hivyo anavyosema Mhe. Mjumbe ni kweli. Tuna madaktari wazuri wanaolifahamu suala hili vizuri. Ukimuona mgonjwa kaweza kwenda nje kwa pesa zake basi ujue hilo suala analifahamu mapema na uwezo anao na kawahi kufika huko hospitalini.
Mhe. Spika, wagonjwa wa hapa kwetu wanaokuja Hospitali ya Mnazi Mmoja nimeshasema katika utangulizi wa jibu mama kwamba kwanza hawafahamu hilo tatizo, na wanapokuja wameshachelewa. Kwa hivyo, hata kama utamfanyia upasuaji bado atakufa hata kama atapelekwa huko nje kwa wakati huo.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Spika, swali langu la nyongeza ni dogo sana. Napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri wa Afya kama ifuatavyo. Kojani ni kisiwa kama visiwa vyengine. Wakojani kisiwani walikuwa na tatizo la nyumba ya madaktari, kwa bahati nzuri nyumba ya daktari imeshamalizika karibuni miaka mitatu hivi sasa.

Je, Mhe. Naibu Waziri wizara yako ina mpango gani wa kutupatia madaktari wa kuweza kutoa huduma Kisiwani Kojani.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kabla sijamjibu swali lake. Mimi nafikiri kuna swali la msingi ambalo lilikuwa linatakiwa lijibiwe hivi ambalo sikupewa nafasi ya kulijibu kwa sababu muda ulikwisha.
Sasa kama anataka tulijibu hapa, ina maana huko mbele hatutoweza kulijibu hilo tena, na nina uwezo wa kulijibu. Sasa sijui maamuzi yakoje, nilijibu leo au utakuja kunipa nafasi huko mbele kwa nafasi nzuri tu nikufahamishe. Kama unataka leo niko tayari.

Mhe. Spika: Nafikiri kama ni suala ambalo angeuliza swali la msingi basi ni vyema ulivyomueleza kama ungepaswa kujibu swali la msingi ambalo halipo. Kwa hivyo, wacha tuendelee.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri ya kutaja takwimu ya wagonjwa wa sukari waliokatwa viungo mwaka 2009/2010, kinachoonekana Mhe. Spika, ni kwamba kuna hatari ya nchi hii kuwa na walemavu wengi baada ya muda mchache, kutokana na athari ya maradhi haya ya kisukari.
Mhe. Spika, nataka kumuuliza Mhe. Naibu Waziri Je, serikali ina mikakati gani ya kutokomeza maradhi haya kabla ya kufikia hatua ya watu kukatwa miguu na viungo vyengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, najua tuna hofu kutokana na haya matatizo kwamba walemavu watakuwa wengi. Mhe. Spika, kwenye swali la msingi nilizungumzia suala la uelewa mdogo wa wananchi. Lakini pia nataka niseme hivi, bado Wazanzibari tuna mwamko mdogo wa kupima afya zetu, tunapoambiwa kupima afya zetu hatumaanishi ni Ukimwi tu. Tunamaanisha ni kila kitu.

Mhe. Spika, Wazanzibari tunapima afya zetu pale tu tunapopewa karatasi za kutafuta ajira, kwa hivyo hapo ndipo unapokwenda ukapimwa sukari na maradhi mengine yote. Yanakuwepo matangazo mengi tu ya kupima sukari na hasa wanapoazimisha siku ya kupima sukari. Wanaokwenda pale huwa wanatambuliwa mapema na hatua zikichukuliwa mapema basi watu watakuwa hawafikii huko kukatwa miguu.

Kwa hivyo, naomba kwa kupitia nafasi hii kwamba Waheshimiwa Wawakilishi waelimisheni wananchi wenu. Ikiwa sukari utapima kila siku au kila wakati basi ikiwa imepanda kidogo itajulikana na ukipimwa ukijulikana unayo, basi utatibiwa kwa sababu matibabu yapo na hutofikia kukatwa viungo.

Kwa hivyo, ushauri wangu kwenu ni kwamba tupimeni ili tuweze kujua mapema na tusifikie kwenye huo ulemavu.

Nam. 14

Mmliki wa Jengo la Watoto Yatima Mazizini

Mhe. Salmin Awadh Salmin - Aliuliza:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibiwa swali langu, naomba kufanya masahihisho kidogo. Katika mstari wa pili wa swali kutoka chini, kuna neno "taasisi" libadilishwe na libakie kuwa ni neno "asasi". Kwa hivyo, isomeke kwamba "limejengwa na asasi isiyo ya kiserikali ya *ZAYADESA*".

Baada ya marekebisho hayo Mhe. Spika, naomba swali langu Nam. 14 lijibiwe.

Kwa kuwa Serikali imewahamisha watoto yatima katika nyumba ya Watoto yatima ya Serikali huko Forodhani na kuwapeleka katika jengo jipya liliopo Mazizini. Na kwa kuwa jengo hili jipya la Mazizini limejengwa na taasisi isiyo ya Kiserikali ya *ZAYADESA*.

(a) Je, Mhe. Waziri nani mmiliki wa jengo hili la Mazizini.

(b) Je. yapo makubaliano yoyote kati ya serikali na asasi iliyojenga jengo hilo.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 14 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mmiliki wa jengo la Kulelea Watoto Yatima Mazizini ni Jumuiya ya *ZAYADESA*.

b) Mhe. Spika, ndiyo kuna hati ya makubaliano ambayo imetayarishwa na wizara na kupelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushauri wa kisheria.

Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tayari imeifanyia marekebisho na kuirejesha wizarani kwa ajili ya kukamilisha taratibu zilizobakia, ili makubaliano hayo yaweze kutiwa saini na

pande zote mbili yaani Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto na *ZAYADESA*.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri wakati alipokuwa akijibu swali langu kipengele cha (a) alisema kwamba jengo ambalo tumewahamishia watoto yatima wa serikali ni jengo la asasi ya kiraia ambayo ni *ZAYADESA*.

Mhe. Spika, kwa kuwa jengo walilohamishwa watoto wa serikali ni la serikali na jengo ambalo wanaishi hivi sasa pamoja na uzuri wake na haiba yake, lakini ni la taasisi ambayo si ya serikali.

(a) Je, Mhe. Waziri kitendo cha aina hiyo inaweza ikafika pahala watoto wale wakakosa jengo la kuishi na kwa sababu jengo wanaloishi sasa si la serikali. *(Makofi)*

(b) Serikali katika mkataba ambao wamekubaliana na *ZAYADESA* kipo kipengele kinachozungumzia juu ya jengo lile kubadilishwa umiliki na kuwa jengo la serikali kuliko ilivyo sasa. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, naomba arudie swali lake kipengele cha (b).

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, wakati Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali langu kipengele cha (a) alisema kwamba yapo makubaliano katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu juu ya mikataba ya makubaliano. Je, katika makubaliano hayo yatamlazimisha mmiliki wa jengo hili, yaani *ZAYADESA* kulimilikisha serikali badala ya umiliki wake kama ulivyo hivi sasa.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, ahsante. Kwanza kabisa nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi pamoja na Baraza kwa jumla, kwamba *ZAYADESA* wamefanyakazi nzuri sana ya kupigiwa mfano ya kujenga jengo hili kwa ajili ya watoto yatima. *(Makofi)*

Kwa bahati nzuri sana wao wamekubali kwa hiari yao kwamba jengo hili litumike kwa ajili ya watoto yatima. Vile vile wamesema kuwa tukae pamoja na kukubaliana kwa masharti maalum ambayo ni masharti ya msingi kwamba jengo hili katika maisha yote tutakayokuwepo hapa, basi liwe linashughulika na watoto yatima na wala si vyenginevyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, jengo hili wenzetu wale walivyoona hali ya watoto kule walikokuwa Forodhani walikuwa wakibanana sana, hawajisikii hara na wala

hawana sehemu ya kucheza. Kwa hivyo, *ZAYADESA* ndipo walipoamua kujenga jengo hilo.

Kwa kweli hawana tamaa ya kusema jengo hilo baadaye walifanyie mizengwe ili lirudi kwao. Isipokuwa jambo kubwa ni kuona kwamba je makubaliano haya yaliopo wakati tutakapokaa pamoja na kukubaliana hivi jengo hili litaendelezwa kwa ajili ya shughuli za ulezi wa watoto yatima. Vile vile suala la usafi wa jengo utaendelezwa na kuimarishwa pamoja na mahitaji wa watoto wetu yatima yatakamilika kama vile chakula, nguo pamoja na mambo mengine. *(Makofi).*

Mhe. Spika, *ZAYADESA* wako tayari kushughulika na kuwasaidia watoto yatima pamoja na sisi wizara tutakuwa bega kwa bega kwa upande wetu katika kulishughulikia jengo hilo. *(Makofi)*

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba niulize swali lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Jengo la Kulelea Watoto Forodhani ni jengo la kihistoria je hivi sasa linafanyiwa shughuli gani. *(Makofi)*

Hivi sasa katika jengo hilo kumeanzishwa biashara za mikahawa na wageni wengi wanakwenda sehemu hiyo kwa lengo la kupata huduma. Je, mikahawa hiyo inadhibitiwa na nani na mapato ya pale yanakwenda sehemu gani. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, jengo la Forodhani kwa vyovyote linavyotumika lakini ni jengo la serikali tena la zamani sana na lipo mikononi mwa serikali, licha ya kuwa kuna mikahawa pamoja na mambo mengine, lakini ni jengo la serikali. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, wakati Mhe. Mjumbe alipouliza swali alijata kuhusu mapato yanayopatikana yanakwenda wapi.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, bila ya shaka wakati tunapofanyabiashara hasa kwa serikali hii ya Umoja wa Kitaifa haina mchezo kunakuwa na taratibu zake. Kwa hivyo, mapato yatakayopatikana bila ya shaka yatakusanywa na kupelekwa serikalini, kwa kweli serikali haikosi kitu ni lazima ipate mahitaji yake. *(Kicheko/Makofi)*

Nam. 3

Matengenezo ya Uwanja wa Amani

Mhe. Ali Abdalla Ali – Aliuliza:-

Baada ya jitihada kubwa kuchukuliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, katika kuufanyia matengenezo makubwa uwanja wa Amani, ambao kwa sasa upo katika hali nzuri.

(a) Je, wafanyakazi waliopo sasa wanakidhi haja ya kuutunza na kuuendeleza uwanja huo.

(b) Je, wizara ina mpango gani wa kuifanyia matengenezo makubwa Hoteli ya uwanja huo, ambayo kwa sasa haiko katika hali nzuri, ili iende sambamba na hadhi ya uwanja huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 3 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ukweli ni kwamba wafanyakazi waliopo uwanjani hivi sasa hawakidhi haja ya kuutunza na kuendeleza uwanja huo, bali taratibu zinafanyika kuwarejesha wale wafanyakazi waliohamishwa, ambao hapo awali walikuwepo lakini kwa sasa wamepelekwa taasisi nyengine zilizomo ndani ya wizara yetu wakati matengenezo yalipokuwa yakifanyika.

(b) Mhe. Spika, Hoteli haikuwemo katika matengenezo wakati uwanja ulipofanyiwa matengenezo makubwa. Kwa kutambua hilo wizara imeanza kufanya juhudi za kuifanyia matengenezo kwa kuipaka rangi eneo la nje na vyumbani. Pia imedhamiria kubadilisha samani, vitanda na kutia televisheni, *aircondition* na *mini refrigerators* iwe kivutio kwa wageni na wanamichezo, ili kuifanya iende sambamba na hadhi ya uwanja.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali moja lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Tulitegemea baada ya matengenezo makubwa ya Uwanja wa Amani kwamba gwaride halitofanyika tena katika uwanja ule, kwa sababu gwaride ilikuwa ni miongoni mwa matatizo ya kuuharibu uwanja ule hasa sehemu ya *tartan*. Je serikali ina mpango gani wa kutafuta uwanja mwengine kwa ajili ya gwaride tu na ule uwe kwa ajili ya michezo.

(b) Hivi karibuni katika Mashindano ya Kombe la Mapinduzi, timu za Yanga na Simba ziliingia kwenye fainali na mchezo huo ulifanyika usiku, lakini uwanja ulifurika na watu wengine kubakia nje. Je, wizara ina mpango gani wa kujenga uwanja unaokidhi haja kwa hivi sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, serikali ina mpango maalum wa kutafuta kiwanja na kujenga kwa ajili ya kuhimili vishindo vya gwaride.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwanza sina budi kutoa shukurani kwa kupata fursa hii ya kutoa ufafanuzi zaidi juu ya swali ambalo limeulizwa na Mhe. Mjumbe. Kwa kweli serikali imefanya juhudi ya kutatua suala hilo la kuunusuru uwanja na imetupa maagizo kwamba tutafute maeneo mengine kwa ajili ya kujenga kiwanja chengine ambacho tutakiita *multipurpose*.

Kwa hivyo, kwa upande wa wizara tumechukua juhudi hizo na tayari tumeshawasiliana na wizara husika ambayo ni Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, ili kutupatia maeneo kadhaa na baadaye tuweze kufanya upembuzi na kuona sehemu ipi ambayo ni muafaka kwa lengo la kujenga kiwanja hicho ambacho kitakidhi mambo yote.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Uwanja wa Amani ni mkubwa tena wa kitaifa hapa Zanzibar, pia uwanja huu umefanyiwa matengenezo makubwa sana na umekuwa mzuri wa kupendeza. Je, Mhe. Waziri ana mpango gani wa kuvitengeneza viwanja vilivyomo kwenye wilaya ndani ya nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, nikushauri uulize swali la msingi na hapa tubakie na suala la Uwanja wa Amani tu. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Kwanza naipongeza Wizara ya Habari, Utamaduni, na Michezo iliyopita kwa kufanyakazi kubwa sana ya kuweza kututafutia ufadhili Uwanja wetu wa Amani na kubadilika kuwa wa kisasa kabisa.

Lakini hali ambayo iliopo hivi sasa ya mazingira ya nje ya uwanja. Kwa mfano, tukiangalia nyuma ya hoteli kuna uharibifu mkubwa sana wa mazingira katika suala la uchimbaji wa mchanga. Vile vile sehemu ya mbele ya uwanja kuna uchafuzi mkubwa wa mazingira pia na naweza kusema hivyo, kutokana na watu kuweka biashara zao ovyo, yaani kiholela bila ya utaratibu maalum.

(a) Je, uongozi wa wizara una utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba wale watu ambao wamejipeleka mbele ya Uwanja wa Amani wanaondosha, ili pale pawekwe mazingira mazuri ya bustani na kuweza kuleta haiba ya Uwanja wa Amani.

(b) Lakini katika eneo la nyuma watatumia utaratibu gani, kuhakikisha lile eneo la nyuma unazuiliwa ule uchimbaji wa mchanga, ili ile jitihada na nguvu za wafadhili wetu wasijekuvunjika moyo na baadaye kushindwa kutusaidia.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ni kweli nakubaliana naye kwamba upo uharibifu mkubwa wa mazingira hasa upande wa nyuma ya uwanja wetu. Kwa kweli suala hili tayari tumeshazunguumza na Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi kuhusiana na ulinzi wa mazingira yale, lakini bado hatujapta *feedback* mpaka sasa na tunaendelea kuwasiliana naye, ili kuhakikisha kwamba pale hakuna uchimbaji wa mchanga unaoendelea.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, wakati Mhe. Mjumbe alipouliza swali alitaja na sehemu ya mbele ya Uwanja wa Amani vipi kuhusu wafanyabiashara.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kuhusu wafanyabiashara tutachukua hatua za kuwaondosha pale, kwa sababu hata na mimi linanikera. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na Mhe. Waziri naomba kutoa wito maalum kwa Waheshimiwa sisi tunaoshughulika na Tawala za Mikoa juu ya suala zima la kusimamia uchimbaji wa mchanga.

Mhe. Spika, nadhani Mhe. Hamza Hassan Juma pamoja na Mhe. Salmin Awadh Salmin watakubaliana na mimi, hawa wachimbaji wa mchanga wengi wanatokea majimbo yao na hao ni wananchi wetu.

Kwa hivyo, ninashauri sana na kuwaomba watusaidie kwamba kuiachia serikali mambo yote si rahisi. Kwa kweli wachimbaji hao wanakwenda saa 8 za usiku au 11 za alfajiri, yaani wakati unapoamka asubuhi tayari uharibifu umeshafanywa. Kwa hiyo, hili Mhe. Spika ni letu sote na Mhe. Hamza anawafahamu ndio wapigakura wetu hawa na mambo mabaya tuwakataze.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, kabla sijajibiwa swali langu naomba nitoe ufafanuzi kidogo, wachimbaji wa mchanga wanatokea Jimbo la Chumbuni na kuja Magomeni kuchimba mchanga.

Nam. 28

Ukarabati wa Chinjio la Kisakasaka

Mhe. Salmin Awadh Salmin – Aliuliza:-

Mhe. Waziri, hali ya Chinjio Kuu la Kisakasaka haliridhishi hata kidogo. Kwa kuwa serikali katika mwaka huu wa fedha imeazimia kulifanyia matengenezo, ili liendane na wakati ikiwa ni pamoja na kupeleka umeme na kuzungusha uzio katika eneo la karantini.

(a) Je, Mhe. Waziri, ni hatua zipi zilizotekelezwa hadi leo hii.

(b) Kama bado unawaahidi nini wananchi wa Zanzibar.

(c) Je, suala la kuanzisha eneo la karantini ya wanyama huko Pemba litatekelezwa lini.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 28 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli hali ya Chinjio Kuu la Kisakasaka hairidhishi. Wizara yangu ina dhamira na azma ya kujenga chinjio la kisasa hali ya fedha itakaporuhusu. Hata hivyo, kwa kulihami chinjio lililopo hatua zifuatazo zimechukuliwa:-

(i) Chinjio hilo limefikishiwa umeme katika maeneo yote.

(ii) Hali ya upatikanaji wa maji imeimarishwa zaidi kwa kupatiwa maji ya uhakika kutoka Mamlaka ya Maji na pia

kuimarisha kisima cha maji kiliopo eneo la chinjio, kwa kukifikishia umeme pamoja na kuifanyia matengenezo pampu ya kisima hicho.

(b) (i) Kazi ya matengenezo ya jengo lenyewe la chinjio kwa kukarabati sakafu yote ya chinjio, kuweka *tiles*, kurekebisha mfumo wa maji na ukarabati wa mitaro na vyoo haijaanza.

Hata hivyo, ninachowaahidi wananchi wa Zanzibar ni kwamba mwanzoni mwa mwezi huu wa Januari zabuni za matengenezo hayo imeshatangazwa na utaratibu wa kumpata mkandarasi unaendelea. Hivyo, wakati wowote kuanzia sasa taratibu za zabuni zikishakamilika, fedha tayari zipo na matengenezo yataanza.

(iii) Hali ya ujenzi wa uzio kuzunguka eneo lote la karantini haijakamilika. Wizara yangu ina mpango wa kwanza kulifyeka eneo lote la karantini, kulipima eneo hilo na kupata hatimiliki, na baadaye ndio taratibu za kuweka uzio zichukuliwe. *(Makofi)*

(c) Mhe. Spika, wizara yangu hivi sasa imo katika mpango wa kuanzisha karantini ya mifugo Pemba. Hivi karibuni nilipofanya ziara ya kutembelea sehemu mbali mbali za Wizara Pemba, wataalamu wangu walitembelea maeneo ya Tundauwa, Nziwengi, Sizini na Vikutani, ambapo wizara itaamua eneo la kuanzisha karantini baada ya kuyafanyia tathmini na kuwasiliana na taasisi nyengine zinazohusika.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali langu la msingi ameeleza kwamba tayari suala la kupeleka umeme katika chinjio limeshafanyika.

(a) Je, kazi ya kupeleka umeme katika chinjio imefanywa na kampuni gani.

(b) Kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi wa Kisakasaka kwa kampuni iliyopewa kazi ya kupeleka umeme katika chinjio, kwamba tayari aliyepewa kazi amechukua fedha na amekimbia.

(c) Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba anipangie siku ili tufuatane mimi na yeye kwa lengo la kwenda kukagua shughuli hiyo kama kweli imefanyika au laa. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, namuomba Mhe. Mjumbe arudie kipengele cha (b) katika swali lake.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, tafadhali rudia kipengele cha (b) katika swali lako.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, kipengele cha (b) katika swali langu kinasema hivi, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi wa eneo la Kisakasaka, ambao pengine na wao wangelifaidika kwa kupelekwa kwa umeme kwenye eneo hilo, kwamba huyu mkandarasi wa kupeleka umeme tayari amechukua fedha na amekimbia na hivi sasa haonekani.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika,

(a) Kampuni iliyopewa kazi ya kupeleka umeme inaitwa *OSAJU* au na shughuli za kupeleka umeme zimegharimu shilingi milioni 152.

(b) Si kweli kwamba kampuni imeshapewa fedha na imeshakimbia. Kwa kweli malipo ya shughuli hii yalikuwa ni kwa awamu tatu na hivi sasa tayari malipo ya awamu mbili yameshafanyika na karibu shilingi milioni 50 bado hajalipwa, mkandarasi amekuja kwangu anataka alipwe na nimeagizwa kwamba hawezi kulipwa mpaka wizara ijiridhishe kwanza na *quality* ya kazi yenyewe. *(Makofi)*

(c) Wakati wowote Mhe. Mwakilishi akiwa Mjumbe na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi afisi yangu iko tayari wakati wowote tupange twende Kisakasaka kwa ajili ya kukagua ujenzi na huo ni wajibu wangu, kwa hiyo Mhe. Spika niko tayari. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nadhani tuendelee kwa sababu muda wangu ni mdogo na maswali ni mengi.

Nam. 91

Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ya Muungano

Mhe. Omar Ali Shehe – Aliuliza:-

Shughuli za ukaguzi na udhibiti wa fedha za umma kwa taasisisi zote za muungano hufanywa na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania.

Kwa kuwa Afisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Tanzania Bara si Taasisi ya Muungano; na kwa kuwa matumizi ya fedha za umma zinapaswa kufahamika kwa pande zote za muungano.

a) Je, ukaguzi unaofanywa na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Tanzania Bara katika Taasisi ya Muungano unamuhusishaje Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu wa Zanzibar.

b) Baraza la Wawakilishi kwa niaba ya wananchi lina nafasi gani ya kujua/kufuatilia matokeo ya Ripoti ya Ukaguzi unaofanya na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi unaofanywa na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Tanzania Bara katika Taasisi za Muungano.

Mhe. Waziri Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 91 kama hivi ifuatavyo:-

Kwanza kabla ya kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yapo kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar na ile ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Shughuli zake zinasimamiwa na Sheria Nam. 11 mwaka 2003 kwa upande wa Zanzibar na Sheria ya Fedha za Umma Nam. 6 mwaka 2001 kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, vyombo hivi vinatakiwa kuidhinisha utoaji wa fedha kutoka Mifuko Mikuu ya Serikali hizi. Vile vile kuhakikisha kuwa matumizi ya serikali yanafanywa kwa mujibu wa sheria na kukagua mapato na matumizi ya serikali na vyombo vyake kila mwaka pamoja na kuandaa ripoti ambazo huwasilishwa serikalini na Baraza la Wawakilishi kwa upande wa Zanzibar na Bunge kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar sehemu ya mapato yake yanatokana na shughuli za vyombo vya muungano vilivyopo hapa Zanzibar. Aidha Serikali ya Mapinduzi inagharamia baadhi ya kazi za vyombo hivyo, kwa msingi huo Baraza la Wawakilishi linapaswa kupata ripoti ya ukaguzi wa vyombo hivyo hasa kwa upande wa Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

a) Ukaguzi unaofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ya Muungano haumuhusishi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar isipokuwa katika baadhi ya miradi ya maendeleo kama vile mradi wa UKIMWI na *MACEMP*.

b) Kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ya awali, ni vyema Baraza la Wawakilishi likajua matokeo ya ukaguzi unaofanywa katika vyombo vya Muungano hasa kwa upande wa Zanzibar. Kazi iliyopo mbele yetu ni kuwasiliana na wenzetu wa Jamhuri ya Muungano ili kuona utaratibu bora utakao mjumuisha Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu Zanzibar katika ukaguzi ili taarifa kuhusu vyombo hivyo ziweze kuwa ni sehemu ya ripoti yake ya mwaka atakayoiwasilisha kwenye Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe muda wa maswali umekwisha na leo ni Ijumaa, jana tulifanya utaratibu angalau tukaomba wajumbe waongezewe muda kumaliza maswali, hoja iliyopo mbele yetu ina wajumbe wengi walioomba kimsingi kumekuwa na marejeo ya jambo hilo. Lakini mawaziri wengi wameguswa guswa hapa na pale katika hoja ile, ingefaa basi mawaziri wale waje wapate nafasi na kwa hivyo tupate muda mchache uliobaki kupunguza wale wajumbe, lakini jioni tuweze kufanya majumuisho kwa mawaziri wengine kumsaidia mtoa hoja ili tuweze kumaliza hoja hii leo kama ilivyopangwa.
Kwa hivyo leo tusiongeze muda kwa sababu ni Ijumaa ni siku fupi.

HOJA ZA SERIKALI

Hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Aliyoitoa katika Uzinduzi wa Baraza la Nane la Wawakilishi Zanzibar Tarehe 11/11/2010

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe kama nilivyosema tuna wachangiaji kumi waliobaki ukiachia mawaziri, tuna muda wa saa moja na nusu kumaliza

mchango huu kwa wajumbe, tukitoa dakika kumi na tano kumi na tano tunapata wachangiaji sita. Tukubali kama wachangiaji kama ishirini na tatu watasaidia pamoja na wale sita ambao tutawapa nafasi kufanya jumla ya ishirini na tisa, tukipunguza zaidi ya hapo kwenye kumi na tano basi namudu kuchukua wachangiaji wengi zaidi sasa uchangiaji uende si zaidi ya dakika kumi na tano, nitawajulisha mara baada ya dakika kumi za kwanza halafu baadae tumalize dakika tano kama mjumbe hajamaliza shughuli yake ya kuchangia.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na mimi kwanza nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa asubuhi hii ya leo ambayo nimepatiwa ruhusa hii ya kuchangia hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, haitokuwa vyema na mimi kama sikutoa pongezi za dhati kabisa kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa hotuba yake hii mwanana ambayo ndio dira ya kuweza kutuongoza kufanikisha shughuli zetu kwa taifa letu hili la Zanzibar.

Lakini pia nichukue nafasi hii kwa kukupongeza wewe mwenyewe binafsi kwa kuwa nasi tena katika baraza hili tukufu kama ni Spika wetu wa Baraza la Wawakilishi, niwapongeze Mawaziri wote ambao wameteuliwa kwa mujibu wa taratibu kuweza kuendesha shughuli mbali mbali za serikali.

Mhe. Spika, na mimi nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitowashukuru wanawake wote wa Tanzania hii ambao walionichagua kuwa Makamo Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania na ndio nafasi iliyoniwezesha kuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, nawaahidi nitawatumikia kwa moyo wangu wote na kuwatetea wote pale inapohitajika.

Mhe. Spika, sasa niendelee kwa sababu mambo mengi yalichangiwa kuanzia jana, lakini na mimi nitatoa dondoo nitasema yale ambayo nahisi yataweza kusaidia yale mengine ambayo hayajachangiwa. Mimi naingia moja kwa moja katika utalii tumejionea wenyewe hapa shughuli za utalii na sasa hivi tunasema ndio uti wa mgongo wa kuweza kutupatia fedha za kuendeshea mambo mbali mbali ya serikali, lakini natoa ombi kwamba siku za nyuma tulivamiwa sana na tulikuwa bado hatujawa wataalam na mambo haya ya utalii, naomba kisiwa cha Pemba tujitahidi kisije kikavamiwa kama Unguja, kuna taratibu mbali mbali ambazo tunatakiwa tuzikamilishe ndio tuvamie kisiwa cha Pemba.

Mhe. Spika, huko nyuma tumeona jinsi tulivyovamiwa kwenye kisiwa cha Unguja kwa mambo ya utalii na kuna matatizo mengi sana ambayo tunayaona sisi wenyewe sasa hivi yanajitokeza, kwa hivyo naiomba sana wizara husika

tuhakikishe kisiwa kile cha Pemba kiwe ni *power dive* ili tuweke utalii wetu wenye uhakika na usioleta mazingira potofu katika kisiwa kile, hapo nilisema nichangie kuhusu habari ya utalii.

Lakini pia nije katika kilimo, kilimo pia tunasema ni uti wa mgongo lakini kutokana na hali halisi ya mazingira yanavyochafuliwa Mhe. Spika, sifikirii kwamba hiki kilimo kweli tutakihitaji kuwa mti wa mgongo, mimi nitagusia kidogo tu kwa sababu wenzangu wamechangia sana. Naomba sana nguvu zetu zote tuzielekeze kwanye uchafuzi wa mazingira.

Mhe. Spika, mimi nitatoa mfano ulio hai kwa shehia yangu ya Mtambwe. Mhe. Spika, katika shehia kubwa Pemba ni shehia ya Mtambwena ilikuwa naweza kusema ni kitovu ambacho hakijaweza kuchafuliwa kimazingira, lakini sasa hivi Mtambwe huwazi kuamini jinsi ilivyovamiwa kwa kukatwa miti ya asili, naiomba sana Wizara hii na mimi nitakuwa tayari kushirikiana nao waziri anayehusika twende Mtambwe tukaangalie ni jinsi gani mazingira yalivyochafuka.,

Mhe. Spika, nikiondoka hapo kwa sababu wenzangu wameshachangia changia nije kwenye elimu wenzangu wamezungumza mambo mbali mbali ya elimu, lakini mimi nitakuja kwenye vipaji. Mhe. Spika, kama unakumbuka hata huko nyuma nilivyokuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi nilisema kwamba kuna haja Wizara ya Elimu tukaweza kupima vipaji vya kila mtoto na kuhakikisha kwamba huyu ana kipaji hiki na huyu hiki ili kuwakusanya kwa pamoja kwa mujibu wa vipaji vya wanafunzi vilivyo, wenzangu walizungumza hapa kama kweli tunataka tusomeshe mambo ya sayansi na teknolojia au tunataja tu ukweli tutapata tabu sana kwa vijana wetu hawa.

Mhe. Spika, sasa nakuja kwenye Afya, hii ni Wizara ambayo ndio mama kwa binaadam na wizara baba kwa binaadam katika kiwili wili chake, ningeomba sana Mhe. Waziri aiangalie tena wizara hii na hasa kwenye *scheme of service* za wafanyakazi wake. Mhe. Spika, wenzangu wamezungumza hapa tulikuwa na madaktari wengi lakini kutokana na kutowapa yale marupu rupu ambayo yanatakiwa yamfanye daktari atulizane aweze kuwa daktari bora tulijisahau, lakini nishukuru kwamba kidogo tume *improve* katika masuala haya.

Lakini nakuja kwenye wafanyakazi ambao ukitoka daktari unakuja *staff nurse* halafu unakuja *orderly* hawa nao naomba Wizara iwafikirie mishahara yao, ili na wao kuwapa moyo katika shughuli zao kwa sababu na wao hawa pia ni mojawapo ambao wana maatizo makubwa sana ya kuweza kufanya shughuli hizim, naomba sana waziri alitizame kwa jicho la huruma.

Mhe. Spika, sasa nakuja kwenye safari za anga namuomba mheshimiwa anyehusika hebu kuna kipi ambacho kila siku hizi safari za anga, leo hivi sasa tiketi ya kwenda Pemba ni elfu thamanini kweli jamani na kila siku bei zinapanda tunajua kweli hali halisi lakini kila siku hakuna mfumo maalum hilo moja, wewe ni binaadamu unakata tiketi unataka kwenda zako Dar es Salaam au Pemba unaweza kutokezewa na dharura, unaambiwa tiketi ile haifai hata ukisema vipi pesa zako zimekwenda arijojo. Naomba Waziri anayehusika na suala hili atuletee taarifa ni kitu gani ambacho kinapandisha nauli kwa kila leo, namuomba sana Mhe. Waziri kwa sababu wenzangu wamechangia.

Tuje usafiri wa baharini. Mhe. Spika, kwanza nipongeze hawa wafanya biashara ambao wamejitahidi kuleta vyombo hivi vya usariri wa baharini, lakini naomba sana Mhe. Waziri aviite vyombo vyake vya usafiri wa baharini kuhakikisha usalama wa wananchi wetu katika visiwa hivi, matokeo ya kila wakati yanajitokeza kwamba leo imebururwa meli kutoka wapi mpaka wapi, leo meli imekaa haiwezi. Hivyo kweli hivi vipando vyetu vya usafiri wa baharini havina kima maalum ya kuchukua abiria, kuna siku hapa tutakuja kulia kiliocha mbwa mdomo juu, naomba sana Mheshimiwa anayehusika na vyombo vya baharini vyombo vimewekewa muda gani wa kukaguliwa.

Mhe. Spika, nije usafiri wan chi kavu. Mhe. Spika, na mimi niunge mkono mwenzangu muwakilishi wa jimbo la Mtambwe aliyetilia mkazo ile njia ya Mtambwe, namuomba sana Mhe. Waziri afanye jicho la huruma njia ile ili iweze kuengenezwa katika Pemba Shehia kubwa sana basi ni shehia ya Mtambwe na karafuu nyingi sana zinatoka kule, mazao mengi sana yanatoka kule lakini matokeo yake tuna matatizo makubwa sana ya usafiri.

Mhe. Spika, natoa mfano kidogo tu nistahamilie. Mheshimiwa aliyekuwa Waziri wa Elimu iliyopita alikuja shehia ya Mtambwe wakati wake ulimuiya mgumu sana alikuja na gari kutizama maendeleo gani yapo katika skuli zile, matokeo yake Mhe. Waziri alikwamba na gari lote lilizama kwa sababu udongo wa njia ya kwendea Mtambwe ni mbaya mno na njia zote zina udongo huo. Wakati ikinyesha mvua huwezi kufika pahala popote naomba sana Mhe.Waziri atupie jicho la huruma ili njia hii ya Mtambwe ifanyiwe matengenezo haraka sana.

Mhe. Spika: Mheshimiwa una dakika mbili tu.

Mhe. Asha Bakari Makame: Kwa kumalizia niseme mwisho kabisa kwa heshima kubwa nawaomba waheshimiwa wenzangu wa Baraza la Wawakilishi kwamba sisi tuwe mfano, kwa kuwatumikia wananchi kwa kuwatetea na kulinda yale maamuzi ambayo tunaamua katika baraza lako hili tukufu.

Baada ya kusema hayo japokuwa sikumaliza lakini naheshimu naunga mkono hoja hotuba hii ya Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwa mara nyengine nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukaa hapa tukiwa na afya njema. Mhe. Spika, mimi nataka niseme kwamba hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliyoitoa hapa Barazani kwa kweli ni hotuba ambayo ina dira na mwelekeo wa maendeleo ya nchi yetu, imani yangu nina matumaini makubwa sana kwambanchi yetu itapiga maendeleo makubwa sana .

Mhe. Spika, nikianza na mchango wangu nataka nimshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa na wananchi wa Zanzibar kuweza kuiongoza Zanzibar ili kuweza kupata maendeleo ya kutosha kabisa, kama alivyotupongeza Mhe. Rais na mimi nataka nichukue nafasi hii kukupongeza wewe kwanza kwa kuweza kuchaguliwa kuwa spika wetu, lakini vile vile kuwapongeza na waheshimiwa wenzangu wote kwa kuchaguliwa na wananchi wao katika majimbo yao kwa ajili ya kuongoza.

Mhe. Spika, na mimi pia nataka nichukue fursa hii kuwashukufu wananchi wangu wa jimbo la Kwamtipura kwa kuweza tena kunipa ridhaa kuweza kuliongoza Jimbo letu la Kwamtipura, nawaahidi nitafanya kazi kwa mujibu wa uwezo wangu nitatumia maarifa yangu yote niliyokuwa nayo na uzoefu kuhakikisha kwamba ninawatumikia vizuri kwa maslahi ya taifa letu.

Nikiendelea na mchango wangu nataka nianze moja kwa moja katika suala zima la ukurasa wa saba Mhe. Rais alivyotuasa sisi waheshimiwa kuweza kuwajibika kwa mujibu wa katiba na sheria katika kuongoza majimbo yetu, tunamuahidi kwamba tutatekeleza majukumu yetu kwa mujibu wa katiba ya Zanzibar na sheria za nchi hii. Mimi nimpongeze sana Mhe. Rais kwa namna alivyoahidi kuweza kutatua kero ambazo zinawakabili wananchi wetu, ameeleza katika hotuba yake kwamba karibu asilimi 75 sasa hivi wananchi wanapata huduma muhimu yakiwemo maji pamoja na umeme, lakini kama walivyosema wenangu bado katika Mkoa wetu wa Mjini Magharibi tatizo la maji ni kubwa.

Mhe. Spika, jana kuna mheshimiwa mmoja alizungumza hapa ni vizuri tunapochangia hizi bajeti mawaziri wote wakawepo lakini kwa bahati kuna baadhi ya mawaziri wengi sasa hivi hawapo, lakini naamini waliokuwepo watafikisha huu ujumbe kwa mawaziri waliokuwa hawapo.

Mhe. Spika, bado sijaridhika na utendaji wa maji katika Mkoa wa Mjini na Magharibi, tatizo la maji ni kubwa kama walivyosema wenzangu mradi mkubwa sana wa Japan serikali imetumia pesa nyingi lakini bado matatizo makubwa ya maji yapo, na mimi nathubutu kusema kwamba ni uzembe wa wafanyakazi kwa sababu haiwezekani katika maeneo hakuna uhakika wala hakuna ratiba maalum ya upatikanaji wa maji, basi angalau ingekuwa wananchi wanajua kila baada ya siku tatu tunapata maji ili wakaweza kujiwekea hakiba nzuri ya maji.

Lakini Mhe. Spika, hasa katika shehia yangu ya Kwamtipura watu wanahishi hawana uhakika wa maji, wanaweza kupata maji katika mwezi siku tatu siku zilizobakia maji yanapotea, kuna siku nyengine wanaweza kupata wiki nzima siku zilizobakia hayapatikani, hili suala la maji chupu chupu linikoseshe jimbo. Sasa nasema sitoendelea kukubali kusulubiwa na wananchi wangu wakati serikali imeshafanya jitihada zote, kwa hivyo namuomba sana Waziri wa maji kama walivyosema wenzangu. Namuomba sana waziri anayeshughulikia masuala ya maji tutafanya nae kazi bega kwa bega lakini ahakikishe kwamba wafanyakazi wake wanawajibika vizuri.

Mhe. Spika, naendelea na mchango wangu imeelezwa hapa katika ukurasa wa kumi kuna pato la taifa, katika takwimu zilizofanywa katika mapato na matumizi ya kaya takwimu za mwaka 2004/2005 imeeleza karibu ya watu 49% wanaishi katika hali ya umasikini, ukiangalia wastani wa pato la taifa na kipato cha mwananchi wa kawaida bado hakiridhishi sasa tunaiomba serikali yetu bado kuna maeneo mengi ambayo tukifanya jitihada tukiweza kuzuia mianya ya uvujaji wa fedha za serikali basi mimi naamini tunaweza kufanikiwa. Sasa hivi wastani wa mwananchi anapata shilingi elfu sitini kwa mwezi mimi nikiwa na shilingi elfu sitini siwahi kuondoka nyumbani pesa hizo vinamaliza, sasa hili ndio pato la wastani wa mwananchi wa Zanzibar.

Kwa hivyo tunaiomba serikali kufanya jitihada zake kuhakikisha kwamba maendo yote ambayo kuna uvujaji wa fedha za serikali basi tuweze kuhakikisha kwamba fedha zinapatikana.

Mhe. Spika, ukurasa wa kumi na mbili tunamshukuru sana Mhe. Rais alielezea kwamba ataimarisha serikali za mitaa na tunaomba sana serikali iweze kufanya ile *reform local gaverment* ili na sisi kuweza kuleta maendeleo katika majimbo yetu, serikali zetu za mitaa sasa hivi tunaziendesha katika hali ya kusua sua hakuna bajeti maalum inayokwenda katika serikali za mitaa. Maendeleo katika maeneo yetu yanakuwa ni mendeleo ya kubahatisha ukiacha yale maendeleo ya serikali kuu lakini kuna maendeleo katika vijiji, katika maeneo yetu na katika majimbo bila ya kuziwezesha serikali za mitaa hakuna maendelea ambayo kuwa yatapatikana. Kwa hivyo naiomba serikali iweze kufanya *reform local*

government ili kuhakikisha kwamba serikali zetu za mitaa zinawezesha kuweza kutoa huduma kwa jamii.

Mhe. Spika, nikiendelea katika kitabu chake Mhe. Rais namshukuru ukurasa wa kumi na nne ameeleza kwamba katika kampeni zake alipita katika majimbo mbali mbali ya Zanzibar na akaweza kutoa ahadi ya mambo mbali mbali, kwa bahati mbaya waziri wa mawasiliano simuoni hapa lakini nadhani yupo. Katika jimbo langu la Kwamtipura Idara ya njia kutoka kwa Abasi Hussein kuendelea daraja bovu kwenye Afisi yako ya Wilaya ya CUF barabara ile Mhe. Rais ameiahidi, waziri aliyepita wa mawasiliano tulimuomba suala lile lakini nilijua kwamba ninapigwa changa la macho tu.

Kwa hivyo sitegemei kwamba na waziri wa sasa hivi kwamba nae atatupiga changa la macho hasa kwa kuwa pale kuna ahadi ya Mhe. Rais. Barabara ile sasa hivi tayari kuna ruti ya daladala na hata yeye wale wanachama wake wanaotaka kwenda mkutanoni kule akishatengeneza barabara ile itakuwa rahisi, unatoka kwa Abasi Hussein unapita Mboriborini Daraja bovu umeshafika Makao Makuu ya CUF ya wilaya kwa hivyo nafikiri utaweza kuimarisha hata chama chako nafikiri umejipanga vizuri na utaweza kusaidia katika suala hilo..

Mhe. Spika: Mhe. mjumbe umebakiwa na dakika tano tu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwa kuokoa muda vile vile nataka nije katika ukurasa wa kumi na nane, hapa kidogo nitakuomba ruhusa Mhe. Spika, nisome ili niweze kueleweka kile ninachotaka kuzungumza. Mhe. Spika, Mhe. Rais katika ukurasa wa kumi na nane *paragraph* ya tatu anaeleza:

"Tutaendeleza usimamizi wa fedha na sheria ya uwekezaji ili kuchochea kasi ya uwekezaji kujenga misingi ya uchumi endelevu, lakini vile vile mbele amesema kuwezesha uchumi wa Zanzibar kutoa asilimia kumi na kupunguza kiwango cha mfumko wa bei hadi chini ya asilimia saba na kuongeza pato la Mzanzibari kutokana na pato la sasa la shingi ambazo zimetajwa. Vile vile tutahakikisha tunaongeza viwango vya ukusanyaji wa mapato katika maeneo muhimu".

Mhe. Spika, kitu ambacho nimekusudia kukizungumza hapa suala la ukusanyaji wa mapato na matumizi, naweza kueleweka vibaya lakini bora nitoe mawazo ambayo niliyokuwa nayo umasikini Zanzibar bado upon a hali ya watu wa Zanzibar ni masikini sote tunajua, lakini bado serikali haijakuwa makini katika kuhakikisha hayo mapato madogo yanayopatikana yanatumika vizuri. Hivi sasa tuna serikali ya umoja wa kitaifa lakini bado nasema ni serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye sura ya umoja wa kitaifa, serikali yetu iko katika

maridhiano zaidi kuliko serikali ya umoja wa kitaifa na serikali yetu ni kubwa tena kubwa sana.

Nathubutu kusema kwamba katika dunia Zanzibar ni serikali ya mwanzo yenye wizara nyingi na mawaziri wengi kuliko uwezo wa serikali, Zanzibar ina majimbo hamsini tuna mawaziri ishirini na nne asilimia katibu arubaini na tisa ni mawaziri huu ni mzigo mkubwa sana tumewabebesha wananchi. Jana rafiki yangu Mhe. Omar Ali Shehe sasa hivi hayupo alisema serikali ya umoja wa kitaifa wananchi wanasema tutakuwa tumeua demokrasia ni kweli, sijamsikia hata mheshimiwa mmoja aliyezungumzia suala hili. Huu ni mzigo mkubwa lakini sasa hivi kwa sababu tuko katika maridhiano kila mmoja anaridhika na kile ambacho kimefanyika, lakini hapa ukweli tumehalalisha matumizi mabaya ya fedha za umma Zanzibar zaidi ya Mawaziri kumi na tisa waliobakia hawana kazi za kufanya ukifanya mahisabu sio chini ya milioni hamsini kwa mwezi, ka mwaka karibu milioni mia sita zinapotea bure bure kuhudumia mawaziri hawa.

Mhe. Spika, fedha hizi zingeligawanywa kwenye majimbo nadhani tungefaidika sana majimbo yetu hatuna bajeti ya maendeleo tuna miradi ya wananchi ambayo tumeiandaa, lakini hatuna uwezo wa kuweza kuitekeleza, tunajua hii ni serikali ya umoja wa kitaifa lakini mimi naita serikali ya maridhiano kwa sababu hatukuangalia maslahi ya taifa. Tunamuomba sana Mhe. Raisi sisemi awafukuze kazi mawaziri lakini serikali yake itakayokuja ya mwaka 2005 tunataka serikali ndogo ambayo yenye uwezo wa kufanya kazi vuziri, hatutaki serikali kubwa ambayo tutatumia fedha nyingi za umma.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache nataka nimalizie kwa kusema suala zima la mazingira, sasa hivi tuna wananchi wanaotumia misumeno ya chuma au misumeno ya umeme namuomba sana Mhe. Waziri anayeshughulikia masuala ya kilimo lakini vile vile na waziri anayeshughulikia masuala ya mazingira. Lazima tupige marufuku kwanza misumeno yote ya umeme hapo ndio tutaweza kuokoa mazingira. Lakini hata hao watakaoruhusiwa baadaye kutumia misumeno ya umeme basi waweze kuwa na leseni maalum.

Mhe. Spika, mwenzangu jana alizungumza unaweza ukaondoka katika shamba lako kuna minazi, miembe kila kitu, ukirudi misheli sheli 20, 30, 40 haipo katika usiku mmoja. Hili nimelithibitisha kwa macho yangu. Kuna kipindi nilipokuwa Waziri nilipata malalamiko ya mwenye shamba mmoja kwamba shamba lake limevamiwa. Nilikwenda kufanya ukaguzi kule tomondo. Baada ya kuondoka usiku ule ule diwani ananipigia simu ananambia Mheshimiwa minazi na miembe inaanguka kama lahaula. Siku ya pili nilipokwenda nikahesabu minazi karibu (18) imekatwa, miembe karibu saba (7), misheli sheli.

Mhe. Spika, kwa shoka la mkono mtu hawezi kabisa kuweza kukata miti mingi kwa kiasi kama kile. Lakini misumeno ya umeme lazima serikali yetu tujaribu kuangalia hilo. Ukiangalia sasa hivi minazi inapotea, mishelisheli inapotea, mashamba ya watu, watu wanauza viwanja bila ya ruhusa.

Baada ya hayo machache napenda kukushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii. Vile vile namshukuru sana Mhe. Rais kwa hotuba yake. Lakini changamoto tulizozieleza naomba zifanyiwe kazi.

Mhe. Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe kabla ya kuendelea na mjumbe anayefuata wale wajumbe wa Kamati ya kusimamia historia ya viongozi wakuu wanaombwa wafike hapo chumba Nam. 2 kwa ajili ya kufanya uchaguzi wa kumtafuta Mwenyekiti na Naibu Mwenyekiti.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, nami kunipatia nafasi hiyo ya kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Rais aliyoitoa November 11 mbele ya ukumbi huu wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, kwanza nianze na kumpongeza Mhe. Rais kwa hotuba yake ambayo ni dira ya maendeleo ya Wazanzibari. Naichukua tena nafasi hii kumpongeza yeye Mhe. Rais kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kuteuliwa kwake Mhe. Rais tuna imani kwamba ataliongoza taifa hili katika misingi ya sheria na taratibu ili kuweza kulifikisha taifa kuendelea au kulipa uchumi endelevu na kuwafanyia wananchi kuwafikisha katika malengo ya kujikwamua kiuchumi.

Mhe. Spika, pia nimpongeze Rais kwa uteuzi wake wa kumchagua Makamo wa Kwanza wa Rais Mhe. Seif Sharif Hamad na Makamo wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi.

Pia nimpongeze Rais kwa kutuchagulia timu ya mawaziri katika Baraza lako hili. Naamini kwamba uteuzi huu wa mawaziri na manaibu waziri likiwemo ongezeko la idadi kubwa ya wanawake mawaziri katika serikali yake italeta mabadiliko ya kweli ya uchumi na ile hali ambayo ilikuwa inadaiwa na wanawake ongezeko katika vyombo vya maamuzi itafikiwa na ule uchumi unaotarajiwa kukuwa kwa kupitia wao wanawake basi utapatikana.

Mhe. Spika, sina budi pia kukushukuru na wewe kuchaguliwa tena kuliongoza Baraza hili katika awamu hii. Tunategemea kwamba utaliongoza vyema Baraza hili kwa kutumia hekma na busara uliyonayo. Sina budi pia nitoe shukurani za aina yake kwa wale wazazi wetu waliotuzalia mtoto maridhiano Mhe. Abeid

Karume na Mhe. Seif Sharif Hamad walioridhiana na kutuletea umoja huu wa kitaifa na kulifanya taifa hili likiwa katika hali ya ummona na mshikamano. Kama unavyoona katika Baraza lako hili tukufu kwamba tumekaa na sote tunachangia hoja bila ya kupitishana migogoro wala migongano kama tulivyozoea mwanzo. Imani yangu kwamba serikali hii iliyopo ya Demokrasia ya Umoja wa Kitaifa ina nia ya kuwaletea mapinduzi ya kweli ya kimaendeleo wananchi wake.

Mhe. Spika, sasa nianze na mchango wangu rasmi. Mhe. Rais katika hotuba yake aligusia kufanya mapinduzi ya kilimo hapa kwetu Zanzibar. Kwa kweli neno mapinduzi lina maana kubwa na pana. Imani yangu kwamba mageuzi haya ya aina yake ambayo Mhe. Rais anayakusudia kwa wakulima au kwa kilimo cha Zanzibar kinaweza kuleta kweli mabadiliko ya uhakika na kuwapatia ajira watu wetu.

Mhe. Rais katika hotuba yake kuhusu kuleta mapinduzi ya kilimo amesema kwamba kilimo hiki kimechangia pato la taifa kwa asilimia 27.3. Mhe. Spika, asilimia hii 27.3 ya pato la taifa hufanya kuwapatia ajira wananchi waliokuwepo vijijini kwa asilimia 44. Mimi katika mchango wangu juu ya suala hili ningependa kumuomba Mhe. Rais katika mapinduzi ya kilimo ambayo yatafanywa basi na mimi nishirikishwe katika Wilaya yangu ya Kaskazini (B) kwa kilimo ambacho amekisema Mhe. Rais kwamba kitakuwa cha kisasa ambacho kitakuwa cha taratibu na mbinu mbadala kuliko ya zile zilizokuwepo.

Mimi katika mchango wangu juu ya suala hili ningependa kumuomba Mhe. Rais katika mapinduzi ya kilimo ambayo yatafanywa basi na mimi nishirikishwe katika Wilaya yangu ya Kaskazini (B) kwa kilimo ambacho amekisema Mhe. Rais kwamba kitakuwa cha kisasa ambacho kitakuwa cha taratibu na mbinu mbadala kuliko ya zile zilizokuwepo.

Mhe. Spika, wananchi wa vijijini kwa silimia kubwa maisha yao huwa wanategemea kilimo. Tunasema kwamba katika sekta ya ajira inaajiri zaidi ya watu asilimia 44. kilimo kwa kweli kilichopo sasa cha kijembe kongoroka kimepitwa na wakati na wananchi wanaendekea kudhalilika na kutokujua la kufanya. Kilimo hichi katika vijiji vyetu wanawake kwa asilimia kubwa ndio wanakuwa wakulima wakuu.

Mhe. Spika, mara nyingi wanaume huwa wanatoka kuzururuka na sekta nyengine lakini wanawake vijijini ndio wanaobakia kuwa wakulima. Wakulima ambao wanakosa pembejeo, wanakosa utafiti wa kitaalamu juu ya taratibu wanazozitumia katika kulima, wanakosa ushauri wa mabwana shamba,

wanakosa mbole na mambo kadha wa kadha na huwafikishia wananchi hawa kuvuna mavuno madogo ambayo hayakidhi haja.

Mhe. Spika, tuangalie kama kilimo cha mpunga wananchi wanatumia zaidi ya miezi sita kuhangaika kulima, lakini mavuno yake yanakuwa ni ya muda mdogo na matumizi yake ni madogo na hubakia vile vile kuhangaika katika maisha katika famia zao lakini hawawezi kujiongezea mali au kujikwamua katika shughuli zao za kiuchumi kifamilia kuweza kuwasomesha watoto wao.

Mhe. Spika, pia ningependa kusema kwamba mapinduzi ya kilimo Mhe. Rais alivyoligusia hili nilipenda sana kusema kwamba lishughulikiwe zaidi sehemu ya mboga mboga ambapo kwa asilimia kubwa tumekuwa sisi tunatumia tungule na pilipili boga na vitu vyengine kutoka Tanzania Bara. Naamini kwamba mapinduzi haya ya kilimo watu wakiwezeshwa na kuweza kupewa pembejeo na utafiti kufanywa juu ya ardhi zetu tutaweza kuwaajiri vijana wetu vijijini pia kuweza kuachana na ile tabia ya kukaa na kuzurura na pengine kushiriki kaka mambo yaliyokuwa hayasaidii katika taifa letu.

Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri anayehusika na wizara hii utakapofikia muda ambao umeandaliwa basi na mimi katika Wilaya yangu niwe mwenye kushirikishwa ili vijana wangu wajikwamue nao kiuchumi. Kupitia haya mapinduzi ya kilimo ambayo Mhe. Rais ameyathibitisha kutekelezwa kwake katika awamu yake hii ya uongozi.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu niende sehemu ya ufugaji. Ugaji ni moja katika taratibu au ni sekta ambayo inawaajiri wananchi wetu. Sekta hii kwa sasa inakabiliwa na matatizo mengi. Wafugaji wanakabiliwa na wizi na uhaba wa kufugia.

Mhe. Spika, vijana wengi katika miradi ambayo ilifanyika kupatiwa ng'ombe wa mazira. Mambo haya yakufanyiwa utafiti wa kina. Ng'ombe wale waliopatiwa vijana walitumia muda mrefu bila ya kuweza kuleta tija, zaidi ya mwaka mmoja ng'ombe anamkatia malisho na kumlisha lakini ng'ombe huyo anashindwa kuzaa na kuweza kumletea tija, bali yeye mwananchi anatumia muda huo kwa ajili ya kumtumikia ng'ombe ambaye amekusudiwa na lengo la serikali ni kumkwamua mwananchi kiuchumi hali ambayo inawapelekea adha.
Mhe. Spika, namuomba waziri husika atumie utaratibu ambao utaweza kuwaondoshea kero hii na kuishauri serikali itafute utaratibu mwengine utakaoweza kuwasaidia wananchi hawa mbegu kwa ajili ya upandishiaji ng'ombe zilizokuwa bora kwa ajili ya maendeleo ya wananchi hao, pia kuwapa taaluma, kwa sababu wafugaji wengi hawakuwa na taaluma juu ya shughuli zao hizi.

Mhe. Spika, niende katika sehemu ya uvuvi. Hapa kwa kweli mimi kwenye uvuvi kitu ambacho nimevutiwa katika hotuba ya Rais ni pale aliposema anamataratijio makubwa ya ujenzi wa kiwanda cha samaki kwa ajili ya kuhifadhiwa samaki wetu. Niliona eneo hili linaweza likakwamua shughuli za ajira kwa vijana wetu, kwa sababu patakapokuwa na kiwanda cha samaki na uvuvi ukawa umeimarishwa basi soko kwa ajili ya wavuvi utakuwa tayari umepatikana na hapatokuwa na shida katika shughuli hiyo. Hii ni moja katika nia ya kuwakwamua wananchi wetu kiuchumi.

Mhe. Spika, niende katika sehemu ya mazingira. Uharibifu wa mazingira ni moja katika tatizo lililoikabili nchi yetu. Nakiri mbele ya Baraza lako hili tukufu kwamba Wilaya ya Kaskazini (B) ni moja katika eneo ambalo limeathirika vibaya na uharibifu wa mazingira kwa uchimbaji wa mchanga.

Mhe. Spika, ardhi ambayo inatarajiwa kwamba wakulima watumie, ardhi ambayo inatarajiwa ifanye mambo mbali mbali na makaazi ya watu sasa sote wamechimbwa mchanga. Naomba sheria zichukue mkondo wake ili kunusuru ardhi hii na wananchi hawa kuepukana na kuwa jangwa katika eneo hili ka Kaskazini (B).

Mwenzangu aliyesimama jana Mhe. Shimba alikuwa shahidi wa kusema hilo kwamba hali ya jangwa ya Wilaya ya Kaskazini (B) imekuwa ya kutisha, hali ambayo inapelekea hata kila mmoja wetu kuanza kushtushwa. Wote wanaohitaji mchanga wanakimbilia Wilaya ya Kaskazini (B) na vibali hutolewa kiholela na watu huenda kuchimba mchanga wakiwemo wale wakuu wa serikali.

Mhe. Spika, tunaomba sheria zifuatwe na taratibu na kufuatilia juu ya hali hii mbaya. Mazingira yanaweza kusababisha hata hii nchi yetu isieleweke tena na wala isipate tena ile siha yake iliyokuwa nayo.

Mhe. Spika, niendelee sehemu kidogo ya kukuza ajira Nchini. Mhe. Rais alinivutia mno jinsi alivyosema kwamba ana azma ya kukuza ajira kwa vijana wetu. Ni kweli kabisa zaidi ya vijana asilimia 40 katika nchi yetu wenye uwezo wa kufanya kazi lakini hawana ajira za kufanya.

Mhe. Spika, wimbi lililozuka la wizi, uvutaji bangi pamoja na madawa ya kulevya limesababishwa na vijana wetu kukosa ajira. Wimbi hilo linasababisha hata kufanya wizi katika mahoteli ambayo sisi ndio nguvu yetu kuu ya uchumi, kwa sababu nguvu zetu zote Mhe. Rais katika hotuba yake anasema kwamba sekta kiongozi ameiita Sekta ya Utalii. Lakini vijana hawa kwa jinsi kushindwa kufanya shughuli zao na hawana kazi ya kufanya wanafanya mambo mpaka

wanafika katika sehemu hizo. Inaelekea kwamba tukiwaacha hivi hivi tu basi inaweza ikafikia hatua mbaya.

Mhe. Rais wa awamu ya saba nimpongeze sana kwamba yeye ameliona hili kamba atalitilia maanani kwa kujenga viwanda na kuleta utalii ambao utaweza kuwasaidia na vijana wetu kwa kupata ajira.

Mhe. Spika, nigusie kwenye sekta ya barabara, kwenye miundombinu na mimi nimo nimejaaliwa kupata kujengewa barabara. Huu ni urithi ambao nimeurithi kwa Mhe. Said Khelef ambaye mara nyingi alikuwa akipiga kelele kupatiwa kujengewa barabara ya Bumbwini. Barara inaendelea ujenzi wake katika Wilaya hiyo lakini ujenzi unakwenda kidogo kidogo mno. Halafu ujenzi huo ambao mvua za masika zinaanza Machi haitopitika barabara hiyo, kama haikumalizika mapema mno, watu wa Bumbwini watashindwa kuja mjini. Nami niungane na wenzangu wale ambao waliomba kupitia hotuba ya Rais iwemo katika umaliziwaji wa haraka wa barabara ya Bububu.

Mhe. Spika, kwa haraka, nauheshimu sana muda wako niingie katika sehemu ya wanawake. Wanawake ndio wazalishaji wakubwa wa taifa hili. Tukiangalia kitakwiwimu tunaona asilimia 51 ni wanawake. Kwa hivyo taifa linategemea zaidi wanawake katika shughuli mbali mbali za kimaendeleo.

Mhe. Spika, tunafurahi sana kumuona Rais katika makundi maalum na sisi ametushirikisha katika vikundi vya wajasiri amali. Naomba na sisi katika bajeti zetu ikuzwe kidogo kwa ajili ya kupewa nafasi maalum kwa kufanya shughuli zetu tulizozikusudia.

Mhe. Spika, mtoto wa leo ndio taifa la kesho. Hali hii inahitaji mtoto wa Zanzibar kulelewa katika misingi imara na mambo muhimu. Nimesikitishwa sana kwenda hospitali nimemkuta mtoto mwenye umri wa mwaka mmoja na nusu bila ya kufanyiwa hoduma ya aina yoyote ya kitiba akiwa anatumia haja yake kwa kutumia sehemu ya tumbo. Hili lilinisononesha na kunisikitisha sana, kwamba mtoto tangu kuzaliwa mpaka anafika mwaka mmoja na nusu hajafanyiwa shughuli yoyote ile katika serikali wakati mtoto yule ndio taifa la kesho.

Mhe. Spika, ningependa iangaliwe zaidi sahemu hii ya upande wa watoto. Pia hili hili niliingize kwamba kuna watu wanaowatumia watoto wetu kwa kufanya vitendo vibaya. Ahsante na naunga mkono hoja.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Allah (SW) kwa uwezo wake mchana huu kutujaalia tukawa tupo salama katika ukumbi huu. Pili ni kutoa shukurani zangu za dhati kwa

waheshimiwa wetu wawili waliotuunganisha Wazanzibari leo hii tukawa kitu kimoja kama watoto tumezaliwa baba mmoja na mama mmoja.

Tatu sina budi kutoa shukurani zangu kwa wawakilishi wenzangu wote tulioshiriki katika uchaguzi wa kukuchagua wewe kuwa Spika wetu wa Baraza hili tukufu. Mwisho nimalizie shukurani zangu za dhati kuweza kutoa maamuzi yao kwangu kuwa mwakilishi wao kwa kipindi hiki cha miaka mitano tunayoianza.

Mhe. Spika, baada ya hayo napenda kwa upande wangu kuchangia baadhi ya mambo mbali mbali yanayohusu hotuba aliyoitoa Mhe. Rais katika Baraza hili hotuba hii ambayo imakamilika kila kitu ndani yake. Namimi naomba nifike katika maeneo machache ili kuweza kutoa mapendekezo yangu ili waziri husika aweze kuyatia maanani.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 16, 17 Mhe. Rais alitaja sana Wizara mbili nazo ni Afya na Ustawi wa Jamii na Wizara ya Kilimo kuhusu watafiti. Kweli Zanzibar tunayo rasilimali ya watafiti katika mambo mbali mbali. Ninachopenda kuchangia hapa ni watafitii wa kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, niliwahi kutembelea katika eneo la Kizimbani. Eneo hili lina ofisi ya watafiti wa kilimo, tatizo kubwa ni mazingira kwa ndugu zetu hawa watafiti. Ile ofisi wanayoishi imejengwa tokea mwaka 1935 kabla ya Mapinduzi Matukufu. Nyumba ile haikidhi haja, haina sura ya kuishi mwanadamu hasa mtafiti wa Zanzibar.

Mhe. Spika, nasema ile ni hazina na kama ni hazina inahitaji kutunzwa. Namuomba sana Waziri wa Kilimo hawa watafiti awaangalie kwa jicho la huruma. Wakati wowote nyumba ile inaweza kuwafunika wakiwa wamo katika shughuli zetu azimu. Kwa hivyo wanahitaji kujengewa ofisi ya kisasa na ya kileo kabisa.

Nikitoka hapo niende ukurasa 25 ambao Mhe. Rais ameeleza sana masuala ya uvuvi. Kwa kweli katika nchi yetu mara hii tumepata Wizara mpya ya uvuvi na mifugo. Lakini pia Mhe. Rais aliwataka wananchi waweze kujikusanya katika makundi mbali mbali kuanzisha Ushirika wa Uvuvi. Lakini niseme kwamba awamu iliyopita ya sita ilifanya kazi kubwa ya kuwakusanya wananchi wetu kuwemo katika makundi mbali mbali ya ushirika. La msingi ni kuendeleza haya na kuwaendeleza wananchi wetu uli kutokana na umasikini uliotugubika kabisa ili waweze kupata maendeleo ya dhati na kutokana na uvuvi ambao ndio rasilimali kubwa katika nchi yetu ya Zanzibar.

Nikiendeleza hapo hapo katika kapindi kilichopita kunatetesi kwamba katika Wizara hiyo hii ya uvuvi hasa katika jimbo langu la Tumbe kuna taarifa kwamba muda mrefu sasa kumekuwa kunataka kujengwa zoko la samaki lakini imeshachukua muda na imekuwa ni historia tu pale. Pia naomba kupata ufafanuzi kwa wizara husika ili atueleze hili suala limeishia wapi.

Mhe. Spika, pia naomba katika hotuba ya Rais alielezea sana suala la afya. Kwa kweli afya ndio msingi wa mwanadamu. Mwanadamu yeyote anahitaji kupata afya tena iliyobora. Afya imekuwa ni maneno zaidi kusemwa kulikoni utekelezaji. Katika jimbo langu la Tumbe tuna tatizo kubwa kabisa la madaktari. Tunavyovituo vitatu katika jimbo langu, lakini tuna upungufu huo. Tukiangalia Kituo cha Sizini pale tunadaktari mmoja tena mwanamke. Daktari huyu inafika siku anakuwa ni mjamzito hapatikani, kwa hivyo wananchi wa pale wanakosa huduma.

Mhe. Spika, Kituo cha Tumbe, kituo hichi ndio tatizo sugu kabisa. Tume ni eneo ambalo limekusanya majumba karibuni 3000 lakini hapana daktari. Kwa hivyo tunamuomba sana Waziri husika alione hili tunahitaji watenda kazi ili wananchi wanapotaka huduma za utibabu waweze kupatiwa kama serikali yetu inavyotaka wananchi wote wapate huduma.

Mhe. Spika, nije katika eneo analolizungumza Mhe. Rais suala zima la elimu. Kwa kweli elimu ndio maendeleo. Bila ya elimu hakuna lolote linaloweza kuwa. Mimi naipongeza sana serikali iliyopita, imefanya mambo mengi, imeanzisha majengo mbali mbali ya mashule, lakini bado tunaiyomba na serikali ya awamu saba pia na hili walipe kipaumbele suala zima la walimu.

Mhe. Spika, leo hii nimewasiliana na walimu mbali mbali kwa kweli tunatatizo sugu la walimu katika jimbo langu la Tumbe. Jimbo hili lina shule karibuni 8 za msingi na sekondari lakini walimu kwa siku moja baadhi yao wanafundisha vipindi vinane hadi sita, kwa hivyo kwa wiki wanafundisha karibu vipindi arubaini. Huu sio uhai wa mwanadamu., mwanadamu anahitaji mapumziko. Ndio ukakakuta kwamba unapochukua madaftari ya wanafunzi utakuta kuna makosa ya kiuwalimu lakini kutokana na kazi ngumu anashindwa kufanya kazi. Kwa hivyo, tunamuomba sana Waziri wa Elimu ajaribu kuzisaidia hasa skuli zetu za mashamba kuondosha tatizo la walimu. Kama skuli yangu ya Tumbe inatatizo la walimu wa msingi tu wasiopungua sita (6), sekondari wasiopungua wanne (4). Wenyewe wanasema kama watapatikana walimu hawa kidogo wanaweza wakakidhi haja. Ingekuwa shule zote za jimbo langu tatizo ni walimu, pia walimu wa sayansi hapana kabisa.

Mhe. Spika, mfumo uliopita nyuma kulikuwa hakuna ubaguzi wa arti na sayansi tulikuwa tunachanganyisha masomo. Kwa hivyo walimu hawa hawa

ndio walikuwa wanasaidia wanafunzi wetu wa sayansi. Lakini kulikuwa hakuna mwalimu husika anayehusika na mambo ya sayansi. Tunamshauri sana Mhe. Waziri wa Elimu shule hizi aziangalie kwa jicho la huruma ili tuweze kukuza wanafunzi wetu katika masomo ya sayansi.

Mhe. Spika, kwa kumalizia ni kwamba tuna tatizo kubwa la umeme katika maeneo mbali mbali, kama hotuba ya rais ilivyosema kwamba tumepiga hatua kubwa katika kuusambaza umeme Zanzibar. Lakini katika Jimbo letu la Tumbe bado suala hili ni sugu hasa katika skuli na vijiji mbali mbali. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri anayehusika na mambo ya umeme aliangalie na alipe kipaumbele ili wananchi wetu watoke katika matatizo haya kuishi gizani kwa muda mrefu.

Mhe. Spika, kuna mengi niliyokusudia kuyachangia lakini kutokana na muda naomba kuiunga mkono hoja. Ahsante.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii nikaweza kutoa mchango wangu juu ya hotuba hii ya Mhe. Rais. Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia tukakutana katika mkutano huu tukiwa wazima na afya njema kabisa. Vile vile ni washukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Mkwajuni kwa kunichagua kuwa mwakilishi wao kwa kura nyingi sana, watarajie mazuri katika kipindi hiki.
Mhe. Spika, nichukue nafasi hii kukupongeza wewe kwa kuchaguliwa kwako kurudi tena katika Baraza hili ingawa la mfumo mpya, lakini umeridi tena na nikupongeze sana, hongera sana.

Mhe. Spika, nianze kuchangia kidogo kwa sababu hii hotuba ya Mhe. Rais imemaliza kila kitu, lakini nichangie kidogo kidogo tu na hasa tukizingatia muda nianze kwenye Mapinduzi ya Kilimo kwenye ukurasa wa 22. Mapinduzi ya Kilimo yameelezwa vya kutosha katika hotuba hii. Mimi naomba niweke msisitizo kidogo juu ya wale maafisa wa kilimo kule mashambani. Wananchi wetu wanakwenda mashambani lakini maafisa wa kilimo wanakuwa wanabakia maofisini hawaonekani kule mashamba. Utakuta hili ni tatizo linalowakumba wananchi wetu hasa wanaolima maeneo ya mabonde ya mpunga. Wataalamu si sana kupita wengi wanabakia maofisini.

Sasa hili linakuwa ni tatizo kwa sababu linapotokea tatizo la maradhi wale wananchi si aghalabu kuyaona kwa haraka, lakini hata wanapokuja kugundua kwamba kuna maradhi au shamba limeshambuliwa yale maradhi yanakuwa yameshachukau muda mrefu. Kwa hivyo, nilikuwa ninaomba waziri anayehusika na kilimo kuhakikisha hao maafisa wake wanasogea kule kwenye maeneo ya mashamba ili wananchi wetu au wakulima waweze kupata huduma bora kwa haraka iwezekanavyo.

Pili, zana wanazotumia mpaka leo hii tuko nyuma katika kutumia zana za kilimo, ukulima wetu tangu wadogo sisi tunaona wazee wetu vile vile na kijembe cha mkono au trekta tu, tena hilo trekta limeanza hivi karibuni. Sasa mimi naiomba serikali iweke kipaumbele katika kuweka zile zana za kisasa za kilimo tuwasaidie wakulima wetu ili tuondokane na zile zana za kizamani ambazo zimepitwa na wakati tuingie kwenye zana mpya sasa. hii hotuba ya Mhe. Rais imeeleza hayo. Kwa hivyo, naomba wizara inayohusika isaidie sana katika hili ili tuweze kufikia mapinduzi ya kilimo.

Mhe. Spika, niingie kwenye Sekta ya Uvuvi . Sekta hii ni sekta muhimu sana katika ukanda wetu hasa kule kwetu sehemu za pwani pwani, wananchi wengi sana hii ndio huduma ambayo wao inawapatia kipato, lakini huduma hii mpaka hivi sasa Mhe. Spika, wanatumia zana zile zile za kizamani ndio maana utakuta kila siku mara wamekamatwa, mara wamefurushwa wanaambiwa wanatumia zana haramu. Naiomba wizara husika iwasaidie sana wavuvi wetu hawa kuwaelimisha na kuwatanabahisha juu ya zana zile za kizamani wanaita zana haramu, wawapelekee zile zana za kisasa, wakiwapelekea zile wataacha tu zile za kizamani.

Hili tatizo lipo hata katika jimbo langu kwenye eneo la Kivunge lipo hili tatizo. Kuna wavuvi wamenyang'anywa mitego yao na kila kitu wakaahidiwa watapelekewa zana za kisasa au mitego ya aina nyengine lakini mpaka hivi sasa hakuna kilichofanyika. Sasa kitu cha namna hii mtu kama huyu na pale ndipo anapotegemea maisha yake atarudi tena tu kwenye zana zile za haramu. Kwa hivyo, tunapowanyang'anya ile mitego basi wapelekewe zile zana nyengine, tukiwapelekea hizo zana ambazo tunazitaka au mitego tunayotaka kutumia kwa sasa basi nina hakika wataacha ile ya zamani iliyo haramu.

Wenzangu waliochangia walichangia juu ya jambo hili sana tu, hasa Mwakilishi wa Jimbo la Kijani, alilichangia vizuri sana suala hili la uvuvi haramu, hili limetapakaa mote. Sisi tunasema uvuvi haramu lakini wale wavuvi wetu mpaka wabadilike tuwabadilishe na kuwabadilisha ni kuwapelekea zana nyengine, tukiwanyang'anya ile mitego ambayo wanatumia sasa hivi basi tuwatafutie mbadala wake, tusipowatafutia mbadala wake tutakuwa tumewanyang'anya watatafuta mingine watarudi pale pale kwa sababu hawana kingine cha kukifanyia kazi.

Halafu vile vile tuwahamasishe katika kufanya vikundi vya ushirika ili tuweze kuwapa zile zana. Mimi katika jimbo langu pale ninavyo vikundi vya ushirika vya mambo ya uvuvi vimeshajikusanya, wamejishajihisha vizuri, wameanzisha ushirika, lakini kupata hizo zana za kutumia sasa kwenda kufanyia hizo shughuli zao ndio kishindo, mpaka hii leo ni vikundi vichache sana labda ni

viwili tu ambavyo vimepata kupewa boti na vitu vyengine, lakini vingi vipo havijapata hizo huduma. Kwa hivyo, namuomba waziri husika atusaidie hilo suala kama hivyo vitu vipo tuwasiliane ili twende tukachukue hiyo mikopo au misaada ya vikundi vya ushirika ili waweze kujisaidia.

Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 27 suala la kukuza ajira. Lengo la dira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya 2020 ni kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2020 asilimia 50 ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi wawe wameajiriwa kwenye sekta ya utalii na viwanda, nianze kwenye sekta hii ya utalii.

Sisi kwetu utalii upo, lakini jana Mheshimiwa mwenzangu wa Jimbo la Matemwe alizungumzia sana sekta hii kwa sababu yeye ndio inamgusa zaidi pale. Lakini hata na mimi kwenye jimbo langu la Mkwajuni watu wengi wanakwenda kufanya kazi sehemu za Nungwi na Matembwe kwenye sekta ya utalii lakini tatizo linabaki pale pale. Ajira katika mahoteli yale ni ngumu, hili liko wazi kabisa Mhe. Spika, wanakwenda vijana wetu tumewasomesha, mimi mwenyewe binafsi nimeshasomesha vijana pale katika Chuo cha Utalii, lakini wanapoomba ajira kule katika mahoteli inakuwa ngumu kupata. Hawana tofauti na wale wengine ambao wanakwenda kufanya kazi pale, tumeshawasomesha katika Chuo cha Utalii Maruhubi vyeti wanavyo lakini ajira wakiiomba mara nyingi majina yao utakuta hayamo.

Kwa hivyo hili nalo ni tatizo waziri anayehusika na wizara hii atusaidie kuhakikisha kwamba hoteli zile zinawasaidia wale wazalendo kwanza ambao wana sifa basi na wao kwanza wapatiwe zile ajira kuliko kwenda kuchukua watu wa mbali zaidi tukawaacha wale inakuwa ni tatizo. Madhara yake inakuwa kwamba wale wananchi ambao wapo katika maeneo yale wanahisi ule utalii hauwafaidishi ndio maana inafika pahala wakawa wanasema utalii hauna maana. Hili ni tatizo Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kwa upande wa viwanda sisi hatuna viwanda vingi lakini tuna kiwanda cha Mahonda cha kutengeneza sukari. Kiwanda kile ni cha siku nyingi sana, sasa hivi kimepewa mwekezaji lakini mwekezaji yule mpaka sasa mimi sijaona sukari inayotoka Mahonda hapa kwetu, kipo tu kiwanda kimebinafsishwa, kimepewa mtu lakini hakuna sukari inayotoka mahonda na kiwanda kile hapo zamani kilikuwa kinachukua soko kubwa la ajira hasa kwa Mkoa wetu wa Kaskazini, ajira za kwenda kukata miwa na mambo mengine walikuwa watu wengi sana wanakwenda kufanya kazi pale., lakini tangu kupewa hawa wawekezaji hakuna hizi ajira sasa sijui wanatumia utaratibu gani kwa kweli. Namuomba waziri anayehusika na mambo haya ya viwanda aliangalie suala hili liweze kusaidia wananchi wetu kuweza kupata ajira katika maeneo ya viwanda.

Mhe. Spika, niingie katika suala la kupambana na umasikini ukurasa wa 29. Mhe. Rais amezungumzia sana uanzishwaji wa vikundi vya ushirika *SACCOS* na hasa kwa vijana na kinamama. Mhe. Rais amezungumza sana maeneo hayo kwa kusema kwamba atayafanyia kazi na kuzitambua rasilimali na biashara za wanyonge ambazo ziko kwenye sekta isiyo rasmi. Sisi tunazo hizo *SACCOS* nyingi sana lakini tatizo linakuja pale pale Mhe. Spika, mtaji. Watu wanajikusanya, wanaanzisha vikundi, lakini kupata mitaji ndio ngumu. Ukigusa mabenki huko hakushikiki kuna mambo mengi masharti yanayotoka ili vikundi vile vipate mtaji ule au vipate kukopeshwa. Vikundi vile havifikii vile viwango vinavyotakiwa.

Sasa hapa namuomba waziri anayehusika na mambo ya kupambana na umasikini atusaidie vikundi vyetu hivi vya ushirika vya kinamama na vijana kuweza kuandaa utaratibu wa kuweza kupata mikopo ambayo haina riba ili tuweze kuanza kuwanyanyua. Sisi vikundi kule tumeshatayarisha, mimi jimboni kwangu nina zaidi ya vikundi 60 vimeshakuwa tayari kama Mhe. Waziri keshakuwa tayari na mambo yapo basi mimi niko tayari hata kesho tukaanze hiyo kazi.

Sasa niende kwenye suala la ardhi. Mhe. Spika, suala la ardhi kule kwetu ni matatizo. Kuna migogoro mingi sana ya ardhi nafikiri waziri anayehusika atusaidie sana. wananchi wetu wanapata matatizo, migogoro ya ardhi imekuwa mingi kila pahala unapotembea hasa sehemu za pwani pwani tunapata malalamiko ya mambo ya ardhi. Kwa hivyo, namuomba waziri anayehusika na wizara hii atusaidie sana kuweza kutatua migogoro ya ardhi, hii inatokana na mambo ya kuuza mara kauziwa huyu, huyu haikuwa kauziwa huyu, sasa haya ni mambo yanayoonekana yanakua sio kuchipuka kwa sababu yashachipuka sasa yanakua. Naomba sana suala hili waziri anayehusika na mambo ya ardhi atusaidie. Bahati nzuri Mhe. Naibu Waziri anatoka kule kule kwenye hiyo migogoro yenyewe Jimbo la Nungwi. Kwa hivyo nafikiri atatusaidia sana katika hili.

Mhe. Spika, nimalizie kwenye suala la Muungano. Suala hili linatusumbua Mhe. Spika, kuna mambo mpaka leo yanazungumzwa tu lakini hayafikii, sasa kama yanazungumzwa tu hayafikii lini yatafikiwa? Hatuafikiani kwa nini? Hivi vitu ni makubaliano ya pande zote mbili, sasa kuna ulazima gani wa kukaa tu tukawa tunalazimishana vitu ambavyo havipo, tufike mahala tuzungumze, tukubaliane tutekeleze.

Mhe. Omar Ali Shehe alizungumza kwenye suala lake la msingi hapa kwenye mambo ya *PAC* ule udhibiti wa fedha za serikali. Yanatupa matatizo, kuna fedha zinakusanywa hapa zinapatikana ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa sababu wananchi ndio tunakwenda kulipa zile fedha pale, lakini

hatuzikagui sisi. Mimi nimo kwenye Kamati ya *PAC* mwenyekiti wangu Mhe. Omar Ali Shehe hatuzikagui zile fedha sasa hatuzijui hata matumizi yake yanakwendaje. Aliliuliza hilo suala lakini nikataka kwenda kwenye suala la nyongeza muda ukawa umekwisha. Hili ni tatizo Mhe. Spika, fedha zile anazikagua nani na zile ni fedha za wananchi, *PAC* ndio kazi yetu sisi kwenda kuangalia yale matumizi yake lakini hatuyaoni, anakagua mkaguzi wa mahesabu yule wa Bara hatuletei ripoti sisi huku kabisa. Sasa ningeomba Mhe. Spika, suala hili taasisi zinazohusika zikae pamoja kulipatia ufumbuzi haraka iwezekanavyo ili fedha za wananchi tuweze kuzijua zinavyoingia na matumizi yake zinavyotumiwa.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, nichukue nafasi hii kurejea kumpongeza Mhe. Rais kwa hotuba yake nzuri sana ambayo inaonekana ni dira ya maendeleo katika miaka hii mitano ya Serikali ya Awamu ya Saba. Baada ya kusema hayo nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ahsante sana Mhe. Spika.

Shadya Mohamed Suleiman: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar. Kwanza kabisa nachukua nafasi hii kumshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kuiongoza Zanzibar kwa awamu ya saba. Pili nichukue nafasi hii kukushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Baraza hili. Vile vile napenda kuchukua fursa hii adhimu kuwapongeza wanawake wa Mkoa wa Kusini Pemba kwa kuweza kunichagua kwa kura nyingi kuwa Mwakilishi wao.

Mhe. Spika, mimi sina la kuongeza kwenye hotuba ya Mhe. Rais, kwani imemaliza kila kitu kazi iliyobaki ni kwa Waheshimiwa Mawaziri na sisi Wawakilishi kuyatekeleza ili tusonge mbele.
Mhe. Spika, naunga mkono hotuba ya Rais kwa asilimia mia moja. ahsante sana.

Mhe. Spika: Mhe. Shadya Mohamed amenisaidia sana kwa sababu ameniokolea muda, kwa sababu katika wale wachangiaji sita huyu ndiye aliyekuwa wa sita kama nilivyosema kabla. Sasa basi nilipata maombi maalum ya mawaziri kwamba jioni watakuwa na dharura, basi waitumie nafasi hii kwa ajili ya kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya mambo yaliyogusa wizara zao. Naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, nakushukuru sana nami kunipa dakika chache kuzungumzia baadhi ya mambo yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu yanayohusiana na Wizara ya

Kilimo na Maliasili yanayotokana na hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Kwanza nianze na mimi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kutujaalia sote kufika hapa siku ya leo tukiwa wazima wa afya na siha, niwapongeze Wawakilishi wenzangu kuchaguliwa kuwa wajumbe wa Baraza hili. Nichukue fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Kiembesamaki kunichagua mimi kuwa Mwakilishi wao kwa mara nyengine tena, nawashukuru sana.

Pia niwakaribishe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Mhe. Spika, Jimbo la Kiembesamaki, hapa tulipo ni Jimbo la Kiembesamaki hamtopata tabu kwa maana ya wananchi wa jimbo hili waungwana, wakarimu, wachamungu, misikiti ipo karibu Waheshimiwa Wajumbe, mkono wa kulia tu mkitoka nje hapo dakika mbili kuna msikiti mmoja wa karibu maarufu panaitwa Mtongani, Misikiti ya Ijumaa ipo mingi kwa hivyo hamtopata tabu.

Pia nimpongeze Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuchaguliwa na wananchi wa Zanzibar kuwa rais wa awamu ya saba, nimpongeze pia Makamo wa Kwanza Maalim Seif Sharif Hamad na wa Pili Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa uteuzi wao wa nafasi hizo.

Mhe. Spika, kutokana na muda Sekta ya Kilimo ni pana yaliyozungumzwa ni mengi sana, lakini kutokana na muda nitagusa baadhi ya maeneo na naamini Waheshimiwa Wajumbe watatukubalia kwa maana vikao vitavyofuata kuendelea kutoa ufafanuzi na mwelekeo wa wizara zetu.

Mhe. Spika, la mwanzo ambalo wengi walilizungumza ni ukosefu wa taaluma kwa wakulima wetu. Mhe. Spika, ni sahihi mfano mmoja ni mabibi na mabwanashamba na ukosefu wake. Kwa wastani bibi na bwanashamba mmoja anatakiwa kuhudumia wakulima 400. Kwa bahati mbaya sana hivi sasa mmoja anahudumia wakulima zaidi ya 1500, kwa kweli ni mtihani mkubwa huu na hata hao waliobaki wengi wao sasa wamekaribia umri wa kustaafu, lakini kwa bahati nzuri serikali ya Dr. Ali Mohammed Shein tayari imeshatupa maelekezo na tunaendelea na mazungumzo na Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ajili ya kuanza utaratibu wa ajira sasa kuwaajiri mabibi na mabwanashamba wa kutosha kuhudumia wakulima wetu.

Tutaongezea hadhi kituo chetu cha Utafiti Kizimbani ili kiweze kujitegemea na kiwe kitovu sasa cha utafiti kwenye ukanda wetu huu na iweze kukidhi haja ya tafiti ya nchi yetu na hata kuwasaidia watafiti wa nchi jirani. Chhuo cha kilimo pia Kizimbani kitaangaliwa maalum, hivi sasa wanatoa cheti tu cha kilimo, lakini tayari wameshaanza tumebadilisha mitaala na utaratibu sasa wa kupata

diploma ya kilimo wameshaanza kuchukua *intake* na tunategemea mwaka 2013 *intake* ya mwanzo itahitimu.

Mhe. Spika, jengine ambalo limezungumziwa na wajumbe wako wengi sana ni umuhimu wa umwagiliaji. Mhe. Spika, eneo ambalo linaweza kumwagiliwa kwa hapa kwetu ni hekta 8521 kwa Unguja na Pemba. Hivi sasa tunamwagilia hekta 700 tu, eneo jengine lote linalimwa mpunga kwa mvua na hivi sasa tuna malengo mahsusi ya kuelekea mwaka 2015 ambapo tayari tumefikia hatua nzuri sana na Serikali ya Korea ya Kusini na uko mradi ambao tunategemea utaanza mwaka huu wenye kima cha dola za Marekani 53 milioni na tumelenga kuweka miundombinu kwenye hekta 2105. Ni *scheme* sita hizo kwa upande wa Pemba ni mbili, Mlemele hekta 75 na Mwakararani hekta 100, kwa Unguja Cheju ni hekta 1200, Chaani Kibokwa hekta 500, Kilombero hekta 230.

Malengo yetu tukifika mwaka 2015 tuweze kukidhi asilimia 40 ya mahitaji yetu ya ndani ya mchele. Lakini kuelekea huko ni lile suala mwanzo la taaluma.

Mhe. Spika, hivi sasa wakulima wetu asilimia 6.8 tu ndio wanaotumia mbegu bora na asilimia 10 tu ndio wanaotumia mbolea. Ili kuweza kufikia malengo haya ya mwaka 2015 la kufikia asilimia 40 ya mahitaji yetu ya ndani, lazima tutoke hapa tulipo kwa kuwashajihisha na kuwaelimisha wakulima wetu kutumia mbegu bora, mbolea, ili malengo yetu yaweze kutimia na wao waweze kupata tija kubwa zaidi katika uzalishaji huo wa mpunga.

Mhe. Spika, jengine ambalo limezungumzwa ni wadudu waharibifu hasa hawa nzi wa matunda. Nataka nichukue fursa hii kumshukuru sana waziri mwenzangu wa Mifugo na Uvuvi kwa jitihada zake za kutusaidia kupitia Mradi wa *MACEMP* na tayari kwa awamu ya pili tumeshaagizia mitego 43,000 na dawa ya kutosha kuendelea kusambaza kwenye wilaya zetu 9 hizi na wilaya zilizopatiwa dawa tayari nyengine ambazo hazijapatiwa ili tuendelee na jitihada hii endelevu ya kukabiliana na nzi wa matunda na pia jitihada zinachukuliwa kuhakikisha kwamba kitengo chetu cha uhifadhi wa mimea tunakiimarisha pamoja na kuimarisha utaratibu wa karantini uwanja wa ndege na bandarini ili kunusuru wakulima wetu na haya maradhi ambayo yanaingia hapa nchini.

Mhe.Spika, jengine lililozungumzwa na hasa Mjumbe wa mwisho aliyekaa hivi sasa Mhe. Mbarouk Wadi Mtando ni zana za kilimo pamoja na pembejeo. Ni sahihi Mhe. Spika, hivi sasa jitihada kubwa inahitajika ili serikali kuchukua jitihada makusudi za kuwawezesha wakulima wetu waweze kulima kwa maeneo madogo wanayotumia na kupata tija kubwa zaidi. Hilo litakuja tu, pale ambapo tutawawezesha wakulima wetu, serikali imekuwa na utaratibu hivi sasa kuwasaidia kwa asilimia 50 wakulima wetu mbolea na mbegu. Bahati nzuri

tayari tumeshapewa maelekezo na serikali kulitizama hili jambo kwa upana zaidi ili tuweze kuwasaidia zaidi wakulima wetu.

Kuna mfano mzuri sana wa nchi jirani, Mchi ya Malawi mpaka miaka mitatu nyuma ilikuwa kila mwaka inakabiliwa na njaa na hata ilipokuwa na hali nzuri ya mvua bado walikuwa wanapata tatizo kubwa sana la uhakika wa chakula. Lakini miaka mitatu hii Zambia tayari sasa inasafirisha hasa mahindi, imekuwa sasa *net exporter* wa mahindi. Walichokifanya Serikali ya Zambia ni kuwasaidia *sup seed* yaani kuwapa nafuu wakulima wa nchi yao hasa wadogo wadogo kwa kuwapatia mbolea kwa kupitia utaratibu wa *voucher*. Ndani ya miaka mitatu au minne hali hiyo imeweza kusababisha sasa Zambia kuweza kusafirisha mahindi. Tunaamini kwamba tukilitizama hili kwa upeo wake kuanzia matrekta, *power tillers*, mbolea, na mbegu tutaweza kufikia pahali kunyanya hali na kuwawezesha wakulima wa nchi yetu.

Kwa mnasaba huo huo, kuna mradi mmoja ambao tayari umeshabuniwa na wataalamu wa wizara yangu wakishirikiana na *African Development Bank* na *IFAD* na taasisi isiyokuwa ya serikali *ACRA* unaoitwa *Marketing Infrastructure Value Addition* na *Rural Finance*. Tunapozungumzia *Marketing Infrastructure* wajumbe wako wengi Mhe. Spika, walizungumzia barabara. Mradi huu ambao tayari umeshapitishwa katika *Axecutive Board* za taasisi hizo nilizozitaja, tunategemea utaanza mwaka huu, utasaidia kujenga zile *feeder road* muhimu zinazotoa mazao ya wakulima wetu ili ziweze kupitika.

Mradi huu pia utasaidia kujenga masoko ya wilaya ambayo yatakuwa na hifadhi *cold rooms*, hilo pia limezungumzwa na wajumbe wako wengi kwa sababu mazao yanaoza, wanapeleka sokoni ikiwa yako mengi kama hawana njia mazao yale huoza. Masoko hayo yatakuwa na nafasi ya kuweza kuhifadhi mazao hayo ili wananchi wakulima wetu waweze kuuza kwa wakati na bei muwafaka.

Mhe. Spika, nakushukuru sana, ninayo mengi lakini nafikiri kwa sasa wajumbe wanikubalie itoshe hapa tutafanya jitihada kutoa ufafanuzi kwa vikao vinavyofuata. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Kazi, na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote na mimi niungane na wenzangu wote kumpongeza Mhe. Rais kwa hotuba nzuri na kumtakia afya njema, na sisi mawaziri wake tuko tayari kufanya kazi kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata lile ambalo wanalihitajia.

Mhe. Spika, nakushukuru wewe na kukuombea Mwenyezi Mungu vile vile upate afya njema na kuwaombea afya njema waheshimiwa wote wakiwemo

mawaziri, manaibu mawaziri na wajumbe wa Baraza ili waweze kutekeleza majukumu yao vizuri. Sitowasahau wananchi wa Jimbo la Makunduchi kwa kipindi cha tatu sasa hivi wanaendelea kunipa heshima hii na ni watu wazuri tu, wana imani kama alivyosema Mheshimiwa aliyekaa kwa wananchi wa Kiembesamaki na wa Makunduchi hivyo hivyo. Kwa hivyo, karibuni.

Mhe. Spika, moja ambalo nata nilizungumze kwa haraka haraka kwamba wizara hii imepewa jukumu kubwa sana kuhusiana na masuala ya kazi na uwezeshaji wananchi kiuchumi na ushirika. Wizara hii inaingiliana na wizara zote na hivi sasa nafanya mawasiliano na Wizara ya Kilimo na Maliasili, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili tufanye vikao vya pamoja. Kwa sababu sasa tunahitajia kuwawezesha wananchi katika hali zote, tunachohitajia maji, nishati na ardhi, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na yote hata Wizara ya Afya kwa sababu unapopata watu wanaougua maradhi ya kisukari na mengine wale wanataka kuwezeshwa vile vile wajihisi kwamba wao ni sehemu ya jamii.

Kwa hivyo, ni wizara ambayo inaingiliana na wizara zote hizo. Sasa tumejipanga vizuri na tutaanza mikutano na wizara hizo husika. Kwa mfano, katika Wizara ya Kilimo, Mhe. Waziri kazungumza hapa wanataka kuwezesha wananchi wapate mbolea, lakini utumiaji wa mbolea wataalamu watakuwa wao lakini kuna wakati itabidi tuwahitajie kwa nyezo fulani, itabidi na sisi wizara yetu ihusike. Katika masuala ya uvuvi hivyo hivyo na masuala mengine yanayohusiana na uwezeshaji.

Kuhusu vikundi vya *SACCOS* Mhe. Spika, napenda niwahakikishie wananchi kwamba serikali imejipanga vizuri na tumeshaanza mikakati ya kutafuta njia mbali mbali na misaada ili kuweza kupata fedha ambazo zitatuwezesha kusaidia vikundi. Lakini hivi sasa naomba niwahakikishie waheshimiwa kuwa fedha za mikopo bado tunazo wala msiwe na wasi wasi na baadhi ya vikundi vinakuja. Lakini sasa kumejitokeza tatizo hii wizara kuitwa uwezeshaji napata shida kwamba wanakuja watu wanasema tumeambiwa wewe ndiye utayetuwezesha utuezekee nyumba yetu, utupe matofali, sasa inakuwa kazi kubwa Mhe. Spika.

Kwa hivyo, kuna haja ya kuelimisha jamii juu ya suala la uwezeshaji hasa lipi ambalo limekusudiwa. Napanga ziara Mhe. Spika, katika majimbo yote 50 na bahati nzuri nimeshapata maombi ya wajumbe kama 15 hivi wameniomba niende kwenye majimbo yao kukutana na vikundi vya kinamama, vikundi vya ushirika vya *SACCOS* na vyenginevyo. Mimi nimeshawakubalia sasa na wale wengine ambao wanahitaji kufanyiwa ziara kama hizo si vibaya tukawasiliana. Katika ziara hii madhumuni ni kwenda kuwasaidia wananchi na ndio wizara hii ya Kazi na Uwezeshaji wa Wananchi, hatwendi kule kwa madhumuni ya

kuwasaidia wawakilishi tu, lakini na wananchi wenyewe. Tukiwasaidia wananchi na waheshimiwa tutakuwa tumewasaidia hivyo nawatoa hofu kwamba *Inshaallah* nitakuwa mgeni wenu huko mnipokee ili tuweze kufanya kazi kwa vizuri zaidi.

Napenda nimalizie Mhe. Spika, kwa kuwahakikishia kwamba wizara yetu imejipanga vizuri kufufua vile vyama vya ushirika vilivyokuwepo hapo awali ambayo haviko katika hali nzuri, kuwawezesha wananchi katika njia mbali mbali kuwapatia mafunzo na tunakusudia kutayarisha taasisi mbali mbali katika kila wilaya ambazo zitatumika kwa ujenzi hasa wa taasisi mpya zitazowezesha wananchi kuwapatia mafunzo na utaalamu waweze kutumia vizuri rasilimali waliyokuwanayo ili waweze kujitegemea zaidi na wafike pahali pazuri.

Mhe. Spika, namalizia kwa kumshukuru sana Mhe. Rais kwa kunipa imani yake kwa kuniteuwa mimi pamoja na wenzangu na *Inshaallah* tutajitahidi kadiri ya uwezo wetu katika kipindi cha miaka mitano kufanya kazi kwa uwezo wetu wote. Nakushukuru Mhe. Spika, na natumai nimetumia muda wako vizuri sana bila ya kuongeza dakika ahsante sana.

Mhe. Spika: Nakushukuru Mhe. Waziri, Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni nyote lakini pia niwaombe radhi wale ambao waliomba waseme lakini wamekosa nafasi, wakiwemo Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Jaku Hassan Ayoub, Mhe. Bikame Yussuf Hamad, Mhe. Waziri Asiyewizara Maalum (Haji Faki Shaali). Muda kama utaruhusu jioni tunaweza kuangalia kwa sababu na yeye ni waziri vile vile, Mhe. Salum Amour Mtondoo pamoja na, nafikiri ndio hao tu.

Waheshimiwa Mawaziri waliobaki wao nadhani tutasikiliza majumuisho yao kwa yale yaliyowagusa katika wizara zao na hatimaye kumalizia na mtoa hoja hapo jioni. Tayari ninayo maombi ya Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Waziri wa Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Fedha, Uchumi na Maendeleo nafikiri ndio hao ambao nimepata maombi yao kama kutakuwa na wengine zaidi basi tutazingatia hapo jioni. Lakini pia namshukuru na namuomba radhi kwa kweli Mhe. Abdalla Mohammed Ali ambaye pia hakuweza kuchangia.

Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe naomba sasa niahirishe kikao hiki hadi saa 11:00 jioni leo ambapo tutafanya majumuisho.

(Saa 6:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kama tulivyokubaliana kipindi cha asubuhi kwamba wakati huu wa jioni tunakwenda moja kwa moja kuwasikiliza Waheshimiwa Mawaziri. Nimepokea majina ya mawaziri watatu ukiachia Mhe. Haroun Ali Suleiman na Mhe.Mansoor Yussuf Himid ambao tayari wao wameshatoa maelezo yao.

Kwa hiyo, sasa naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Dakika 15 nafikiri zitasaidia kwa kazi hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza na mimi naomba nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi. Lakini pia nichukue fursa hii nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kuwasilisha hotuba hii ya Mhe. Rais. Kama walivyosema wenzangu hotuba hii imekamilika, hotuba nzuri na kwa kweli ndio dira yetu ya kufanya kazi katika serikali kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Mhe. Spika, baada ya kueleza hayo, nieleze yale mambo ambayo kwa kweli yamegusa gusa katika wizara yetu. Moja linahusu hili suala la Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Mhe. Spika, kwanza napenda nipokee pongezi nyingi za Waheshimiwa Wajumbe ambao wameupongeza muundo huu na kuutakia kheri ya mafanikio makubwa. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Lakini pia Waheshimiwa Wajumbe walieleza kwamba wananchi wengi sana wa visiwa vyetu vya Unguja na Pemba wana matumaini makubwa na Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa.
Mhe. Spika, mimi nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi kwamba nia ya serikali ni kuilinda na kuiendeleza Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa ili iweze kufanya wajibu wake kwa wananchi. Mhe. Spika, wajibu mkubwa ni kuwatumikia zaidi wananchi kwa kuleta maendeleo yaliyo makubwa zaidi na kuimarisha amani, umoja na upendo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kazi kubwa iliyo mbele yetu ni changamoto ambayo ni kuvumiliana katika safari hii. Mhe. Spika, katika safari hii nzito lazima uvumilivu iwe ndio kitu kikubwa sana katika kufanikisha safari yetu. Lakini kwa hali ambavyo ilivyo maelewano yapo makubwa, shughuli zinafanyika vizuri na nataka niwahakikishie wananchi kwamba tuna hakika safari yetu itakuwa nzuri zaidi.

Mhe. Spika, jengine lililokuwa linahusu wizara yangu ni kuhusu daftari la kudumu la wapiga kura. Mhe. Spika, yalikuwepo malalamiko kwa baadhi ya wajumbe humu ndani kwamba wapo wananchi ambao walikosa fursa za kukandikishwa katika daftari hilo na wakati walikuwa na haki ya kuandikishwa.

Mhe. Spika, ni kweli kasoro ndogo ndogo zimejitokeza katika mchakato mzima wa Uchaguzi Mkuu uliopita, lakini nia yetu ni kurekebisha kasoro hizo. Lakini lazima nichukue nafasi hii Mhe. Spika, kuipongeza sana Tume ya Uchaguzi kwa mara ya kwanza katika nchi yetu tumefanya uchaguzi tukiwa katika hali ya amani na utulivu mkubwa, umoja na upendo. Hiyo ni historia kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa dhamira hiyo hiyo Mhe. Spika, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu na wananchi wote kwamba tutachukua kila hatua zinazofaa kurekebisha kasoro zilizojitokeza ili sasa tuwe na tume iliyo nzuri zaidi. Vile vile uchaguzi wowote ambao utatokea tuufanye kwa kulinda maslahi ya wananchi wetu kikatiba na kidemokrasia. *(Makofi)*
Mhe. Spika, jambo jengine ambalo linagusa wizara yangu ni suala la mambo ya Muungano. Mhe. Spika, ningependa niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba nia kubwa ya serikali hii ya Awamu ya Saba ni kuimarisha Muungano wetu. Mambo makubwa ambayo yatatiliwa mkazo miongoni mwake ni:

1. Kuimarisha utendaji wa Kamati ya Pamoja ya Kutatua Kero za Muungano kwa kuandaa utaratibu madhubuti wa vikao vya kamati na utekelezaji wa haraka wa maamuzi yanayofikiwa.

2. Kuimarisha uchangiaji na mgawanyo wa mapato ya Muungano.

3. Kuimarisha utaratibu wa kuandaa na kutekeleza mikakati na mbinu za pamoja na kuinua uchumi wa pande zote mbili za Muungano wetu.

4. Kushughulikia taratibu za ajira ya watumishi katika taasisi za Muungano ili utumishi huo uwe na sura ya muafaka ya Kimuungano.

5. Hivi sasa tuna endelea na mazungumzo kuhusu namna bora tutakavyosaidiana katika Sekta ya Utafiti ili tupige hatua katika shughuli za utafiti hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, waziri anayeshughulikia mambo hayo alikuwepo Zanzibar tokea majuzi kwa nia ile ile ya kutusaidia katika mambo haya ya utafiti. Napenda nimshukuru sana Mhe. Waziri Makame Mnyaa Mbarawa kwa kasi aliyoanza nayo katika kusaidiana kwenye masuala haya ya utafiti.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nina hakika Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko atakuja kulieleza kwa kina ni suala la kupanda bei za vyakula. Mhe. Spika, ni kweli kumejitokeza kupanda bei za vyakula na jambo hili linaathiri sana wananchi wetu hasa wale wenye kipato cha chini.

Mhe. Spika, tatizo hili kwa kiasi kikubwa linachangiwa na hali iliyojitokeza ulimwenguni. Kwa sababu sisi kwa kiasi kikubwa tunaagiza bidhaa za vyakula kutoka nje ya nchi yetu. Kwa msingi huo, kadri ya hali itakavyotokea kupanda kwa bei za vyakula ulimwenguni basi itaathiri na upande wetu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, licha ya kupanda kwa bei za vyakula pia kuna tatizo la kupanda bei za mafuta. Vile vile matatizo mengi yanayojitokeza ulimwenguni hasa mafuriko yaliyotokea Amerika ya Kusini na Australia yamesababisha uzalishaji wa chakula kuwa mdogo ulimwenguni. Hivyo, kwa njia moja au nyengine tatizo la upandaji bei za vyakula limejitokeza hapa kwetu.

Lakini serikali imechukua hatua mbali mbali ikiwemo kwanza kupunguza ushuru kwa bei za vyakula hasa sukari, unga wa ngano na mchele. Vile vile kuna mpango kabambe ambao Mhe. Mansoor Yussuf Himid asubuhi hii aliueleza kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa nia ya kuimarisha kilimo chetu tuweze kujitosheleza kwa chakula hasa kilimo cha mpunga kupitia mpango wa umwagiliaji.

Lakini pia Mhe. Spika, hatua nyengine ambazo serikali inachukua ni kuanzisha utaratibu wa kuwa na akiba ya chakula. Mhe. Spika, kadri hali yetu ya kiuchumi itakavyokuwa nzuri nia yetu ni kuwa na utaratibu wa kuwa na akiba ya chakula ambayo kwa kiasi kikubwa yanapotokea matatizo kama haya tunaweza kuyatumia ili kutoa upungufu wa bei za vyakula kwa wananchi wetu. Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo nakushukuru kwa kunipa nafasi na namtakia kila la kheri Mhe. Rais. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza na mimi nataka nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia na kutuwezesha kufanya uchaguzi wetu kwa salama na amani. Pia kumuwezesha Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuunda Serikali yetu ya Umoja wa Kitaifa ambayo leo hii sote tunajivunia. *(Makofi)*

Lakini pia nataka nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuiweka Zanzibar katika amani na utulivu na namuomba sana aendelee kutupa amani na mapenzi miongoni mwa Wazanzibari. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya shukrani hizo nataka nimpongeze sana Mhe. Rais kwa hotuba yake ambayo Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ameweza kuiwasilisha hapa ili sisi Waheshimiwa Wawakilishi tuweze kuichangia. Mhe. Spika, nampongeza sana Mhe. Rais, hotuba yake imekuwa ni dira kwetu na ndio itakayotuongoza katika kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Spika, mimi naomba nichangie katika maeneo fulani fulani ambayo baadhi ya Waheshimiwa Wawakilishi wameomba ufafanuzi hasa katika maeneo ya kuongeza mapato ya wananchi na vile vile katika suala zima la kupunguza utegemezi.

Mhe. Spika, nataka nianze kwa kusema kwamba katika hotuba ya Mhe. Rais ukurasa wa 10 ame-*quote* amesema kwamba "Utafiti wa matumizi ya kaya uliofanyika mwaka 2004/2005 umeonesha kwamba kwa kila Wazanzibari 100 basi Wazanzibari 49 ni maskini".

Mhe. Spika, hii ni changamoto kubwa sana na ziko sababu za msingi ambazo zinapelekea Wazanzibari 49 kuwa ni maskini. Lakini Mhe. Spika, nataka nikuhakikishie kwamba tumefanya utafiti mwengine na hivi karibuni tu takwimu nyengine zitatoka zitaweza kutupa picha halisi katika kipindi hichi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2004/2005 hadi mwaka 2009/2010.

Lakini kama nilivyoeleza Mhe. Spika, ziko sababu za msingi zinazopelekea Wazanzibari wengi kuwa ni maskini. La kwanza ni uchache wa ajira na hasa katika sekta binafsi. Mhe. Spika, serikali yetu ya awamu ya saba inataka kuhamasisha sekta binafsi iweze kushirikiana na serikali katika kuwekeza hasa kwa njia ya *Public Private Partnership* kwa maana ya ushirikiano baina ya serikali na sekta binafsi, ili tuweze kuzalisha ajira nyingi zaidi na wananchi wetu waweze kupata ajira kupitia sekta binafsi badala ya kukimbilia serikalini peke yake.

Lakini la pili Mhe. Spika, ambalo linasababisha Wazanzibari wengi kuwa ni maskini ni kasi ya ongezeko la idadi ya watu. Mhe. Spika, Zanzibar tunakua sana. Ukitazama takwimu za sensa iliyopita inatwambia kwamba mwanamke mmoja mpaka afikie kipindi chake cha kusita uzazi ana watoto watano. Hiyo ni idadi kubwa sana hasa ukizingatia kwamba hali halisi ya uchumi wa Zanzibar. Kwa maana hiyo, kasi ya ongezeko la watu nayo vile vile inachangia katika kuongeza udogo au kupunguza mapato ya kila mwananchi wetu.

Mhe. Spika, takwimu zinatuonesha kwamba asilimia 40 ya *population* yetu ni watoto walio chini ya umri wa miaka 18. Huo ni mzigo mkubwa Mhe. Spika. Lakini pia asilimia 6 ya *population* yetu ni wazee ambao wana umri zaidi ya miaka 65. Hawa wote wanahitaji kulelewa na hichi kisehemu kidogo kilichobakia hapa kati kati. Kwa hiyo, huo ni mzigo mkubwa Mhe. Spika, kuna haja vile vile ya kuangalia.

Mhe. Spika, ninachotaka kusema ni kwamba kama alivyoeleza Mhe. Rais katika hotuba yake kimbilio kubwa la Wazanzibari ni serikalini kwa upande wa ajira au sekta ya kilimo. Ukitazama kilimo nacho uzalishaji wake nao ni mdogo. Serikali yetu kama Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili alivyoeleza na sasa hivi Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais amegusia tutatilia mkazo sana katika kilimo cha umwagiliaji.

Mhe. Spika, nawaomba sana Wazanzibari waelekeze nguvu zao katika kilimo cha mboga mboga hasa kwa kutilia maanani kwamba ukubwa wa sekta ya utalii iliyopo Zanzibar. Tukijiimarisha katika kilimo cha mboga mboga hasa huko chini tunaweza kwa kiwango kikubwa tukapunguza huu ukali wa umaskini tulionao hivi sasa.

Lakini pia Mhe. Spika, jukumu la serikali ni nini hasa kwa upande wa kilimo. Jukumu la serikali ni kumuwezesha mkulima kuweza kulikaribia soko kwa maana ya kwamba kumuwekea miundo mbinu. Tunashukuru kwa kusema kwamba leo barabara ziko kila pembe ya Zanzibar yetu kwa maana kwamba mkulima anaweza akalifikia soko kwa urahisi zaidi. Sasa hakuna sababu kwa nini tusiimarishe kilimo hasa kilimo cha mboga mboga na kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo, serikali ya awamu ya saba itatilia mkazo na kuweka fedha za kutosha katika maeneo hayo.

Mhe. Spika, sisi sote ni mashahidi sasa hivi nishati imesambaa asilimia 75 katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Nishati hii sio tuitumie kwa kuwasha taa na kuzima taa. Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili amesema hapa kwamba kama kuna mazao ambayo yanaharibika sasa ni wakati mazao hayo yaweze kuhifadhiwa kwa kutumia nishati tuliyonayo.

Lakini pia Mhe. Spika, kwa upande wa mawasiliano ya simu kama zamani ilikuwa unatafuta siku nzima kufanya mawasiliano ya kutafuta soko la nje sasa hivi hutafuti tena siku unatafuta dakika tu kuweza kuwasiliana na masoko ya nje. Kwa hiyo, umuhimu upo, hii miundombinu tuliyonayo ambayo tayari serikali imeshaweka kuna haja kubwa kwa wananchi wetu kuanza kuitumia kwa faida na manufaa yetu.

Mhe. Spika, nini cha kufanya ili tuweze kupunguza au kuongeza mapato ya kila mmoja wetu. Kwanza Mhe. Spika, tuhakikishe kwamba wananchi wetu wanaingia katika kilimo cha mboga mboga ambacho kwa sehemu kubwa kitatusaidia. Leo ukitazama takwimu zaidi ya asilimia 80 ya mboga mboga hazizalishwi hapa Zanzibar wakati tayari tuna maeneo ya kuweza kuzalisha mboga mboga za kutosha kuweza kuisaidia sekta ya utalii.

Mhe. Spika, nimezungumza na Mhe. Hamad Masoud Hamad wa Jimbo la Ole kule kwake tayari ameshaanzisha vikundi vya kulima vitunguu. Ninaamini kama sote Waheshimiwa Wawakilishi katika maeneo yetu tutafanya jitihada hizo tunaweza tukapunguza lile pengo wanaloliona la uhaba wa mapato miongoni mwa wananchi wetu.

Lakini pia Mhe. Spika, lazima tutoe elimu ya ujasiriamali kwa wananchi wetu. Leo wananchi wetu wanataka kufanya biashara lakini elimu ya kufanya biashara hawana. Ukimuuliza unataka kufanya biashara gani anakwambia yoyote tu, hakuna biashara inayoitwa yoyote tu. Ukimuuliza unataka mtaji wa kiasi gani anakwambiwa chochote tu, hakuna mtaji unaoitwa chochote. Mhe. Spika, hii inaonesha dhahiri kwamba kuna haja ya kuangalia jinsi ya kuweza kuwasaidia wananchi wetu katika kuwapatia elimu ya ujasiriamali.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo Waheshimiwa Wawakilishi walitaka kupata ufafanuzi ni suala la kupunguza utegemezi. Mhe. Spika, nataka niwaambie ni kweli kwamba serikali yetu kwa kiwango kikubwa inategemea mikopo na misaada kutoka nje. Bajeti hii tunayokwenda nayo mapato ya ndani ni bilioni 171 ukilinganisha na bajeti yetu ya bilioni 444.

Mhe. Spika, kuna sababu nyingi sana za kufanya bado tuendelee kutegemea wenzetu kutoka nje. Lakini kama nia tunayo basi kidogo kidogo tunaweza kupunguza utegemezi. Kwanza Mhe. Spika, bado tunahitaji fedha nyingi kwa ajili ya kujenga miundombinu hasa tukitilia maanani miundombinu ya bandari, uwanja wa ndege, barabara, umeme asilimia 25 iliyosalia lazima nayo tuweze kuitafutia fedha ili tuweze kuikamilisha.

Lakini Mhe. Spika, katika bajeti yetu bilioni 83 ni mishahara tu, ni sawa na asilimia 40 ya *recurrent budget,* ni sawa na asilimia 18 ya bajeti yetu yote, ni sawa na asilimia 10 ya pato letu la taifa. Ukweli ni kwamba kiwango hicho ni kikubwa sana. Aidha, huku upunguze au uongeze uchumi ili uweze kufikia kile kiwango cha asilimia 10 au chini ya asilimia 10 ya kiwango cha pato la taifa.

Mhe. Spika, ukurasa wa 14 wa hotuba ya Mhe. Rais ameeleza jinsi ya kuishirikisha sekta binafsi kwa kutumia utaratibu kama nilivyoeleza wa *Public Private Partnership* ili sekta binafsi nayo iweze kuchangia katika sehemu

kubwa. Sekta binafsi itakavyoshiriki katika ujenzi wa miundombinu serikali itakuwa haina haja ya kukopa, kwa hiyo fedha zetu nyingi zitakuwa sio za utegemezi na huo ndio utaratibu sasa hivi dunia nzima unautumia.

Mhe. Spika, pia nataka nieleze kwamba sasa hivi kiwango cha utegemezi ni zaidi ya asilimia 60 katika bajeti yetu. Lengo la serikali ni kupunguza awamu kwa awamu utegemezi na nia hiyo tunayo na hatimae Mwenyezi Mungu akitusaidia tutaweza kupunguza utegemezi.

Lakini katika kutekeleza hilo Mhe. Spika, kuna mambo ya msingi lazima sote sisi kwa umoja wetu tuyasimamie na tuyatekeleze. Kwanza tuzalishe zaidi hasa kwa kutilia maanani kwamba kwa upande wa kilimo tuweze kutumia umwagiliaji, tuweze kutumia mbolea na tuweze kutumia mbegu bora.

Lakini pia Mhe. Spika, Zanzibar ni kisiwa hatuwezi tukategemea sana kilimo hatuna ardhi hiyo lazima tutegemee huduma. Huduma za utalii, huduma za kibenki, huduma zinazotolewa katika bandari na kadhalika, hayo ndio yatakayotupelekea tuweze kuondokana na utegemezi.

Mhe. Spika, mimi nimekabidhiwa tu sekta ya fedha, lakini tuna haja kwa umoja wetu sote tushiriki kwa ukamilifu kuziba mianya hii ambayo wenzetu wanakwepa kodi.

Lakini pia Mhe. Spika, kuna sekta kama ya uvuvi nayo lazima tuipe kipaumbele. Nia ya serikali ya awamu ya saba ni kutoa kipaumbele katika sekta ya uvuvi ili nayo iweze kuchangia katika pato la taifa. Kwa hivi sasa sekta hii inachangia chini ya asilimia 5 ambapo ni kiwango kidogo sana ukilinganisha na rasilimali tuliyonayo huko baharini.

Vile vile Mhe. Spika, lazima tukubali kupunguza misamaha ya kodi. Hili ni jambo ambalo tunalisimamia na tutaleta marekebisho ya sheria mbali mbali ili tuweze kupunguza misamaha ya kodi na hatimae Mhe. Spika, tutafika kuweza kuupunguza utegemezi.

Mhe. Spika, dira inatwambia kwamba lazima kama ni kisiwa asilimia 50 ya ajira basi ziende katika huduma kwa maana ya utalii na viwanda, hilo ndio lengo letu. Hapa utaona kwamba asilimia 30 zimeelekezwa katika sekta nyengine. Leo hii tunazungumzia asilimia 28 za ajira basi ziko katika sekta ya serikali, wakati asilimia 30 zimeambiwa sekta nyengine. Kwa hiyo, kuna haja nalo kuliangalia zaidi hasa kwa upande wa Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Spika, nataka nimalizie kwa kusema kwamba tuna nafasi kubwa sana ya kukua kiuchumi. Tunataka sana tuigeuze Zanzibar iwe ni sehemu ya kuuzia mafuta sio sehemu ya kuzalisha mafuta. Tunaweza tukauza mafuta kwa maana ya *bankery*, kwa maana meli zote zinazopita hapa zinaweza zikajaza mafuta Zanzibar, ndege zote zinazokuja hapa zinaweza zikatia mafuta Zanzibar. Lengo hilo tunalo na lengo hilo litatusaidia kuiweka Zanzibar kama ni sehemu ya huduma. Tunachokiomba Mhe. Spika, ni kwamba amani na utulivu tuendelee kuwa nao ili kila mmoja wetu aweze kufaidi matunda ya Mapinduzi.
Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja, ahsante.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii ya kuchangia katika hotuba ya Mhe. Rais. Mhe. Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kufika hadi leo *Alhamdullilah* tuko katika hali ya furaha, uzima na afya.

Mhe. Spika, pili nakupongeza wewe binafsi kwa kuteuliwa kwako kuwa Spika wa Baraza hili. Hii inaonesha dhahiri kwamba hekima zako na uwezo wako unathaminiwa sana na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, pia naomba kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Mhe. Rais kwa hotuba yake nzuri ambayo itakuwa ndio dira yetu katika miaka mitano yote katika kufanya kazi zetu kama mawaziri wa serikali ya awamu ya saba.
Mhe. Spika, nachukua fursa hii vile vile kumshukuru Mhe. Rais kwa kunichagua mimi kuwa Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, imani yake hii imenipa motisha kubwa kabisa ya kufanya kazi hii. Ninamuahidi kwamba nitafanya kazi hii kwa uadilifu na kwa nguvu zangu zote. Vile vile nachukua fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Mtoni kwa kunichagua mimi kuwa mwakilishi wao.

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba nipitie yale masuala ambayo baadhi ya wajumbe walichangia katika mchango wao wa kuchangia hotuba ya Mhe. Rais.

Mhe. Spika, suala la kwanza lililochangiwa sana hapa na wajumbe ni suala la ubora wa bidhaa na kupanda bei kwa bidhaa katika kipindi hichi. Mhe. Spika, naomba kukiri kwamba kweli bidhaa nyingi zinazoingia nchini ziko chini ya viwango na hasa vyakula. Hiyo ni sababu kubwa inayotufanya wizara yetu kuandaa kwa haraka sana na kuleta katika Baraza lako tukufu ile sheria ya kuunda *Zanzibar Bureau Standard (ZBS)* ili kuweza kudhibiti hali hiyo isiendelee.

Mhe. Spika, kwa kuwa dhamira yetu ni kuifanya Zanzibar kuwa kitovu cha biashara basi ni lazima tujikite katika masuala ya kuwa na vyakula pamoja na vitu vyote vitakavyokuja Zanzibar viwe katika viwango vya kimataifa.

Mhe. Spika, ni ukweli usiopingika kabisa kwamba wananchi wanalalamika sana kutokana na upandaji wa bidhaa hasa kuanzia mwezi wa Oktoba hadi hii leo. Kwa kweli katika mwezi wa Oktoba na kabla ya hapo ilikuwa ni mwezi wa uchaguzi kwa hiyo wafanyabiashara wengi sana walifanya woga na hawakuweza kuagiza bidhaa kwa kipindi hicho. Kwa hiyo, katika kipindi cha mwezi wa Oktoba na mpaka leo bidhaa bado hazijaingia nchini. Ni matarajio yetu kwamba kuanzia mwezi wa Februari ndio bidhaa zitaingia nchini. Kama tunavyojua kwamba bidhaa zikiadimika upandaji wa bei vile vile huwa mkubwa.

Mhe. Spika, pia nilitaarifu Baraza lako tukufu kwamba kwa mwaka huu 2011 tunakabiliwa na upandaji wa bei za vyakula katika soko la dunia. Katika mwezi wa Oktoba mchele ulikuwa ukiuzwa dola 480 mpaka Zanzibar kwa tani. Vile vile mwezi wa Novemba mchele ulipanda bei ukafikia dola 560, mwezi wa Disemba mchele ulifikia dola 610 kwa tani. Kwa hivyo, ongezeko la bidhaa ya mchele imeanzia 480 mpaka imefikia sasa hivi 610 katika soko la dunia.
Vile vile sukari imepanda bei kutoka dola 700 katika mwezi Oktoba mpaka kufikia dola 880 katika mwezi wa Disemba na huu mwezi wa Januari sukari imefikia dola 900 kwa tani.

Mafuta ya kupikia yameongezeka bei kutoka dola 19.2 mpaka kufikia dola 26 baina ya mwezi Oktoba na mwezi wa Disemba. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba bei za bidhaa zimeongezeka kwa kiwango kikubwa katika soko la dunia. Lakini hii haikuwa sababu tosha kwa wafanyabiashara kuongeza bei za bidhaa ambazo zilikuwa zimeshaingia nchini kabla ya mwezi wa Oktoba. Wafanyabiashara wametumia mwanya huu wa kupanda bei kwa vitu na wao wakaongeza bei za vitu hapa hapa Zanzibar zikafikia kutoka paketi moja ya mchele Shs. 40,000/- hadi kufikia Shs. 47,000/- mpaka Shs. 48,000/-.

Mhe. Spika, hali hii inampelekea mtumiaji ambaye ananunua mchele kwa reja reja kununua paketi moja kwa Shs. 55,000/-. Hili ni ongezeko kubwa sana la bei ambalo kwamba limetushtua sana na tumechukua kila adhari kuwaita wafanyabiashara, kuongea nao na kuona kwamba wanapunguza bei hizo.

Suala hili Mhe. Spika, ni muhimu sana na tunalifanyia kazi. Katika kurekebisha sheria yetu ya biashara ambayo itakuja mwezi wa Machi katika Baraza lako tukufu, hili tumelizingatia sana. Namna gani tutaweza ku-*regulate* bei za bidhaa kuliko kuwaachia soko huria likenda likawa huru bila kiasi kwa kiasi hichi.

Mhe. Spika, hata ule mchele uliopatikana juzi Pemba ambo ulibainika kwamba hauna viwango. Yule muuza mchele amewauzia wafanyabiashara Shs. 42,000/- kwa paketi moja, lakini wafanyabiashara wale wameuza mchele ule kwa Shs. 48,000/-. Kwa hivyo, wale wafanyabiashara kule Pemba wameweka faida ya Shs. 6,000/- kwa kila paketi moja, zaidi ya faida ambayo ameiweka yule mfanyabiashara aliyeleta ule mchele kutoka Pakistani. Kwa hivyo, inaonesha kwamba wafanyabiashara wakipata upenyu wanautumia

Mhe. Spika, natumia fursa hii kuwatahadharisha wafanyabiashara hawa kwamba wasije kulalamikia na *income tax* watakapowafuata kudai ile haki yao kutokana na faida hiyo kubwa waliyoipata kutoka kwa wananchi. Naomba wafanyabiashara wote washirikiane na sisi yaani serikali kwa kupitia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kuona kwamba tunawahurumia wananchi wetu kutokana na kupandisha bei kiholela.

Vile vile Mhe. Spika, katika hotuba yetu hii, katika ukurasa wa 20 mpaka 21 Mhe. Rais amezungumzia sana masuala ya viwanda vidogo vidogo na viwanda vya kati. Lengo la serikali yetu ni kuona kwamba viwanda vidogo vidogo na vya kati vinaimarishwa ili tuweze kuzalisha mali na kuuza nchi za nje, na kupunguza urari wa kibiashara baina ya kusafirisha na kununua.

Pia Mhe. Spika, suala la viwanda litatusaidia sana katika kujenga ustawi wa soko la ajira katika nchi yetu. Fursa za ajira kwa vijana na vile vile kuingiza teknolojia mpya na kujenga uhusiano wa kutegemeana na sekta nyengine katika sekta za biashara, utalii na kadhalika. Mhe. Spika, wizara yetu imejiandaa kikamilifu katika kukabiliana na suala hili na kuona kuwa viwanda vinashamiri nchini na ajira inashamiri nchini vile vile.

Mhe. Spika, suala la ujasiriamali kwa kuona umuhimu wake katika muundo wetu wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko tumeweka kurugenzi maalum ambayo kwamba itashughulikia na wajasiriamali. Hii itasaidia sana kujenga msingi madhubuti ambao utawaweka wajasiriamali katika mkakati maalum wa kuweza kuwaunda na kuwaboresha, ili waweze kufanyakazi zao kwa maslahi ya nchi yetu na vile vile itasaidia sana katika suala la ajira.

Mhe. Spika, suala la ubora wa bidhaa tutalijadili katika sheria yetu inayokuja Jumatatu, na naamini kwamba Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako, watachangia kwa ukamilifu na watafurahi kuona kwamba sasa hivi Zanzibar inakwenda kwa kutumia viwango, na hitokwenda tena kiholela holela. Kwa hivyo, yale masuala ya mapembe na wenziwe mapembe wote yatatoweka katika kipindi kifupi katika mwaka huu *Inshaallah (Makofi).*

Mhe. Spika, nawaomba wananchi wote wawe wastahamilifu katika kipindi hiki kigumu, kwa imani kwamba serikali yao inajali sana shida zao na inachukua yote haya kwa uangalifu mkubwa na kuyatatua kwa kipindi kifupi kijacho.

Mhe. Spika, suala la kuwa na ghala la akiba, hili ni suala muhimu sana. Kwa sababu katika kipindi hiki ambacho bidhaa zimeadimika, kama tungekuwa na ghala la akiba basi lingetusaidia sana katika kupunguza bei na vile vile kuondosha ile kasma iliyokuwepo sasa hivi ya kukosekana kwa chakula nchini. Kwa hivyo, wizara yetu ikishirikiana na serikali kuu yaani Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, itaandaa mikakati maalum kuona kwamba tunakuwa na maghala ya akiba ambayo tutaweka bidhaa zetu ndani ya maghala yetu ambayo kwamba yatatufaa wakati wa dhiki. Hatuwezi kuondelea na hali hii ya kuwaamini moja kwa moja wafanyabiashara kuleta bidhaa nchini bila ya kuwa na maghala ya akiba ambayo yatakuwa na chakula cha akiba wakati wote.

Mhe. Spika, baada ya kupanda bei katika mwezi wa Disemba kwa vyakula vyote, vyakula vinavyoagizwa nje hata vyakula vinavyoagiziwa kutoka Tanzania Bara. Baada ya kuangalia njia zote hizo zinazotumiwa kuleta vyakula kutoka Tanzania Bara na kutoka nje na mazungumzo ya kina na wafanyabiashara, kuanzia mwezi wa Januari wiki ya kwanza mpaka wiki ya tatu tunashukuru kwamba kuanzia hapo hakujapanda bei kitu chochote kile, isipokuwa unga wa ngano kidogo ulipanda kwa Shs. 150. Kwa hivyo, tunaamini kwamba wafanyabiashara wamekuwa wasikivu na watatusaidia katika suala hili.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa tamko rasmi kwamba kwa niaba yangu na niaba ya wizara yangu tunaunga mkono hotuba ya Mhe. Rais na tutaifanyia kazi kikamilifu *Inshaallah* tutafanikiwa, ahsante sana Mhe. Spika, *(Makofi).*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Mawaziri, tujitahidini kubana muda kidogo, kwa sababu mtoa hoja najua tunamsaidia, lakini aje apate muda kidogo wa kuweza kufafanua mengi ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameyasema katika hotuba hii.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote kufika hapa tukiwa wazima.

Pili napenda niwashukuru uongozi wa juu ya nchi yetu wakiwemo Mhe. Rais, Mhe. Makamo wa Kwanza na Mhe. Makamo wa Pili kwa miongozi yao ambayo wanatupa katika utendaji.

Lakini tatu, napenda niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Mgogoni kwa kunichagua tena kuwa mwakilishi wao.

Mhe. Spika, kama nilivyosema tarehe 11/11/2010 wakati nikitoa neno la shukurani kwa hotuba ya Mhe. Rais. Nilisema kwamba hotuba hii ni dira ambayo sisi kama mawaziri sasa tutaifanyia kazi kikamilifu. Katika michango ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wajumbe, wizara yangu ilikuwa na mambo mawili. Suala la kwanza lililozungumziwa ni mahakama.

Mhe. Spika, ni kweli napenda nikubali kwamba kuna matatizo katika mahakama zetu, lakini matatizo haya ni mengi kidogo yakijumuisha pamoja na wafanyakazi wenyewe hasa kwa upande wa mahakimu. Zaidi ya hivyo ni kwamba matatizo mengine ni vitendea kazi vikiwemo vile vyumba vya kuendeshea zile kesi zenyewe. Kwa maana hiyo, kwa sababu mahakimu ni kidogo, vyumba vya kufanyia kazi ni kidogo, maana yake hakimu mmoja mpaka amalize ndio aende hakimu mwengine, kwa hivyo bila shaka kutakuwa na ucheleweshaji wa kesi. Haya Mhe. Spika, tumeyaona na tumeshaanza kuyafanyia kazi na naamini baada ya muda kidogo basi matatizo haya yatapungua sana.

Mhe. Spika, suala la pili lililozungumzwa ni kuhusu vyeti vya kuzaliwa kwamba navyo vina matatizo. Ni kweli katika vyeti vya kuzaliwa kulikuwa kuna matatizo ya aina tatu. Tatizo la kwanza ni pale kwenye Afisi yetu maarufu tunaita Mambo Msiige. Lakini la pili ni vyeti ambavyo vilikuwa vinatolewa katika mawilaya. La tatu ni vyeti vinavyoitwa *late registration*, yaani uandikishaji wa vyeti uliochelewa.

Mhe. Spika, tatizo la vyeti kwenye afisi yetu tuliliona na napenda niliarifu Baraza lako tukufu kwamba tatizo hili sasa tumeshalisawazisha, na kwamba mtu yeyote ambaye anakwenda pale basi atapata cheti chake katika wiki mbili na sio zaidi ya hapo. Kwa hivyo, suala la ucheleweshaji tumeshaliondoa kwa hapa. Tatizo liliopo ni tatizo la mawilayani, na hii ni kwa sababu ya mdorongo ambao upo mpaka kupata cheti chako.

Mhe. Spika, hivi sasa tumeshatoa taarifa kwa wakuu wa wilaya tunataka kukaa nao, ili tuweze kupunguza mdorongo huo wa uandikishaji, naamini tukishafanya hivyo tukijaaliwa nako huko wilayani upatikanaji wa vyeti nao utapungua sana na hautochelewa. Mhe. Spika, tunavyotaka iwe ni kama afisi kuu yaani baada ya wiki mbili mtoto anapozaliwa basi apate cheti chake.

Tatizo la tatu ni suala la *late registration*. Suala hili Mhe. Spika, napenda niliarifu Baraza lako tukufu kwamba litachukua muda kidogo, kwa sababu

tatizo ni kwamba kuna *duplication* nyingi za *late registration*, kutokana na ule utaratibu wake. Kwa sababu mtu anapojaza anakwenda kula kiapo mahakamani na akishakurejea basi fomu ile itakuwa ni halali kupewa cheti. Lakini tumegundua kwamba kuna udanganyifu mkubwa, kwa sababu mtu mmoja anaweza akenda kula viapo mara tatu, inategemea ni shughuli zipi ambazo anazitaka. Anaweza akenda kuandikisha jeshi kwa mfano akala kiapo, kufika kule akakataliwa.

Kwa hivyo, ikija nafasi nyengine ya polisi au ya shughuli nyengine atakwenda tena kula kiapo kwenye mahakama nyengine na atakwenda kuandikisha. Kwa hviyo, mtu mmoja anaweza kuwa na vyeti vitatu mbali mbali, na hiyo tumeshaigundua. Sasa suala hili tunalifanyia kazi ili kuweza kudhibiti utoaji wa vyeti kiholela kama hivi naamini baada ya muda mfupi tukijaaliwa tunaweza tukapata ufumbuzi na tatizo hilo litaondoka.

Kwa ujumla Mhe. Spika, napenda niseme kwamba matatizo haya kweli yapo na tumeshaanza kuyafanyia kazi na *Inshaallah* tutayafanyia kazi kwa muda mfupi tunaweza tukayakamilisha na kukawa hakuna tatizo katika suala hili.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo na mimi kwa upande wangu na kwa upande wa wananchi wangu wa Mgogoni, tunaunga mkono hotuba ya Mhe. Rais kwa asilimia mia moja, ahsante *(Makofi).*

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwanza mimi nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kusimama hapa na kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya Mhe. Rais wa Zanzibar.

Pili nakupongeza kwa kuchaguliwa tena na Baraza hili kuwa Spika wa Baraza la Wawakilishi. Vile vile nampongeza Mhe. Rais kwa kutoa hotuba nzuri ambayo ni dira kwetu sisi, itatusaidia sana katika miaka mitano hii.

Pia namshukuru kwa kuniteua mimi kuingia katika Baraza lako tukufu kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi. Vile vile kunipa jukumu la kushughulikia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Naahidi kwamba kwa kadiri ya uwezo wangu nitaifanya kazi hii na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atanisaidia.

Mhe. Spika, hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar ni muhutasari wa yale mengi ambayo alikuwa akiyazungumza wakati alikuwa akitafuta kura kutoka kwa wananchi, ahadi za aina mbali mbali.

Mhe. Spika, kwa upande wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ukiisoma hotuba ya Mhe. Rais inazungumzia juu ya suala la kukuza au kuboresha elimu ya lazima, yaani kuanzia *Nursery School* mpaka *Form Four* na Elimu ya Fursa

ile ya *Form Five* na *Six*, Vyuo Vikuu, Vyuo vya Ufundi, Vyuo vya Amali, Elimu Mbadala na Elimu Mjumuisho. Hayo ni mambo ambayo ni jukumu kwa wizara hii ambayo imekabidhiwa na naahidi kwamba nitayashughulikia kwa kadiri nitakavyoweza.

Mhe. Spika, lakini mkazo mkubwa ilikuwa ni kuboresha elimu sasa hivi, kuwa na *quality education* na ndio maana Mhe. Rais akawa anazungumzia sana suala la kuhakikisha kwamba suala la matatizo ya madawati, suala la vifaa vya sayansi na suala la madarasa kuwa na wanafunzi ambao wasiozidi 35, ni jukumu ambalo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imekabidhiwa na inalishughulikia. Katika suala hili wizara italazimika kuandaa miradi mbali mbali ambayo itasaidia kutatua tatizo hili.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe walipozungumza wamegusia maeneo ambayo ni vizuri na mimi nikayagusia. Suala la kwanza ni la kuchangia elimu na watoto kutokuandikishwa kwa sababu wazee wao wameshindwa kuchangia elimu.

Mhe. Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali haikulenga hivyo, kwamba mwanafunzi anayeshindwa kuchangia basi asiandikishwe katika kusoma. Kwa sababu lengo ni kwamba watoto wote wa nchi hii ni lazima wapate elimu. Nadhani hili ni suala ambalo inabidi kamati za wazee zilizomo katika mashule waweze kushirikiana na wazee wenzao na ndio jukumu kubwa ambalo wamepewa kufahamu huu umuhimu wa kuchangia. Fedha ambazo wanachangia inakuwa ni kama *school fine* na inawasaidia wao wenyewe. Na wao wazee wanawajua nani mwenye uwezo na nani asiye na uwezo wa kuchangia. Lakini hata hivyo hairuhusu kwamba yule ambaye hakuchangia mwanawe asiandikishwe.

Mhe. Spika, nakumbuka hata ule wakati ambao sisi tulikuwa tukilipa ada ya skuli, basi tatizo kama hili likitokea basi masheha walikuwa wanahusika moja kwa moja kwa kutoa ufafanuzi mzuri, kwa wakati ule mamudiri na tukifikiriwa kiasi gani upunguziwe mchango ule. Hili lilikuwa likifanyika ni suala mbalo linaweza likafanyika kwa kushirikiana na kamati ya wazee, masheha kwenye maeneo yao, ili kuhakikisha kwamba nani mwenye uwezo na nani hana uwezo. Lakini suala la kuandikishwa mtoto kuingia skuli ni lazima kwa wote kabisa.

Halafu suala jengine lililozungumzwa ni suala la vifaa vya sayansi. Mhe. Spika, vifaa vya sayansi serikali imechukua uamuzi makusudi kabia wa kuhakikisha kwamba vifaa vya sayansi vinakuwemo katika maskuli. Navyo vimeagizwa na vimefika hapa na vimegaiwa, isipokuwa ilionekana kwamba kama kila skuli itapewa vifaa vya sayansi, basi vifaa vitakuwa kidogo sana na havitatosheleza, kwa sababu huo mradi wenyewe wa kuendelea kununua vifaa vya sayansi

unaendelea na watoto hivi sasa hivi tayari wako madarasani. Kwa hivyo, ni vizuri wakakubaliana wenyewe kwamba ni vizuri viwepo katika *TCs* na walimu waliokuwa na haja navyo wanakwenda katika *TCs* zile wanachukua katika vituo vyao vya ualimu, wanachukua na wanakwenda kutumia katika shule zao.

Mhe. Spika, kwa kuanzia baadhi ya skuli nakumbuka mimi zimepewa ni Skuli ya Sekondari ya Benbela, Haille Selasie, Lumumba, Chuo cha Kiilamu Mazizini na baadhi ya *TCs* kama Bububu, Kiembesamaki, Kitogani, Dunga na Mkwajuni wamepewa vifaa vya sayansi na vipo na ni jukumu la walimu kuvifuatia na kwenda kuvichukua kwa ajili ya kusomeshea sayansi katika skuli zao.

Kwa Pemba Skuli ya Sekondari ya Konde, Chuo cha Kiislamu Micheweni. Vituo vya walimu kama Michakaeni, Mizingani, Mitiulaya, Wingwi pia wamepewa na walimu wakuu wanajua kwamba wakitaka vifaa vya sayansi waende wape, huo ndio utaratibu wa kuanzia. Bila shaka utaratibu huu utabadilika kadiri ya wingi wa vifaa vya sayansi vitakapokuwa vinapatikana. Mhe. Spika, nakubaliana na Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kwamba sasa ni wakati wa kukuza sayansi wala sio vyenginevyo.

Mhe. Spika, tuna nia hata ya kukuza uwezo wa walimu kusomesha sayansi. Tuna mradi ambao tunauita ni *basic education* ambao tunashughulikia masuala haya ya kuwawezesha walimu wetu kusomesha sayansi kwa kutumia vituo vyetu vya *TCs* pamoja na vyuo vya ualimu, ili kuwasaidia walimu kuwakuza uwezo wao juu ya suala la kuweza kusomesha sayansi katika skuli zetu. Ndio maana hata *World Bank* wakatusaidia tukaweza kupata vitabu vya sayansi kwa ajili ya *secondary schools* ambavyo tunavyo, vitaendelea kutumika na vitaishi kwa muda wa miaka mitano bado tutaendelea kuwapa na kila mwanafunzi atakuwa na kitabu chake katika secondary schools cha kusomea sayansi. Hiyo ndio shabaha ambayo tunaendelea nayo ili kuweza kupata ile niliyoizungumza mwanzo kwamba ni *quality education*.

Mhe. Spika, nakubaliana na wenzangu kwamba sasa hivi ni vizuri kuwaandaa vijana wetu kuweza kuja kuishi popote kisayansi na kiteknolojia. Hili ni suala muhimu na ndio nia ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuwafikisha watoto katika hatua hiyo. Mhe. Spika, tuna mradi sisi tunataka kuuanza hivi karibuni tu na pengine mwisho wa mwezi huu au mwanzo wa mwenzi ujao wa kuwapatia vijana wetu mafunzo maalum kuanzia darasa la kwanza mpaka darasa la kumi na mbili kuwapatia mafunzo ya kompyuta *ICT*, tutakuwa tunawasomesha katika maeneo hayo. Mtu anaweza kukuuliza kwamba kompyuta mbona kubwa, *laptop* ndio kompyuta yenyewe, ukiipata ile unaweza kuihamisha kutoka darasa moja kwenda jengine na jengine. Pia katika hatua

hiyo tuna shabaha ya kujenga uwezo wa walimu wetu ili waweze kuzisomesha hizo kompyuta katika maeneo hayo.

Mhe. Spika, kuna tatizo la ukosefu wa madawati. Tatizo hili tunalikubali na kusema kweli ni lazima tufike mahala uwe ni mradi kabisa. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba wazee wamefahamu umuhimu wa kuwapeleka watoto mashuleni, ndio maana watoto wanapelekwa mashuleni kwanguvu sana madawati hayatoshi kusema kweli, ni lazima tuwe na mradi maalum wa madawati na wizara yangu italifanyia kazi suala hili ili kuona kwamba wanafunzi mashuleni wanapatiwa madawati.

Lakini suala hili Mhe. Spika, linakwenda sambamba na madarasa yenyewe katika kuyajenga. Tunataka kujitahidi kwamba mabanda yote yaliyokwisha kujengwa kwa ajili ya madarasa basi tuyaezeke, hiyo ndio shabaha yetu. Tuyaezeke tuyamalizie plasta pamoja na saruji ili tupate kutanua vyumba vya madarasa badala ya kuwa mwalimu mmoja anasomesha wanafunzi 130 au 120 kwa wakati mmoja, ambayo ni kazi ngumu sana Mhe. Spika, ni lazima tuweze kulishughulikia vizuri suala hili.

Mhe. Spika, nije kwenye suala zito la mikopo. Mhe. Spika, ni kweli sio wanafunzi wote wanaoweza kupata mikopo, ni kwa sababu ya uwezo wa nchi yetu katika kutoa hiyo mikopo mpaka sasa hivi. Jambo moja ambalo Zanzibar kwa jumla tumebahatika sana ni kwamba siku hizi tunapata walimu ambao wanamaliza kidato cha kumi na nne wengi wanao *qualify* kuingia katika vyuo vikuu. Kwa hivyo, ni wengi kiasi ambacho ule uwezo wetu wa kimapato kuweza kuwakopesha wote mikopo inakuwa sio rahisi. Sasa hivi tunatizama mkazo tuuweke wapi na mahitaji yetu katika nchi ni sehemu gani. Sasa hivi tunaanza kuelekea kwenye sayansi, tunataka wanafunzi ambao wana uwezo wa kuendelea na sayansi wale ndio tuweze kuwapatia mikopo kwa sababu tunahitaji watu wa sayansi hivi sasa walio wengi.

Mhe. Spika, tuna walimu wengi kabisa wa *art*, kwa kweli walimu wengi tulionao sasa ni walimu wanaosomesha Dini, Kiswahili na Kiarabu katika skuli mbali mbali. Lakini tunataka tuweke mkazo kwenye somo la sayansi, kwa sababu ndio ulimwengu tunaokwenda nao. Kiasi tunachoomba hatuwezi kukipata chote, huo ndio ukweli kwa sababu huyo sungura wenyewe ni mdogo, tunagawana wizara zote. Sasa hatuwezi kutimiza kila wizara ikapata kile anachokitaka.

Kwa hivyo, tunafanikiwa, tukiomba tunapunguziwa, lakini tukitiliwa tunatiliwa asilimia 57, 63,55 wakati mwengine na asilimia 65 tulitiliwa hivi juzi ya kile tulichokiomba. Ndio hapa asubuhi tulikuwa na suala la kuwa tuliomba 4.5, lakini tukatiliwa 2.5 ambayo ukiitizama inakuja kwenye asilimia 65. Sasa hapo

katika kuchagua watu wa kuwapatia mikopo, lazima tutizame kipaumbele cha nchi yetu, hiyo ndio muhimu sana. Vyuo vikuu vipo na tunawasomesha watoto wetu kwa ajili ya kuja kulisaidia na kulijenga taifa letu hili. Hiyo ndio hali halisi Mhe. Spika. Kwa hivyo, tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe watustahamilie.

Mhe. Spika, hata wenzetu wa Tanzania wamejua kwamba wanafunzi wa sayansi ni tabu kuwapata, ndio maana sasa hivi wanachukuliwa katika karibu vyuo vyote, mwanafunzi wa sayansi ukipata *point* 2.5 basi unachukuliwa kwa ajili ya kusoma sayansi. Lakini kwenye masomo ya *art* ni lazima upate *point* 4.5 ndio uchukuliwe kwenye *art* kwenye vyuo vikuu, ni kwa sababu kwamba wanafunzi wa sayansi ni tabu kuwapata na tunawahitaji tuwapate, ndio maana tukaweka mkazo kwenye mradi huu wa kukuza sayansi zaidi kwenye *basic education* katika maskuli yetu mbali mbali na kuwasaidia walimu kuwajenga uwezo kwa kujiendeleza.

Zaidi ya hayo Mhe. Spika, kwa sababu ya muda ni mfupi nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na kuweza kuzungumza machache juu ya hotuba hii nzuri kabisa ya Mhe. Rais wa Zanzibar, ambayo tunakusudia kuifanyia kazi vizuri kabisa na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatuwezesha. Kwa niaba ya Jimbo langu la Ikulu naiunga mkono hotuba hii, ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii muhimu sana na dira katika nchi yetu, ambayo imetolewa na Mhe. Rais wa Zanzibar tarehe 11/11/2010.

Mhe. Spika, kwanza naomba nikupongeze kwa kunipa hii nafasi na kama walivyosema wenzengu nikupongeze kwa kuchaguliwa katika hii nafasi uliyonayo. Nakumbuka enzi zile za hali siyo nzuri ya kisiasa, ilikuwa kwa kweli unatanzika sana na mambo yalivyokuwa na ulifanya jitihada kubwa. Sasa hali imetengamaa unafurahi na una-*enjoy* kwamba Baraza sasa linakwenda vizuri *(Makofi).*

Pia naomba niwapongeze sana wananchi wa Jimbo la Gando kwa busara zao na uamuzi wao wa kunichagua ili niendelee kuwa mwakilishi wao. Mhe. Spika, alipokuwa akihutubia Baraza hili Mhe. Rais alikusudia kuanzisha mapinduzi ya mifugo na uvuvi katika kitabu chake na katika kuyaendeleza mapinduzi hayo ya mifugo na uvuvi, alitafuta mwana mapinduzi mwenzake amsaidie. Namshukuru sana kwa kuniamini kumsaidia katika shughuli hii ya kusimamia Wizara ya Mifugo na Uvuvi na ninaahidi kwamba nitamsaidia kwa uaminifu sana. Hasa nikitilia maanani kwamba mapinduzi haya yatasimamiwa na Wajumbe wa Baraza lako tukufu. Kwa hivyo, ninaamini kwamba kwa vile

wajumbe hawa wako imara sana katika kuyasimamia mapinduzi haya, basi ninaamini kwamba tutafika salama tukijaaliwa.

Mhe. Spika, katika hotuba hii ambayo imekuwa inajadiliwa tangu jana, nimefurahi kwamba wajumbe wengi wa Baraza lako tukufu wamenisaidia maarifa sana. Kwa hivyo, mimi nachukulia michango yao waliyoitoa katika Sekta ya Uvuvi na Mifugo ni maarifa ya kufanyiakazi. Kwa kweli nitayachukua, ninayathamini pamoja na kunisaidia sana katika kuendeleza shughuli ambazo ninakusudia kuzifanya, nawashukuru wote.

Katika hili Mhe. Spika, kwenye mifugo tunakusudia kuanzisha Vituo vya Utafiti wa Mifugo pamoja na Maabara za Mifugo kuziimarisha, kwa sababu hatuwezi kufuga kama hatuna Vituo vya Utafiti, vyenginevyo tutakuwa tunachunga na nimeambiwa sasa tufuge na wala tusichunge. *(Makofi)*

Vile vile tumekusudia kuimarisha elimu kwa wafugaji. Waheshimiwa Wajumbe wengi walikuwa wakisema hapa kwamba hatuna taaluma ya kutosha na matokeo yake wafugaji wetu matokeo yao baadhi ya ng'ombe hawazalishi vizuri na kuku wanakufa. Sasa hili ni jambo ambalo tumeliona na tutalifanyiakazi.

Mhe. Spika, pia tunakusudia kuanzisha Viwanda vya Kusarifu Bidhaa za Mifugo kwa kushirikiana na Wawekezaji, kwa sababu hili ni tatizo kubwa ambalo lipo hivi sasa. Lakini kwa kuwa tutafanya Mapinduzi ya Mifugo, basi hili ni jambo ambalo tunakusudia kulisimamia.

Suala jengine ambalo tunakusudia kulifanya tunazungumza na wawekezaji kuanzisha *Contact Farming*, ambapo mwekezaji anaweza kuja hapa akaleta mitaji na wananchi wakawa wanafaidika kwa makubaliano maalum. Sasa jambo hili linafanyika katika nchi nyengine na sisi tunaendelea na mazungumzo na wawekezaji na dalili nzuri ipo ya kufanikiwa.

Kwa hivyo, tukifanikiwa hapa yale matatizo ya Vikundi vya Ushirika kwamba havina mitaji na mambo mengine, basi itakuwa suala hili limepata suluhu nzuri. Mhe. Spika, katika mchango uliozungumzwa jana, nataka nimshukuru sana Mwakilishi wa Jimbo la Chambani Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi, pale alipokemea suala la ukatili kwa wanyama. *(Makofi)*

Kwa kweli hatuwezi kudhamiria kuimarisha aina fulani ya mifugo na tukaacha aina fulani ya mifugo iteswe na ifanywe ukatili katika nchi, hilo haliwezekani. Kwa hiyo, lazima kwanza kwa pamoja tupige vita ukatili wa wanyama ambao hivi sasa katika nchi yetu umeshamiri sana.

Hili ni jukumu la kila mmoja wetu, sisi katika wizara tunao mchango wetu na kwa upande wa wananchi, masheha, madiwani na hata Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi nayo nafasi kubwa katika kukemea na kupiga vita suala hili hasa katika maeneo wanayoishi.

Mhe. Spika, nimeambiwa maeneo ya Mwembemakumbi, Amani na Gulioni ni sehemu ambazo suala la ukatili wa wanyama linafanyika kwa kiwango kikubwa sana. Kutokana na hali hiyo, wizara yangu inakusudia kushirikiana na wadau wengine katika nchi mara baada ya Baraza lako tukufu kupanga mikakati ya pamoja kuona kwamba suala hili haliendelei tena katika nchi yetu. Nikiendelea sasa nizungumzie kuhusu suala la uvuvi. Kweli kwamba suala la uvuvi halijapata kutoa mchango unaostahili katika uchumi wa nchi yetu. Kwa kuwa nchi yetu imezungukwa na bahari na hivyo ikiwa na jitihada nzuri, basi uvuvi unaweza kuwa na mchango mkubwa katika pato la taifa ya nchi yetu.

Katika hili Mhe. Spika, ni vizuri kufahamu kwamba kama alivyosema Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwamba *population* ya Zanzibar inakua kwa kasi sana, lakini rasilimali zetu ama zinapungua au zinabakia pale pale. Kwa mfano, mwaka 1988 Sensa ya Watu ilionesha Zanzibar ina watu kama laki 6 na kidogo. Lakini leo *probation* ya Sensa inaonesha tupo karibu milioni 1 na laki 3. Sasa maana yake ni kwamba katika miaka hii michache tumeongezeka zaidi ya asilimia 100 wakati rasilimali za bahari zinaendelea kupungua.

Kwa hivyo, katika hili Mhe. Spika, wizara yangu imepanga mambo matatu. Kwanza kuimarisha uvuvi wa kienyeji. Katika hili tunakusudia kuanzisha vitu vinavyoitwa *Fishing Aggravate Devising*, vifaa ambavyo vinawekwa kwa majaribio katika bahari hivi sasa, ili kuona kwamba wavuvi wetu wa kienyeji wanaweza kuyaendea maeneo ambayo yanakiwango kikubwa cha samaki, kwa lengo la kupunguza kwenda katika maeneo ya uvuvi wa kubahatisha.

Mhe. Spika, tayari tumeshapata vifaa na tunavifanyia majaribio na baada ya muda mfupi vitaweza kutuonesha kwamba vifaa hivyo vinaweza kufanyakazi vizuri kwa Zanzibar. Kwa hivyo, vifaa hivi vikiweza kufanyakazi vizuri, basi hali yetu kwa uvuvi wa kienyeji utakuwa mzuri.

Suala jengine ambalo nimekusudia kulifanya ni kuvutia wawekezaji kwenye Uvuvi wa Bahari Kuu. Mhe. Rais kwenye kitabu chake ukurasa wa 21 naomba kunukuu Mhe. Spika.

Kitabu cha Mhe. Rais, ukurasa wa 21 *paragraph* ya mwisho inasema hivi:-

> “Tutawashajihisha ndugu zetu wa Tanzania wanaoishi ughaibuni, wanaoishi nchi za nje kwa jina la maarufu la Diaspora, ili nao waje wawekeze nchini kwao”.

Sasa hili ni eneo ambalo Mhe. Spika, sisi katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi tunangalia jinsi gani linaweza kutusaidia, sio lazima tupate wawekezaji wa nje, lakini hata Wazanzibari walioko nje wanaweza kuja hapa kwao kuwekeza katika masuala ya Uvuvi wa Bahari Kuu.

Kwa hivyo, naomba kupitia Baraza lako tukufu Mhe. Spika, nitoe wito kwa Wazanzibari walioko nje kwa makusudi kabisa waamue kipato walichokipata, basi wakirejeshe nyumbani kwa ajili ya kuwekeza kwa lengo la kusaidia uchumi wa nchi yao, vizazi pamoja na ndugu zao walioko nyumbani.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo tumelikusudia ni Ufugaji wa Mazao ya Baharini. Hili pia ni suala linaloweza kutusaidia sana, kama tunavyosema kwamba kwa vile rasilimali ya bahari hasa katika maeneo ya maji madogo zinaelekea kutoweka kwa wingi.

Kutokana na hali hiyo, suala la ufugaji wa mazao ya baharini samaki, chaza, kome pamoja na viumbe vyengine vya bahari vinaweza kuisaidia nchi yetu sana. Kwa kweli kuna nchi ambazo zimepiga hatua kubwa sana katika suala hili na wameweza kuongeza pato la taifa.

Mwisho Mhe. Spika, kuna baadhi ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walizungumzia suala la Uvuvi pamoja na Mitego Haramu. Sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi lazima tulipige vita kwa kiwango kikubwa sana si vizuri na wala si busara hata kidogo kuwaachia wananchi wetu wakaendeleza aina ya uvuvi, ambao unaweza kuleta madhara katika rasilimali yetu ya bahari. Kwa mfano, kuna aina ya mitego ambayo ina matatizo, basi ni vizuri kuachana nayo, sheria yetu tuliyoitunga mwaka jana iko wazi kabisa na inataja aina gani ya mitego ambayo haifai na ipi inafaa.

Kwa hivyo, ni vizuri Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi turejee katika sheria yetu, ambayo tuliyoitunga sisi wenyewe na tuangalie namna gani tunaweza kuwashauri wananchi wetu, ili kuachana na uvuvi huu ambao kwa kweli unaleta maangamizi makubwa kwa rasilimali zetu za baharini. Kwa mfano, wenzetu walipuuzia mambo haya katika nchi zao, basi leo habari zao zimekuwa jangwa na wala hazina kitu hata kidogo.

Sasa sisi ili kuepukana na hilo lazima kwa pamoja Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuwaelimishe wananchi wetu kuona kwamba tunafanya uvuvi ambao unakubalika, usioharibu matumbawe na wala mazalio ya samaki,

ili kuona kwamba rasilimali hii tunaitunza pamoja na kuiendeleza kwa maslahi yetu na uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Spika, nakushukuru na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Gando pamoja na wafanyakazi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, naunga mkono hotuba ya Mhe. Rais. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nami naomba niungane na wenzangu kutoa shukurani na kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwamba leo tupo hapa tunajadili masuala ya nchi yetu kama Wazanzibari, bila ya kujali itikadi zetu Mwenyezi Mungu atusaidie umoja huu uendelee. *(Makofi)*

Mhe. Spika, la pili ni mara yangu ya kwanza kusimama kama waziri na kuzungumza katika Baraza la Wawakilishi. Kwa maana hiyo, naomba nikupongeze kwa kuchaguliwa kuwa Spika kwa mara nyengine katika nyumba mpya nzuri yenye baridi nyingi sana. *(Makofi)*

Kwa kweli nisingependa kuchukua muda maana umeshatuambia tupunguze maelezo, lakini na mimi nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuniamini kusimamia wizara ambayo mara zote inaambiwa kuwa ni ngumu sana kuliko hata ile ya Mhe. Omar Yussuf Mzee ya Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Kwa hivyo, namshukuru kwa kuniamini pamoja na mwenzangu Dr. Sira Ubwa Mamboya kusimamia Wizara ya Afya. Kwa kweli naomba nimshukuru sana Dkt. Sira Ubwa Mamboya Mhe. Naibu Waziri wa Afya, kwa kunitoa ushamba katika Wizara ya Afya na kunisaidia kuielewa kutokana na yeye kuwa mwenyeji wa wizara ile na pia ni Daktari.

Mhe. Spika, mimi na mwenzangu kabla ya kuanza kazi tuliona ni suala zuri sana kutembelea wizara katika kila eneo ambako kuna taasisi za wizara hiyo. Kwa kweli tumetembea Unguja na Pemba, mashamba na mjini na tumejifunza mengi kutokana na wafanyakazi ambao tulikuwa tukiwasikiliza zaidi kuliko kuwahutubia. Kwa kweli wametuambia mengi na tumezungumza hata na wagonjwa ambao tumewakuta hospitali mbali mbali.

Mhe. Spika, kwa taarifa yako simu zetu ni kama *hot line* mpaka saa 7 za usiku wale wanaolalamikia huduma za afya, basi huwa wanatupigia simu na kwa lile tunaloweza kulishughulikia tunalishughulikia. Kwa hivyo, wanashukuru wananchi kwa kushirikiana na sisi kubadili taratibu za sehemu ambazo zililokuwa haziridhishi.

Hotuba za Mhe. Rais ni mbili kuna hii ambayo aliyoitoa hapa Baraza la Wawakilishi na ile aliyoitoa pale Amani wakati wa Sherehe za Mapinduzi za Miaka 47. Sasa hotuba hizi zote nimezisoma na wala siajabu kwa sababu na yeye ni mtu wa afya ameeleza kwa ufasaha sana umuhimu wa sekta hii. Nini ambacho angetutaka wasisimamizi na watekelezaji wa wizara hiyo tungefanya. Mhe. Spika, hotuba hii ukurasa wa 37 mpaka 39 Mhe. Rais ameeleza juu ya kutoa umuhimu wa maadili ya ufanyaji wa kazi za afya. Vile vile amezingatia sana matatizo ambayo yameelezwa na baadhi ya Wajumbe wa Baraza hili, kuhusu maslahi ya wafanyakazi na mazingira mazuri ya kazi ngumu wanazofanya wafanyakazi wa wizara hii. Namshukuru sana Mhe. Rais kwa kutuelekeza hivyo.

Kwa kweli lazima tujipongeze pamoja na matatizo yanayoonekana, lakini Wizara ya Afya imepiga hatua sana. Maana si vibaya Waheshimiwa Wajumbe wako Mhe. Spika kuelewa, kwamba licha ya matatizo tuliyonayo lakini hatuna Mzanzibari yeyote anayetembea zaidi ya kilomita tano bila ya kukuta kituo cha afya.

Hili ni suala la kujipongeza na mafanikio makubwa sana ya miaka 47 ya Mapinduzi, ambapo wakati huo ilikuwepo hospitali moja tu, mtu anapoumwa Makunduchi au Nungwi lazima aje Mnazimmoja na kule Pemba zilikuweko tatu, lakini sekta hii imeimarika.

Sekta hii imeimarika kwani hivi sasa tunavyo vifaa vya kisasa, ambapo zamani tulikuwa tukivisikia hadith tu, lazima tuvifuate Dar-es-Salaam na sasa vingi vinapatikana hapa. Kwa mfano, kuna kifaa kinaitwa *CT Scan*, pia kuna vifaa vyengine hata majina visijui. Vile vile *Pathology Laboratory* yetu inaendelea, pia kuna mashine ambayo zinatizamwa na watu wawili na kuambizana hicho ndicho nini au kitu gani.

Pamoja na hayo, tumekuwa na msaada wa madaktari kutoka Spain huwa wanakuja kila miezi mitatu kwa ajili ya kufanya upasuaji wa matatizo ya mgongo nadhani na kichwa.

Mhe. Spika, hata hivyo bila ya shaka matatizo yapo na Mhe. Rais ametuagiza jinsi ya kuchukua hatua kuyakabili matatizo hayo. Kwa hivyo, ukweli ni kwamba kazi ya afya na kazi nyengine zozote zile kuna kitu kinaitwa lengo mama, afya maana yake ni kutibu kwa yule anayeumwa na kumwambia kumkinga asiumwe (maana yake *prevention and cure*).

Sasa ili mtu asiumwe unamwambia jikinge na wakati anapoumwa unamtibu na wanaofanyakazi ya kumtibu ni madaktari, lakini nyuma ya madaktari na

wauguzi inabidi kuwe na huduma, ili hao walioko kwenye *front line* waweze kufanyakazi zao.

Kwa maana hiyo, tunahitaji madaktari pamoja na wauguzi wa kutosha na juzi tumekwenda kufungua Chuo cha Afya Mbweni, yaani kimeongezwa, ili kiweze kutoa wauguzi pamoja na wafanyakazi wengine wa hospitali waongezeke.

Kwa hivyo, pale kimefunguliwa Chuo Maalum cha Madaktari wanaosomeshwa na Madaktari wa Cuba na hivi sasa tunao wanafunzi kama 38 wanaoendelea na tunao mradi wa *ADB* unaoendelea umetoa sehemu kubwa ya matumizi kwa ajili ya kusomesha watu wetu nje, yaani Tanzania Bara pamoja na nchi za nje. Pamoja na uhaba tunaouona wa madaktari, lakini hatua zimechukuliwa kuhakikisha kwamba upungufu wa wafanyakazi unapungua. Vile vile tunachukua hatua Mhe. Spika kutafuta wataalamu wa kuazima wanaitwa (*Emergence Doctors*), ambao wanaweza kuja kwa muda mfupi kama vile wanavyokuja Madaktari wa Spain.

Mhe. Spika, kiasi wiki moja iliyopita nimekutana na Balozi wa South Korea amekuwa tayari kutusaidia kwa kutuletea madaktari tena kwa gharama zao. Kwa hivyo, Mwenyezi Mungu akitujaalia kila siku zikipita tunategemea huduma zitazidi kuimarika.

Pamoja na uzuri wa madaktari lazima wawe na vifaa na dawa za kutosha, yote hayo tunayashughulikia kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Kwa hivyo, matatizo yale yaliyozungumzwa hapa mengi yao tunayaelewa na tumeyakuta huko tulikokuwa tukitembelea. Kwa mfano, wengine wamesema kwamba vituo vyao havina madaktari, lakini sehemu zile ambazo hazina madaktari tuna kitu tunaita *out reach services*. Kwa hivyo, sehemu zile kuna madaktari huwa tunawapeleka angalau siku mbili kwa wiki.

Mhe. Spika, tunajua kwamba wananchi wanayo matumaini makubwa sana na wizara yetu. Kwa hiyo, sisi tunasema kuweni na matumaini, yaani mimi na mwenzangu pamoja na wafanyakazi wa Wizara ya Afya, ambapo lazima nishukuru kwa sababu nimekuta timu ya wataalamu ambayo ni nzuri sana, inategemea ni kiasi gani tutaweza kuitumia mimi na mwenzangu kwa ajili ya kutusaidia na kuweza kuleta mabadiliko.

Kwa maana hiyo, tunaahidi kuwa wananchi wajenge matumaini na sisi katu hatutowaangusha. Katika kuonesha nia hiyo moja miongoni mwa malalamiko makubwa kwenye Hospitali ya Mnazimmoja kwamba imeelemewa sana na huduma zake zimezidiwa na mahitaji.

Kukabiliana na hali hiyo, tayari tumeshatiliana saini na Serikali ya Netherlands, kwa ajili ya kusaidia katika kuimarisha lile jengo ambalo lilikuwa Kiwanda cha Madawa, ili liweze kutusaidia kupunguza hili zogo la *out patient* liende kule, Wodi ya Watoto pamoja na Sehemu ya *Emergence*, kwa lengo la kuipunguzia mzigo hospitali yetu. Kwa wale wanaokuwepo pale basi wajulikane wanafanyiwa utaratibu mzuri badala ya kuwa wanatibiwa kila siku.

Mhe. Spika, tumeagizwa katika kuisaidia Hospitali ya Mnazimmoja isielemewe tujenge Hospitali za Wilaya. Kwa mfano, tukiangalia *Cottage Hospital* ya Makunduchi, Kivunge, Vitongoji na Micheweni, lakini hakuna *Cottage Hospital* kwa Wilaya ya Kati, Magharibi wala Mjini. Kwa hivyo, lile zogo lote la watu wanaoumwa Wilaya ya Mjini, Magharibi na Kati *Cottage Hospital* yao ni Mnazimmoja.

Sasa ili hili lipungue basi tumeagizwa ikiwezekana tujenge *Cottage Hospital* au *Hospital* ya Mkoa kama zile zinazolingana na Chakechake na Wete angalau mbili katika Wilaya zetu hizi za Unguja, kwa lengo kupunguza zogo la pale Mnazimmoja. Mhe. Rais amesema Mwenyezi Mungu atupe uhai miaka mitano ijayo Hospitali ya Mnazimmoja iwe ni kweli Hospitali ya Rufaa, yaani yale ambayo hayakuwezekana vijijini au kwenye Hospitali za Wilaya ama Mkoa ndipo waje Hospitali ya Mnazimmoja.

Kwa hivyo, mimi na mwenzangu tunayo matumaini kwamba hayo yatawezekana, kwa sababu ushirikiano tunaoupata labda kwa kuwa Mhe. Rais na yeye ni Daktari na kwamba anafahamu matatizo yetu pale tunapomuendea. Kwa kweli tunamshukuru sana kwa kutuelewa na tunaomba mashirikiano kwa wananchi, ili tuendelee kusaidiana katika suala la tiba na kinga ya nchi hii.
Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, naomba kukushukuru na kuzipongeza hotuba hizi na kuziunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, nakushukuru na awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha jioni hii kuwa wazima wa afya na kuweza kuendelea na shughuli zetu hapa ndani ya Baraza.

Naomba nianze kwa kukupongeza wewe Mhe. Spika kwa kuendelea kukishikilia kiti hicho cha Uspika na imani yangu ni kwamba, kwa sababu kule kuzito kote ulitoka ukiwa kidedea, basi hapa mambo yatakuwa mazuri zaidi. *(Makofi)*

Vile vile naomba nichukue nafasi hii japo muda mfupi kwanza kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar kwa udhati wa moyo wangu kabisa kwa kuchaguliwa

kwake kuiongoza nchi yetu kwa miaka mitano. Vile vile nimpongeze Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais pamoja na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa kuteuliwa katika kuliongoza jahazi hili la kuiongoza Serikali ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kabla sijaendelea kuyaelezea yale ambayo nataka kuyaelezea yaliyozungumzwa na wajumbe kuhusiana na hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ambayo aliitoa siku ya Uzinduzi wa Baraza hili la Nane.
Kwa kweli naomba uniruhusu nitoe pongezi maalum kwa Mhe. Rais Mstaafu wa Zanzibar Dkt. Amani Abeid Karume na Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais kwa kutufikisha hapa tulipofika. *(Makofi)*

Pia nitoe pongezi maalum Mhe. Spika kwa Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi la Saba, kwani bila ya wao haya mafanikio ambayo tunayo hapa yasingefanikiwa. Kutokana na uelewa wao pamoja kupevuka kwao kisiasa, basi wameweza kutufikisha hapa. *(Makofi)*

Pamoja na hayo naomba niipongeze Kamati ya Mhe. Ali Mzee Ali ambayo nayo ilifanyakazi kubwa ya kutufikisha hapa, ambapo leo ni mafanikio katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nawaomba wananchi wa Zanzibar watumie fursa hii, ambayo tunaipata ndani ya nchi yetu ya maelewano, mshikamano pamoja na umoja kwa kuweza kushirikiana na serikali yao, ili kuweza kupiga hatua za maendeleo ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Katika hotuba hii ya Mhe. Rais wa Zanzibar amegusia maeneo mengi hasa katika suala la mazingira. Kwa mfano, kuna Wajumbe wawili ambao wamechangia hotuba hii na nitaanza na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, ambaye aliguswa sana na jinsi uharibifu wa mazingira unavyofanywa kwa kiwango kikubwa sana, hasa katika suala zima la uchimbaji mchanga na kwa fikra zake aliona kwamba kuna uzembe wa taasisi husika. Pia Mhe. Assaa Othman Hamad aliguswa kwa upande wake na msumeno wa moto.

Mhe. Spika, naomba nikubaliane nao kwamba hayo ni matatizo ambayo katika Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais baada ya kukabidhiwa wadhifa huu ndio iliyokabidhiwa kushughulikia suala la mazingira, basi tumeona kwamba uharibifu wa mazingira ni tishio kubwa ndani ya visiwa vyetu.

Katika kuthibitisha haya ni ziara ambayo Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais na mimi nikiwa waziri wake, tumefanya katika visiwa hivi viwili kwenye maeneo mbali mbali. Kwa mfano, tukianza kwenye maeneo ambayo

yanachimbwa mchanga na pia kwa upande wa kule Pemba katika maeneo ambayo wananchi wamejiajiri kwenye shughuli za kutengeneza matofali, yaani kuchonga matofali kutokana na mwamba kwaiyo kutokana na hali hiyo tunatakiwa kudhibiti mazingira ya nchi yetu ambayo yakitoweka uhai wetu nao uko hatarini.

Mhe. Spika, naomba niwaeleze Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba serikali kupitia Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais imeandaa mikakati madhubuti ya kukabiliana na uharibifu huo, kwa kuanzia imetakiwa Idara ya Mazingira ambayo ipo chini ya Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kuangalia sheria na kuhakikisha kwamba sheria zinasimamiwa kikamilifu, kama nilivyoeleza wakati najibu maswali yanayohusu mazingira tuna sheria nzuri ya udhibiti wa mazingira, tatizo tulilonalo ni jinsi ya utekelezaji na usimamiaji wa sheria hizi. Kwa hivyo, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais imekusudia kusimamia kikamilifu utekelezaji wa sheria ambazo zitadhibiti uharibifu wa mazingira.

Kuhusu msumeno wa moto ambao Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais aliuita juju wa majuju wa miti kwamba kwa dakika chache au masaa mawili miti mingi sana inaweza kuangamizwa, basi Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais tayari juzi katika ziara yake Nungwi ametoa tamko la kutaka halmashauri za Wilaya na Mikoa na Masheha vile vile watakapoona kwamba kuna uharibu wa mazingira kwa kutumia msumeno wa moto kuikamata misumeno hiyo mara moja.

Mhe. Spika, Afisi yangu hivi sasa inashirikiana na vyombo husika ikiwemo Afisi ya Mwanasheria Mkuu na taasisi nyengine zinazohusiana na mazingira, kuweza kulihalalisha hilo kisheria ili kuipiga marufuku misumeno ya moto ndani ya nchi yetu. Hilo tunalifanya kwa haraka sana kwa sababu tumegundua nchi ya Kenya ambayo hivi karibuni imepiga marufuku misumeno hiyo ya moto sasa wakenya hao wanaingia kwa *speed* sana ndani ya visiwa vyetu, wanavamia maliasili ambayo hairejesheki kwa kuikata ovyo.

Kwa hivyo naomba niwahakikishie wajumbe wako wa Baraza na wananchi kwa ujumla kwamba watupe mashirikiano pale wanapoiona watoe taarifa kwa vyombo vinavyohusika, karibu sheria itahalalisha upigaji marufuku wa misumeno hiyo.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo napenda kulizungumzia ambalo Mhe. Farida Amour Mohammded aliligusia kuhusu kuwaenzi walemavu, ndani ya hotuba hii Mhe. Rais alionyesha jinsi ambavyo serikali inawajali sana watu ambao wanaishi na ulemavu, kwa kuthibitisha hilo tayari tuna watu wenye ulemavu lakini vile vile kuna jumuiya mbali mbali ambazo zinahusika na watu

wenye ulamavu wa aina mbali mbali, nia ya serikali kuona kwamba zinawapa msukumo jumuiya hizo ili kuweza kutekeleza majukumu yao kwa nia ya kutatua shida za watu wenye ulemavu.

Lakini vile vile nia ya serikali kuhakikisha kwamba hakuna mtu yoyote ambae ana ulemavu, lakini vile vile nia ya serikali ni kuhakikisha kwamba hakuna mtu yoyote ambae ana ulemavu atakayebaguliwa au kunyimwa haki yake au fursa ya kuajiriwa kwa sababu tu ya ulemavu. Tunaomba wananchi watupe taarifa kama kuna mlemavu ambae amekoseshwa kuajiriwa kwa sababu tu ya ulemavu wake, tunaomba taarifa hiyo tuletewe katika Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais na sisi tutalishughulikia kwa sababu walemavu ni katika sisi wenyewe na wana haki kama tulivyokuwa nayo sisi na wanastahiki kupata haki zao kwa mujibu wa katiba na sheria ya nchi hii.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo na kwa sababu muda wako ni mchache, naomba kuunga mkono hotuba hii ambayo ni dira ya utendaji wetu wa kazi katika serikali hii nakushukuru sana. Ahsante *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Ardhi Makaazi Maji na Nishati: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii adhimu nami niweze kuichangia hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliyoitoa hivi karibuni katika baraza lako hili tukufu.

Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu Subuhana wataala kwa kutuwezesha sote kuwepo hapa na kuwa kitu kimoja na kufanyakazi ya taifa letu. Pili kama walivyotangulia wenzangu na wewe nikupongeze kwa kurudi tena katika nafasi yako ya Uspika wa Baraza hili tukufu na katika juhudi zako ulizozichukua kuweza kututoa pale duni na kutuleta hapa patukufu, ishaalla Mwenyezi Mungu akulipe kwa haya uliyotutendea.
Mhe. Spika, katika kitabu cha hotuba ya Mhe. Rais ukurasa wa tisa naomba kunukuu. Mhe. Rais amesema.

“Tunaianza awamu hii ya serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar awamu ya saba tukiwa tumebeba dhima ya matumaini makubwa ya Wazanzibari”.
Ni kweli kabisa chini ya serikali hii ya umoja wa kitaifa wananchi wa nchi hii Wazanzibari wanasubiri mafanikio makubwa sana, waswahili wanasema nyota njema huonekana asubuhi, dalili hii tuliyoianza nayo inaonekana kwamba tutafika kule tunakotaka kufika Mwenyezi Mungu ishaalla atufikishe. Kulikuwa kuna usemi unaosema mzigo mzito hupewa mnyamwezi sijui usemi ule umebadilika, inaonekana sasa mizigo mizito hubebeshwa Watumbatu, na mimi nimekubali kuubeba na ishaalla nitaufikisha kule ninakotakiwa, nina dhima ya ardhi, nina dhima ya maji, nina dhima ya makazi na nina dhima ya nishati, zima hizi zote zimebeba matumaini makubwa kwa wananchi nina

hakika kwa misaada na mashirikiano nitakayoendelea kupata hapa na uzoefu mkubwa sana niliokuwa nao na kwa mapenzi yangu ninayopenda kushirikiana na wenzangu pamoja na viongozi wangu nina hakika nitafanikiwa. *(Makofi)*

ARDHI:

Mhe. Spika, ardhi sitaki nizungumze sana kwa sababu matatizo yake ni mengi, mipango yake ni mingi na tumeanza kuchakachua na kuchakachua huku kutatuwezesha kupembua kati ya mchele na chua ikieleza sasa nitapata matatizo katika kufanya kazi hiyo, lakini sina shaka katika idara hii kuna watu wazuri sana na nitashirikiana nao kwa karibu sana ili tuweze kutuliza hali iliyopo hivi sasa. Jana nilichangia kuhusu ardhi leo asubuhi nilikuomba ruhusa niende Chuwini nikatizame matatizo ya ardhi yalivyojitokeza, namshukuru sana Mhe. Waziri wa Habari Utamaduni Utalii na Michezo kwa vyombo vyake vilivyonifanyia kazi nzuri sana jana ya kwenda kwa haraka kwenye matatizo niliyoyasema jana lakini watu wakaniletea vinoti vya kunichokoza kistaarabu wakanambia Mheshimiwa haya maeneo ya usiku sio yako, haya huwezi kuyadhibiti ni kweli, maana huku nasema jana usiku watu walipima ardhi wakagawana wakauziana na bahati mbaya sana ardhi yenyewe imetengwa na serikali siku zijazo au wakati wowote tujenge Ikulu ya Rais Wetu.

Sasa imeshauzwa na watu wameshagawana pesa hayo ndio matatizo ambayo yamenikabili na nina hakika kwa msaada wenu na msaada wa Mwenyezi Mungu nitayatatua.

Mhe. Spika, maji ni uhai sasa hivi nimepata kijinoti hapa cha watu wawili wanazungumza kwenye majimbo yao hakuna maji, hakuna hata jimbo moja nchi hii lililokamilika kupata maji ya kutosha safi na salama hakuna, lakini tukubali kwamba awamu ya sita imefanya kazi nzuri sana ya kueneza maji mijini na vijijini, miradi ya Japani na wengine wametusaidia sana angalau kuwa na vianzio vizuri vya kugawana maji hivi tutavitunza na kuviendeleza, katika hatua mojawapo tuliyofanikiwa nayo ni kupata msaada wa kusambaza maji vijijini kupitia shirika la *UN* au *UNDP* na shirika la *ADB* tutapata fedha za msaada na mkopo kusambaza maji Unguja na Pemba vijijini.

MAJI NI UHAI:

Mradi huu utaanza mapema sana mwezi wa March, 2011 na unatarajiwa kumalizika mapema sana mwaka ujao, nasema tukifanikiwa kwa sababu haya mengine tumejitahidi lakini hatukufanikiwa kwa asilimia mia moja tunapambana nayo, lakini huu tukifanikiwa angalau yale madai ya vijijini yatapungua kwa kiwango kikubwa. Mwenyezi Mungu atufanikishe na juhudi hizo ili tuweze kufanikisha usambazaji wa maji mjini na vijijini.

MAKAAZI:

Mhe. Spika hivi jana nimepata bahati ya kuzungunza na muwakilishi kutoka nchini Trinidad huyu amekuja na miradi mitatu, Makaazi, *energy* na *investment* nyengine za kawaida, nimempa kila msaada na kila kipaumbele bahati nzuri ameshatoa dalilili za kutuondoshea tatizo za kupata nafasi za masomo ya vijana wetu kumi tuliowachagua kwenda kusomea shughuli za mafuta, mjumbe huyu ameshachukua *passport* anakwenda kutengeneza viza, pesa zipo tayari mapema sana vijana wetu kumi waliokwama watakwenda kusoma.

Lakini pia Waziri wa Nishati kutoka Trinidad atakuja karibuni Zanzibar kututembelea na kupanga mikakati ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta (*Makofi).* Adhma hiyo iliyoanzishwa na wenzangu ya kutafuta mafuta bado nitaisimamia kwa nguvu zangu zote, tunaambiwa mafuta yapo *survey* imefanywa na imeonekana kuna maeneo kiasi sita mpaka saba ya mafuta, hatuna uhakika mafuta tuliyonayo ni *commercial buyable* tunaweza kuchimba na yakatulipa, maana kuwa ni mafuta ni kitu kimoja na kuwa na mafuta mengi ya kututosha ni kitu cha pili utafiti tutauendeleza na mimi nilikuwa sijui kwamba Trinidad kuna mafuta mengi sana na jamaa hawa wanaonekana wako tayari kutusaidia bahati nzuri kuna Mzanzibari kule ameolewa na Mtrinidad huyu sasa tutamtumia wakala wetu mzuri sana na ni muwekezaji atakayekuja kutusaidia kutafuta mafuta yetu.

Huyu atafanya utafiti wa aina mbili kubwa *energy* mbadala na *energy* hii ya mafuta ya petrol, diesel, kerosene pamoja na gesi asilia tutazungumza na wenzetu mpaka tutawafikiana hakuna lisilo zungumzika na hakuna lisilo fahamika bado tutaendelea kusema kwamba mafuta yabakie Zanzibar *(Makofi).* Tutaendelea kushauriana na wenzetu katika mikakati yetu ya kulitaka suala hili liwe letu, sasa hivi tutafanya hivyo kwa nguvu za pamoja chini ya serikali ya umoja wa kitaifa *(Makofi).*

Mhe. Spika, tutajenga hoja na hatugombani na wala hatutogombana lakini tutajenga hoja mpaka ifahamike na ishaalla ifafahamika, waliochangia katika hotuba hii ya Rais na kuwa na wasi wasi labsa suala la mafuta tumeliwacha hapana hatukuliacha hii ni haki yetu na kama tunataka kuendeleza uchumi wetu katika nchi hii, pamoja na hotuba nzuri sana aliyoizungumza ndugu yangu Omar Yussuf, amezungumza kitakwimu maana ndio *professional* yake amazungumza kitaalam. Lakini pamoja na hayo yote aliyoyazungumza ya uhakika mafuta ni namba moja, tukichimba mafuta tutakuwa tuna nguvu za kiuchumi na nguvu za ustawi wa jamii, tukipata nguvu hizo mbili tutajenga nchi yetu kwa salama na amani.

Mhe. Spika, kwa kuwa umenipa nafasi hii nakaribia kusema kwa upendeleo naomba nisichukue muda wako mrefu, nakushukuru na naiunga mkono hotuba hii ya Mhe. Rais ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru jioni hii kunipa nafasi ya kuwa miongoni mwa wachangiaji wa hotuba hii adhimu ambayo mimi naita dira ya ufanyaji kazi kwa moyo wa uzalengo, ufanisi mkubwa na udugu mkubwa ambao hatimae utaleta tija kubwa kwa Wazanzibari na nchi nzima. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwanza na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyeumba tukijuacho na tusichokijua kwa uwezo wake mkubwa kwa kuifanya Zanzibar kuwa hivi ilivyo sasa, kila kitu kina wakati wake tulijaribu sana kwa mbinu mbali mbali na muda mrefu Zanzibar kuwa hapa ilipo lakini ilishindikana. Kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu wakati ulipofika Zanzibar sasa ni moja, Wazanzibari ni wamoja baba mmoja mama mmoja katika nyumba moja, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuteuliwa kuwa Waziri wa Miundombinu baada ya wananchi wa jimbo la Ole kwa ridhaa yao kunichagua kuwa mwakilishi wao kwa mara ya pili. Sina maneno ya kutosha ya kuwashukuru wananchi wa Ole kwa heshima hii kubwa ambayo wamenipa lakini ishaalla maneno yangu hayatokuwa yakitoka mdomoni lakini yatakuwa kwa vitendo, kwa yale ambayo wao watayaridhia.

Mhe. Spika, nikupongeze wewe ten asana kwa kuwa tena Spika wa baraza hili, nilikuwa nafikiria kungetokea miujiza kuhusu spika sijui nyumba ile ambayo kila nikipita mimi huelekea kushoto angaihamia nani, unastahiki kwa namna ambavyo umekuwa ukifanya kazi huko nyuma. Kwa hivyo nasema sio upendeleo ni haki yako, lakini kuliko yote Baraza lako la Saba lilifanya kazi kubwa sana wewe ukiwa kiongozi wao mchakato uliotufikisha hapa walishiriki wao kikamilifu na chanzo ilikuwa ni wao, lakini kuna kitu kimoja tu naomba nikukumbushe kwamba wajumbe wa baraza lililopita kulikuwa na ahadi kwamba kuna jiwe moja la maru maru jiwe hilo litaandikwa majina ya wajumbe wote na litapachikwa mbele ya baraza hili kwa kumbu kumbu za wanaokuja hapo baadae kwa hivyo nakumbusha.

Mhe. Spika, niwapongeze san asana wajumbe wenzangu waliochaguliwa na walioteuliwa lakini wakumbuke kwamba hichi ambacho tumefanyiwa na wananchi na Rais wa Zanzibar ni changamoto na inahitaji mikakati ya uhakika, Wazanzibari wana matumaini makubwa ya awamu ya saba wanataka kuona kuna tofauti gani ya awamu ya sita na za nyuma na hii awamu ya saba, kwa hivyo changamoto yetu tujue kwamba katika awamu hii ili wananchi wetu tusiwaangushe, tusiwakatishe tama na haya maamuzi mazito waliyofanya basi ni vyema tujue kwamba baada ya hotuba ya Mhe. Rais ambayo tunaijadili sasa

hivi na tunaichangia si mke si mume, si waziri si bekibencha si wewe mwenyewe hakuna kulala mpaka kieleweke. Kueleweka ni kutimiza matumaini ya Wazanzibari hakuna namna nyengine.

Mhe. Spika, sasa na mimi niende moja kwa moja mimi na Naibu Waziri wangu tumejaribu kusikiliza kwa makini hata nilipokuwa sipo yeye alikuwepo na wakati alipokuwa yeye hatupo mimi nilikuwepo, kwa hivyo hakuna wasi wasi kwamba kuna mwengine yoyote ambae sisi hatukumsikia. Mhe. Spika, waliochangia hotuba hii katika miundo mbinu ni.

Mhe. Salim Abdalla Hamad	-	Mtambwe
Mhe. Abdalla Juma Abdalla	-	Chonga
Mhe. Salehe Nassor Juma	-	Wawi
Mhe. Salmin Awadh Salmin	-	Magomeni
Mhe. Rashid Seif Suleiman	-	Ziwani
Mhe. Abdi Mosi Kombo	-	Matemwe
Mhe. Asha Bakari Makame	-	Vitimaalum Makamo M/kiti W/wake CCM
Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Kwamtipura
Mhe. Ashura Sharif Ali	-	Viti maalum CUF

Kama kuna wengine sikuwaandika ni kwa sbabu nimesahau kama binaadam sijakusudia kwamba nisiwaandike.

Mhe. Spika, sitaki kuchukua muta wako mrefu lakini kwa ujumla mambo ambayo yameelezwa ni wasi wasi, maomba, ushauri na kukumbushwa maneno ya Mhe. Rais wa Zanzibar katika hotuba yake ambayo tunaijadili kuhusu Wizara ya Miundombinu, maneno hayo yote yako katika ukurasa wa 30 mpaka ukurasa wa 33. Hii ni hotuba ya Mhe.Rais aliyoeleza humu ni machache sana kwa sababu angeeleza yote kuhusu miundo mbinu basi hiki kitabu chote kisingetosha, lakini waheshimiwa wawakilishi wenzangu wao wamekwenda mbali zaidi ya haya ambayo yamo kwenye hotuba hii.

Mhe. Spika, kuhusu barabara kwa ujumla Mhe. Rais ameeleza hapa jukumu la kwanza ni kuhakikisha kwamba barabara zote kuu zilizobakia asilimia 30 maana yake ni kwamba tayari asilimi 70 ya barabara kuu Unguja na Pemba tayari zimejengwa, kwa hivyo asilimia thalathini za barabara kuu zilizobakia zinakamilishwa katika kipindi kifupi kijacho. Napenda kulihakikishia Barara hili mbele yako wewe mwenyewe kwamba katika kipindi kifupi hapo hakijatajwa lakini ahadi hii na maelekezo haya ya Mhe. Rais yatakuwa yametimizwa.

Kama nilivyosema juzi kwamba *Ishallah* katika sherehe za Mapinduzi zinazokuja kutimia miaka 48 Wizara hii ya Miundombinu itaongoza kwa ufunguzi wa barabara na utiaji wa jiwe la msingi na *terminal* mpya jengo jipya

la abiria linalojengwa kwa mkopo nafuu kutoka Jamhuri ya Watu wa China. Pia nina hakika sheria hizo zitashuhudia utiaji wa jiwe la msingi wa Bandari kubwa, bandari mbadala inayotegemewa kujengwa katika eneo la Maruhubi kwa maarufu Mpigaduri.

Sina wasi wasi kwamba sherehe hizo hizo kwamba mtashuhudiwa kuwekwa kwa jiwe la msingi kwa bandari nyengine ya Mkumbuu kisiwani Pemba. Nasema haya kwa sababu tayari mchakato umeanza na kwa maelekezo ya Mhe. Rais kwamba sasa tunaweza kwenda kwenye *systerm* inaitwa *BOT*. (*BOT*) *Build Operate Transfer* wafadhili au wawekezaji baada ya mikataba iliyomadhubuti baina ya wawekezaji hao na serikali watajenga, wataendesha na hatimae watarejesha bandari au chochote ambacho tulichokubaliana kwa serikali. Lakini wakati wanaendesha na serikali nayo itakuwa inapata mapato.

Lakini vile vile uajiri utakuwa mkubwa sana katika nchi hii kuliko hao wageni. *Systerm* hiyo ya *BOT* na nyengine inaitwa (*PPP*) *Public Privet Perfect* huu ni mshikamano, nimashirikiana kati ya serikali na wawekezaji binafsi. Wengi wamejitokeza wao wenyewe wamependekeza hivyo wakati na sisi vile vile tulikuwa tunataka iwe hivyo. Kwa sababu si jambo la kubahatisha ni kweli kwamba serikali yetu kutokana na uchumi wetu hatuna uwezo wa kujenga bandari ya Mpigaduri wala ya Mkumbuu. Kwa makisio tu hivi hivi kabla ya kuzidi sana au kabla ya dizain hakuna hata bandari moja itakayopungua gharama ya dola milioni 400, sasa hizo ni gharama kubwa.

Mhe. Spika, suala la maneno na ahadi na maelekezo ya hotuba hii adhimu ambayo mimi naiita ni dira maalum. Dira iliyomaliza kila kitu. Tukiweza kuifanyia kazi hii Mawaziri na watendaji wote wa serikali, humu ilani zote zimechanganywa, ilani ya CCM imejaa tele imehamia na yale mengine yote kutoka ilani nyengine yaliyomazuri naona humu yamo. Kwa hivyo hata mkisikia kuna ilani ya Chadema humu msishangae. Mhe. Rais alitafuta kila zuri akaliweka humu yakiongozwa na ilani ya CCM. Ndivyo ilivyo, chama ambacho kimetoa Rais ilani yake au sera zake ndizo ambazo zinatelezwa katika utendaji wa serikali.

Mhe. Spika, nije kwenye barabara za vijijini. Mhe. Rashid Seif alimnukuu Mhe. Rais kwamba jukumu la pili ni kuhakikisha kwamba tunazijenga kwa kiwango cha kupitika mwaka mzima barabara zote ndogo ndogo za Mjini na Mashamba. Kazi hii itafanyika kwa wakati mmoja Unguja na Pemba. Mhe. Rais alipokuwa anazungumza haya alikuwa haoti. Hivi mimi nazungumza kuna barabara sita Pemba ambazo zote hizo sita mhandisi, mkandarasi, *contractor* barabara hiyo ni Wete/Konde, Wete/Gando, Mtambile/Muwambe, Mtambile/Kangani, Mzingani/Wambaa na barabara ya Kenya/Chambani.

Lakini wakati huo huo hata Unguja kuna barabara ya Amani/Dunga, Mfenesini/Bumbwini. Wakati naongea hapa *contractor* hupo juu ya barabara nane (8) Unguja na Pemba kwa hivyo Mhe. Rais hapa alikuwa anazungumza kitu ambacho yeye mwenyewe ana hakika nacho. Hakukusudia barabara zote hata kama 20 zitajengwa siku moja na siku ya pili au baada ya muda fulani zote zitajengwa. Hapana hakukusudia hivyo. Naomba Mhe. Rashid akumbuke kwamba masuala haya sio kama ni ya kubuni bali ni ya uhakika.

Mhe. Spika, barabara nyengine za vijijini zimetajwa hapa za Matemwe na hata barabara ya Mhe. Hamza inayotoka kwa Abasi Hussein mpaka imekwenda kwenye Afisi ya Wilaya inatoka Saateni, inakwenda zake Mboriborini inaungana na na barabara inayotoka Amani au barabara ya Mkapa road. Si hiyo tu, utaratibu wetu na mpango wetu ambao tumeu *revise* kutokana na *National Transport Master Plan*. Barabara zote ziwe za vichochoroni au za vijijini ambazo zimo katika *National transport master plan* barabara hizo tunazijenga kwa kiwango ambacho *master plan* imependekeza. Kuna nyengine ni za lami, nyengine za kifusi na nyengine za kila wakati kwamba greda linapita na kuweka sawa.

Mhe. Spika, kwa ufupi ni kwamba mara nyingi baada ya mvua kubwa za masika, kutokana na mmong'onyoko wa ardhi basi njia ambayo ilikuwa inapitika kabla ya masika baada ya masika njia hiyo inakuwa haipitiki. Dawa yake barabara kama hizo kwa nusra baada ya mvua tunapitisha greda tunaweka sawa, gari zinapita na baada ya muda kila tunapopata nafasi tunazitia kifusi na baadaye hatimaye tunazitia lami.

Mhe. Spika, kama nilivyokwambia suala la Miundombinu hata mkinipa siku tatu simalizi. Lakini jengine ni suala la wasafiri wa wananchi wa Zanzibar wanaosafiri Unguja na Pemba kuhusu usafiri wa baharini. Lakini hata hawa wanaosafiri kwa ndege Constal, Zan air, Tropical na nyenginezo. Ni kweli tumegundua kwamba kwa malalamiko yaliyopo kuna haja ya kukutana na wanaomiliki vyombo hivi viwe vya baharini au vya angani.

Mhe. Spika, kwa taarifa yako na kwa taarifa ya wajumbe wako ni kwamba mara ya kikao hichi cha Baraza mkutano huu wa baraza kumalizika basi tumepanga kwanza tukutane na wadau wa viwanja vya ndege wakiwemo hawa wanaomiliki hizi ndege, wawe wa ndani au wa nje. Kikao hicho madhumuni yake kujadili, kuona kuna matatizo gani, kunachangamoto zipi na kwa pamoja tupendekeze mkakati wa pamoja ili kuhakikisha kwamba kila mtu habebeshwi mzigo ambao si wake. Yule ambaye ana mzito wake unatakiwa na watu wengine basi mzigo huo autuwe.

Hivyo hivyo na kwa vyombo vya baharini na wao tutawaita, tutaelekezana, tutaelezana. Nina hakika kwa siku kama hizi serikali na hawa wenye vyombo ni hakika ufumbuzi utapatikana kama ambavyo huko nyuma tumekuwa tumekipata ufumbuzi wa mambo chungumzima.

Mhe. Spika, kuhusu barabara, kuhusu bandari, kuhusu viwanja vya ndege, hayo ndiyo maeneo makubwa ambayo Waheshimiwa wameeleza. Naahidi mbele ya Baraza lako tukufu kwamba Wizara yangu nikishirikiana na Kamanda Gavu na timu ambayo tumeikuta wizarani.

Mhe. Spika, tutajitahidi kuhakikisha kwamba hotuba ya Mhe. Rais tunaikamilisha hata kabla ya kipindi chake kumalizika cha miaka mitano. Ili kama atachaguliwa tena 2015 au zaidi basi yeye awe anahimiza suala kwamba barabara fulani inashimo lakini sio kwamba barabara fulani haijajengwa. Kuhakikisha kwamba tunapata wahisani, tunatafuta wawekezaji ambao watakuwa na manufaa kwetu sisi na kwao wao. Si kila muwekezaji tu, tupo *very careful* na tunashirikiana sana na wenzetu hasa Wizara ya Fedha. Hatufanyi maamuzi yoyote ambayo yana *involve* mambo ya *fund* na *financial* na ni yote bila ya kushirikiana na Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na kwa wale ambao sikuwataja moja kwa moja. Mheshimiwa wa Matemwe asiwe na wasi wasi nimeshamjibu kabla ya hapa tukimaliza kikao hiki tunakwenda zetu Matemwe tena atakaa mbele kwenye gari yangu ili aonekane kwamba kweli anatekelezewa ahadi zake.
Na wale waheshimiwa wote na popote nitakapofanya ziara nitawajulisha mapema ili wananchi wao wawaone kwamba kweli mwakilishi wetu anafanya kazi tuliyomtuma. Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na nakupongeza kwa kipindi chako cha nne mfululizo kuchaguliwa rasmi tena kwa kura nyingi kuwa Spika, wa Baraza hili .

Jengine naomba niwashukuru wananchi wote wa Zanzibar waliomchagua Alhaji Dr. Ali Moh'd Sheni kuwa Rais wa Zanzibar. Na yeye akapata nafasi akaniteuwa mimi kuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na akanikabidhi Wizara hii ya Ustawi wa Jami, Maendeleo ya Vijana Wanawake na watoto.
Mhe. Spika, kwanza kabla sijamaliza dakika zangu naomba niunge mkono hotuba hii ya Mhe. Rais mia kwa mia. Nikianza kulikuwa kuna mchango unaosema lazima tunatakiwa tuwaenzi wazee. Ninalotaka kumwambia Mheshimiwa Mjumbe aliyetoa wazo hili kwa kweli yupo juu ya mstari.

Tutawaenzi wazee na tutaweka sera maalum kwa ajili ya wazee, ili mambo yao yaweze kwenda kwa uhakika na vizuri zaidi.

Jengine pia nilipata hoja ya kuwa ni lazima tuwawezeshe wanawake kupitia katika vikundi vyao vya ushirika. Mimi natoa kauli ya kusema kwamba mimi nipo tayari kushirikiana na wanawake pamoja na wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kupitia katika vikundi vyetu vya ushirika. Wao wawawezeshe wanawake na mimi nitoe mchango wangu. Tutakuwa pamoja kwa hali na mali katika kuwaendeleza na kuwafunza wanawake kiuchumi na kimaendeleo.

Jengine kuhusu vijana. Vijana tumetakiwa kwenye hotuba hii tuunde sera ya vijana, tuanzishe baraza la vijana ili vijana wajisikie na wajione kwamba serikali yao ipo pamoja na wao. Kwa sababu nguvu zote katika nchi yeyote ile inatagemea vijana wake. Pamoja na kwamba hatuna ajira ya kumpa kila kijana lakini tunao uwezo wa kuwashirikisha vijana katika kujitafutia ajira zao wenyewe kwa kujituma na kujiendeleza. Sisi tutalisimamia jambo hili ipasavyo.

Mhe. Spika, pia katika hotuba hii ya Mhe. Rais amegusia sana kuhusu Benki ya Wanawake. Tumeshachukua hatua mbali mbali Wizara hii ya wanawake na watoto kwa kuzungumza na wenzetu wa Tanzania Bara ambao wameshaanzisha hii Benki ya Wanawake ili na sisi huku Zanzibar tuweze kupata *branch* ya benki hiyo. Tutawaendeleza wanawake na sasa tunasema wanawake basi tena kuchukua fedha kutia kwenye vikabati wakatokea wezi wakawanyang'anya, tunaweka katika benki yetu. Nategemea kwamba riba haitokuwa kubwa, changamoto kubwa ninaitoa kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hasa wanawake, tujitayarishe tutakapoanzisha tu benki yetu wao ndio wawe watu wa mwanzo kuifungua au kuweka fedha zao katika benki ya wanawake.

Mhe. Spika, kwa hayo machache kwa sababu nimeomba dakika tatu naomba niseme tena naunga mkono hotuba hii mia juu ya mia. Haina dosari wala siwezi kuijadili sana nikaja nikapotea. Nashukuru sana kwa kunikumbuka na kunipa nafasi. Asanteni sana.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, sina budi kutoa shukurani kwako kwa kuweza kunipa fursa hii. Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeumba mbingu na ardhi kwa kutuwezesha au kuniwezesha kuwa miongoni mwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na vile vile kuwa Waziri wa Habari.

Vile vile sina budi kumshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuweza kuniteuwa kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii

na Michezo. Pia sina budi kuwashukuru wananchi wangu wa jimbo la Magogoni kwa kuliona hilo na kuniona kwamba ninafaa na Mwenyezi Mungu atanipa wepesi.

Nikirudi kwenye hotuba ya Mhe. Rais ambayo ameitoa ndani ya chombo hichi cha Baraza la Wawakilishi ambayo kwa kweli ina uzito mkubwa naiyunga mkono mia kwa mia. Baada ya kuunga mkono nina hoja kwa nini nikaunga mkono. Kwenye hotuba yake kaeleza mambo mengi lakini yote yamenigusa na kilichonigusa zaidi ni lile suala la kusema kwamba sote tumebeba dhima kwa hivyo ni wajibu tuwatendee haki wananchi.

Waheshimiwa wajumbe na Mhe. Spika, *good well* ambayo imeonyeshwa katika Baraza la awamu ya sita kwa kweli ilikuwa ni kilio cha Wazanzibari kwa miaka mingi na *Alhamdulillah* tumefika mahali pake. Mara hii awamu ya saba nina imani kwamba *good well* hii itaendelezwa.

Nimesema *good well* hii ndio asasi ya yote, haya yote yaliyoelezwa humu yatakuwa hayana maana kama tutakuwa hatujatekeleza asasi hii, yaani maridhiyano, kupendana na kuweka Uzanzibari mbele. Pamoja na yote hayo nawapongeza vile vile baadhi ya Waheshimiwa wajumbe ambao wamejaribu kutoa baadhi ya maoni na fikra na kasoro ambazo zimegusa wizara yangu ni wajibu wao. Binadamu kama baskeli, baskeli kila wakati inatakiwa uwe unaisukuma pedeli ukiiwachia inakuwa matatizo.

Kabla ya hayo kwanza naomba nimpongeze Mhe. Rais kwa kuona umuhimu wa chombo cha habari na kukiunganisha na sekta ya utalii. Kiuwoni utaona kama ni vitu ambavyo haviowani lakini umuhimu wa chombo cha habari ni mkubwa katika jamii. Vyombo vya habari ndio kiyoo cha jamii na suala la utalii ni suala la jamii. Bila ya kuelimisha jamii huu utalii baada ya kuwa ni wenye faida basi unaweza ukaleta maangamizi baadaye. Vyombo hivi hususan TV, radio na magazeti, vina wajibu wa kutoa taaluma kubwa kwa wananchi na zaidi vijijini kwa sababu huko ndio kwenye utalii zaidi, kwa hapa ni mahali pake.

Katika suala jengine ambalo wameliona lina tija ni umuhimu wa kuwa na kiwanja chengine cha michezo. Nakubali kwamba kiwanja tulichonacho kwa kweli hakikidhi, kimeshakuwa kidogo na wizara imeliona hilo na kumshauri Mhe. Rais na Mhe. Rais ameshaliona umuhimu wake na ametukabidhi kwamba tutafute maeneo mengine ili kuweza kujenga kiwanja cha kisasa kabisa na ambacho kitakidhi mambo yote ya kimichezo. Hilo limejitokeza dhahiri hivi juzi tu baada ya kumaliza mechi ya fainali ya Simba na Yanga katika Mapinduzi Cup kwa kweli kiwanja kilifurika ikawa wale wapenzi tukawa hatujui wapi pa kuwaweka, hatimae ikabidi tuwaweke kwenye tatan. Ule ni

ujumbe kwamba hichi kiwanja kimeshakuwa hakidhi tena kwa hivyo kuna haja yakutafuta kiwanje chengine. Hivi sasa tumeshawasiliana na wizara husuka ya ardhi kuhisiana na kutafuta maeneo ili kufanya maarifa ya kujenga kiwanja chengine cha kisasa kabisa na kikubwa zaidi.

Eneo jengine wajumbe waliliona ni suala la ajira. Wizara ina nia ya kuboresha chuo kile ili kuweza kuzalisha wahitimu wazuri. Waheshimiwa Wajumbe muelewe kwamba kile chuo sio kwa sababu ya kujenga ajira ya mahoteli tu. Kile chuo vile vile kinaweza kikawaelimisha watu kikawafanya kuwa wabunifu hata kuwa wajasiri amali wa kuweza kujitegemea wenyewe wa kuunda vitu vya ajabu ajabu ambavyo kwa watalii vinakuwa ni vivutio vikubwa tu. Ahsante sana

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena nakushukuru kwa kunipa wasaa huu kuja kufanya majumuisho ya michango mbali mbali ya Waheshimiwa Wajumbe walioitoa katika kuchangia hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati akizundua Baraza la Nane la Wawakilishi hapo November 11 mwaka 2010.

Mhe. Spika, niungane na wenzangu kukushukuru wewe kwa dhati kabisa kwa kuteuliwa kwako kuwa Spika wetu kwa mara nyengine tena na mimi nikinyamaza haitokuwa vyema. Vile vile naomba niwashukuru kwa dhati kabisa waheshimiwa wote waliorejea tena katika Baraza hili na niwapongeze na wale wapya niwakaribishe ingawa si wapya lakini niseme karibuni.

Kubwa zaidi sote hatuna budi tupongezane kwa kazi nzuri sana tuliyoifanya ya kutimiza matakwa ya Katiba ya kufanya uchaguzi wa vyama vingi katika hali ya umoja, Uhuru, amani na utulivu. Hilo ni kubwa sana na ndio lililotuwezesha kuja hapa Barazani leo kukutana hapa.

Mhe. Spika, hotuba ya Mhe. Rais kwa kweli ilijaa falsafa, busara na yamezungumzwa mengi sana. Waheshimiwa Wajumbe kama walivyosema imeandikika, kila sentensi ukiifanyia analysis sijui utaikosea wapi. Mimi nawapongeza sana Waheshimiwa kwa michango yao. Naamini Mhe. Spika, ungetupa fursa zaidi tungeweka *record* . Naamini hata hivyo hii nambari tumeiweka *record* sijui huko nyuma, kwa ujumla tumepata wachangiaji arubaini (40), 39 wamechangi hapa ukumbini na mmoja kachangia kimaandishi. Kwa ujumla wote tunawashukuru na zaidi maswali waliyouliza, fikra za kuendeleza zaidi.

Mheshimiwa mwenzangu mmoja alisema maarifa ya kufanyia kazi, changamoto, wamezitoa na naamini yatatusaidia katika hii dira ambayo Mhe.

Rais ametupa. Baada ya hotuba ile kama alivyoahidi Mhe. Rais alikutana na Wizara moja moja takriban hii dira aliyoisema humu akaipa hiyo wizara moja moja. Wizara iliongozwa na Waziri mwenyewe, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Manaibu Makatibu Wakuu na watendaji wote. Kwa hivyo hii dozi Mhe. Rais, aliyotupa hapa nasema kwa watendaji wote. Kwa hivyo, hii dozi Mhe. Rais aliyotupa hapa nasema kwa watendaji wetu imeshafika. Nini wanapaswa wafanye wanajua.

Mhe. Spika, naomba kwa haraka haraka niwatambue wale waliochangia. Kwanza kabisa ni:

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2 Waziri Asiye na Wizara Maalum, (Machano Othman Said)
3. Mhe. Saleh Nassor Juma
4. Mhe. Ali Salim Haji
5. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
6. Mhe. Fatma Mbarouk Said
7. Mhe. Assaa Othman Hamad
8. Mhe. Omar Ali Shehe
9. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
10. Mhe. Mohammed Haji Khalid
11. Mhe. Hija Hassan Hija
12. Mhe. Hassan Hamad Omar
13. Mhe. Salim Abdalla Hamad
14. Mhe. Salma Mussa Bilal
15. Mhe. Rashid Seif Suleiman
16. Mhe. Salmin Awadh Salmin
17. Mhe. Ussi Jecha Simai
18. Mhe. Abdi Mossi Kombo
19. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
20. Mhe. Asha Bakar Makame
21. Mhe. Hamza Hassan Juma
22. Mhe. Ashura Sharif Ali
23. Mhe. Rufai Said Rufai
24. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa
25. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman
26 Mhe. Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili
27. Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.
28. Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais
29. Mhe. Waziri Nchi (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo
30. Mhe. Waziri wa Bishara, Viwanda na Masoko.
31. Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria.
32. Mhe. Elimu na Mafunzo ya Amali
33. Mhe. Mifugo na Uvuvi

34. Mhe. Afya
35. Mhe. Waziri Nchi Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais
36. Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.
37. Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu.
38. Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.
39. Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mheshimiwa mmoja aliyechangia kwa maandishi ni:
40. Mhe. Shawana Bukheti Hassan.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wote hawa tunawashukuru sana kwa michango yao. Vile vile natoa pongezi maalum kwa Waheshimiwa Mawaziri, kwa kweli kazi yote wameshafanya wao. Kwa sababu pale walipokuwa wanachangia yale mambo muhimu yaliyozungumzwa na waheshimiwa nilikuwa nayatia *tick* moja baada ya jengine. Lakini kuna mambo yalizungumzwa na waheshimiwa wengi sana na kuna mambo yalizungumzwa *very specific* na baadhi ya waheshimiwa. Sasa naomba yale yaliyozungumzwa na waheshimiwa wengi na takriban waheshimiwa mawaziri wametolea ufafanuzi naomba niyataje tu, na mimi niya- *acknowledge* kwamba kweli haya mambo ni muhimu na serikali tumeona umuhimu wake.

Kwanza ni suala zima la mazingira. Suala hili limezungumzwa kwa mapana yake, uchimbaji wa michanga. Namshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais sitaki tena kurejea majubu.

Lakini suala muhimu ambalo nataka kulisema ni suala la ushirikishwaji wa wizara mama, Wizara ya Kilimo na Maliasili. Huko tunakotoka Wizara ya Maliasili ndio ilikuwa dhamana wa yale mambo, wao wana-*identify* maeneo, panachimbwa mchanga wanasimamia, wanatoa vibali. Siku hizi mambo kidogo mambo yamebadilika, ile dhamana imewapungukia baadhi ya sehemu Halmashauri za Wilaya ndio zinatoa vibali, wanachimba wao, wanakusanya pesa, sasa wizara hata haijui pengine mabonde gani yanachimbwa. Kwa hivyo, kidogo kumekuwa na kutokufahamiana.

Sasa serikali tutajitahidi sana kuona kwamba wizara yenyewe wanalisimamia hili hao wenye Halmashauri za Wilaya watafanya kazinao tutashirikiana pamoja tuone kwamba hakuna migongano. Suala zima hii migongano mpaka ardhi zinachoka, tunaweka mmong'onyoko ambao *replacement* yake ni ndogo kidogo.
Mhe. Spika, suala la Mwambe la rafiki yangu Mhe. Hija Hassan Hija tumelisikia tutalifanyia kazi ipasavyo.

Suala la uvuvi takriban Waheshimiwa wengi sana wamelizungumza na tumeona kweli ni rasilimali muhimu sana katika kutanua uchumi wa nchi yetu. Sitaki kueleza zaidi mwenyewe Mhe. Waziri amefafanua vizuri kabisa na mipango yake ya maendeleo.

Lakini suala la kilimo nalo takriban waheshimiwa wote tena wamezungumza kwa hamasa kabisa na wameonesha vipi kilimo chetu kinapaswa kiendelee mbele zaidi. Namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kutoa ufafanuzi na kwa kweli tumeona kunahitajika *input* za kisasa kukiendeleza kilimo chetu. Lazima tupate matrekta, rotoveta, mbegu bora, elimu ya wakulima, haya yote ukiyajumlisha ndio tutazalisha zaidi. Kwa hivyo, yote tumeyasikia na tutajitahidi serikali kwa uwezo wetu tuone haya mambo tunayafanikisha.

Ukuzaji wa ajira, suala hili nalo waheshimiwa wengi wamelizungumza nalo sitaki kulisisitiza zaidi. Lakini suala la utalii Mhe. Waziri amemalizia mwenyewe hapa nalo tunashukuru watu wameshauri sana kwamba utalii uwanufaishe Wazanzibari zaidi kuliko wageni. Tunashukuru hali sasa hivi nzuri, utalii umewekezwa sana lakini unawanufanisha nani? Sasa maoni yenu waheshimiwa tumeyasikia tutayafanyia kazi.

Suala la afya nalo waheshimiwa mmelizungumza sana, mnakwera sana na baadhi ya utendaji ulivyo lakini na mapungufu yaliyoko kwenye Sekta ya Afya. Waziri mwenyewe tunamshukuru sana katoa ufafanuzi na serikali imeyasikia, tutajitahidi kuona kwamba yanafanyiwa kazi. Ukosefu wa madaktari kwa mfano, Tumbe, Sizini na vituo vyengine yote tumeyasikia nasema na wizara imeyasikia na tutayashughulikia ipasavyo.

Lakini suala la makundi maalum, waziri mwenyewe Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto katoa pongezi na waheshimiwa wameligusia makundi vipi yanashughulikiwa na hayatotengwa katika mchakato wetu wa kusukuma mbele maendeleo.

Suala la maji nafikiri sote takriban waheshimiwa wengi sana wamezungumza kwa hamasa sana suala hili. Dada yangu Mhe. Fatma Mbarouk wa Jimbo la Amani amezungumza SEMUSO vipi matumainio yao na mapungufu yaliyotokezea kwa Mkoa wa Mjini Magharibi, lakini hata katika miji mingine matatizo yaliyopo na changamoto zilizopo niseme kwamba, kweli kuna mapungufu lakini pia kuna mafanikio makubwa kabisa katika mle tulimofanikiwa. Tumeambiwa kwamba tusizungumze *figure* tuone *reality* yake zile *figure* zina ukweli?

Mimi niseme kwa kiwango kikubwa kuna ukweli. Tatizo liliopo unajua wenyewe wataalamu wa maji wanatwambia, unajua tunategemea zaidi visima

hivi, leo maji yapo kesho hayapo, *fluctuation* hii ipo. Kwa hivyo, kuna matatizo na *break down* hizi za *pump*, njia kongwe, kwa hivyo inabidi mfumo mzima upitiwe si suala dogo. Lakini kwa kweli mimi nashauri tuipongeze sana, tumpongeze Mhe. Waziri kwa kazi walioifanya na wao wenyewe wameahidi kwamba watajipanga vizuri.

Ningeomba sana kuna waheshimiwa walisema watakaanae *bent*, ningeomba hiyo *benet* iwe kwa upande mzuri tuisaidie wizara twendenayo, isiwe *bent* ile ya kumngojea Mhe. Waziri tukenda tukampiga maswali mazito ya kumlaumu aa. Ningeshauri sana *benet* hiyo Mhe. Hamza na waheshimiwa wengine twendenayo vizuri ya kufanikisha mambo. Kweli tunakubali kuna mapungufu na suala maji ni nyeti kwa jamii yetu inapaswa lifanyiwe kazi ipasavyo.
Mhe. Abdalla Juma Abdalla nakumbuka ulizungumza kwamba utakwenda bega kwa bega na wizara kusaidia kufanikisha mambo ya mji katika Jimbo lako la Chonga. Tunakushukuru sana kwa kauli ile.

Suala la elimu waheshimiwa wengi sana takriban wote wameonesha kukereketwa kwao au kutoridhishwa na mapungufu yaliopo katika kufanikisha Sekta ya Elimu. Lakini kwa kweli tumepiga hatua tena kubwa mapungufu madogo madogo kwenye utekelezaji lazima yatokee. La msingi ambapo Mhe. Rais katika hotuba yake amesisitiza ni suala la kuboresha elimu katika nchi yetu. Hilo tumeona lazima tulipe upeo unaostahiki. Sitaki kuzungumza zaidi suala la kuchangia waziri kalieleza vizuri kabisa.

Kuna Mheshimiwa mmoja alisema kwamba *graduates* hawana kazi, tuache kwanza kuwasomesha mpaka wote tuwapatie kazi, mimi nasema *approach* hiyo sio sahihi. Kwa sababu tusitegemee kwamba *graduate* wanaomaliza wote waajiriwe serikalini, kuna sekta binafsi, kuna kujiajiri wenyewe, lazima tubadilishe mwelekeo huo sasa kwamba tunamtegemea *graduate* aje angoje kazi serikalini, mtizamo huo kidogo sio wa busara.

Mhe. Waziri kasema vizuri sana, kila mtoto tunahakikisha kwamba anapelekwa skuli, kama hana uwezo wa kuchangiwa serikali itachangia. Kweli kuna mapungufu baadhi ya walimu wakuu wanawarejesha tunapata salamu, hilo tutashirikiana na waziri hao walimu wanaofanya mambo hayo tuwarekebishe wasifanye vitendo hivyo.

Suala la uchumi kwa ujumla Mhe. Waziri amezungumza kwa ufasaha kabisa na kwa vizuri, lakini naungana na Mhe. Omar Ali Shehe aliposema kwamba uchumi usikue ndani ya takwimu. Nasema kweli haukui ndani ya takwimu kwa sababu hizi takwimu zinakuwa *computed* kutokana na hali halisi ya mambo sio kama zinabuniwa tu, hizo takwimu alizosema zinakuwa *computed* zinapigwa hesabu. Kwa hivyo, namhakikishia Mhe. Oamr asiwe na wasi wasi haya

mambo ni ya ukweli na tunakubali rai yake ya kuishirikisha ipasavyo *private sector*. Nafikiri Mhe. Waziri kazungumza vizuri kabisa hata Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano nae kazungumza umuhimu wa sekta binafsi katika kuchangia uchumi wetu.

Mhe. Spika, suala la *scheme of service* hasa upande wa walimu na Wizara ya Afya, hilo tumelisikia na hili niseme kwamba ndio maana serikali ikaamua kuunda wizara kamili ya utumishi na utawala bora ili kuona kwamba haya mambo ya *scheme of service* yanatengenezwa na yanafuatilia ipasavyo. Tulikuwa na matatizo kweli malalamiko ni mengi sana kabisa katika mawizara na mambo hayendi vizuri kwenye masuala ya maslahi ya wafanyakazi. Kwa hivyo, haya nawahakikishia Waheshimiwa Wajumbe kwamba ndio maana

Mhe. Rais nalo akalipa uzito suala zima hili la maslahi ya wafanyakazi.
Mhe. Spika, kuhusu suala la ardhi mwenyewe Mhe. Waziri ameeleza kwa ufafanuzi kabisa mimi sitaki kuongeza na naomba sote tumsaidie. Mhe. Spika, nawaomba sana waheshimiwa sote tumsaidie kwa sababu sisi ndio wenye maeneo, sisi ndio wenye majimbo haya mambo yanatokezea katika maeneo yetu. Mhe. Spika, basi haidhuru angalau tumpe *tip* tu kwamba kuna kitu hiki na hiki basi itamsaidia kufanya kazi zake.

Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi sio kigowigowi liwezeshwe, kilio hicho tumekisikia nafikiri na hili serikali itasimamia ipasavyo.

Mhe. Spika, kuhusu suala la barabara waheshimiwa wengi wamezungumza Mhe. Waziri mwenyewe ameshaweka sawa kwa ufanisi kabisa, Mhe. Abdalla Juma Abdalla Jimbo la Chonga, Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani, Mhe. Abdi Mosi Kombo Jimbo la Matemwe, Mhe. Salim Abdalla Hamadi Jimbo la Mtambwe yote waliyoyazungumza ameshasema Mhe. Waziri tumsubiri muda baada ya muda atayafanikisha mimi sitaki tena kuzidisha chochote.

Mhe. Spika, kuhusu suala la mmong'onyoko wa maadili hili nalo waheshimiwa wengi wamelizungumza na wameonesha *concern* zao vipi maadili yetu yanavyomong'onyoka kadiri siku zinavyokwenda. Hili nalo ni suala la kufanyiwa kazi na hasa sisi kama waheshimiwa inabidi tuwasimamie na kama wazee basi tushirikiane na jamii hili suala tuone kwamba kweli ustaarabu unakuja lakini mambo ya maadili ya nchi yetu hayamong'onyoki.

Mhe. Spika, kuhusu misumeno ya umeme hili nalo Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Asaa Othaman Said, Mhe. Mahamoud Muhammed Mussa na wengi walizungumza lakini namshukuru Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa

Kwanza Rais amelitolea ufafanuzi ipasavyo. Mhe. Spika, nataka kusema tu kwamba ile rai mlotupa aliyotoa Mhe. Hamza aidha tupige marufuku na tutoe ruhusa maalum kwa kazi maalum, nafikiri hilo tutalifanyia kazi. Mhe. Spika, hilo tutalifanyia kazi lakini pia tutajitahidi kama serikali tuweke mkakati wa kupiga marukufu kabisa misumeno hii ya moto, kwa kweli inatutia hasara na wewe usiku mmoja tu ukija utaona.

Mhe. Spika, juzi nilipata salamu Mhe. Makamo wa Kwanza walikwenda kirombelo wakaona vipi minazi zaidi ya mia mbili na hamsini imeteketea kwa mpigo mara moja tu. Kwa kweli ni suala la kusikitisha sana, lakini suala la msingi ninaloomba Waheshimiwa mtusaidie tunao viongozi wetu kule katika maeneo yetu, masheha, madiwani, tusaidiane taarif, haiwezekani maeneo tunayaona lakini wengine wananyamaza tu. Sasa hili Mhe. Spika, nafikiri tutajitahidi kufanya mambo ya maamuzi ya pamoja na kuwajua hao wanaofanya hayo mambo.

Suala la uchafu katika manispaa yetu limezungumzwa sana. sote tunajua kwamba miji yetu ndio kioo hasa mji wa Zanzibar, lakini kuna suala zima la kuimarisha usafi pia kuweka mazingira yetu kwa hali ya kuridhisha.
Suala la kuimarisha mapato na kuziba mianya ya uvujaji mapato, Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo namshukuru sana kutoa ufafanuzi mzuri na sina haja ya kurejea.

Haja ya kiwanja kipya cha michezo namshukru Mhe. Waziri kalizungumza na suala la karibu na mwisho la amani na utulivu. Suala hili waheshimiwa wengi wamelizungumza hasa Mhe. Omar Ali Shehe na naomba nimnukuu alisema kwamba, “Zanzibar yenye amani imewezekana, basi Zanzibar yenye maendeleo inawezekana”. Hili ni suala la msingi tunalikubali kabisa.
Kupanda bei za vyakula namshukuru sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko katoa ufafanuzi mzuri tu na niseme kwamba hiyo ndio hali ya kilimwengu tutizame vipi tutapambana nayo.

Mhe. Spika, kulikuwa na masuala *very specific* lakini muda naona umekwenda, sasa haya mengine tutashauriana tuone vipi tutayafanikisha. Lakini kwa ujumla nataka nimalizie majumuisho yangu kwa kuwaomba sana Waheshimiwa tupitie kurasa mbili za mwisho kabisa ukurasa wa 56 na 57 wa hotuba ya Mhe. Rais. Umeandikwa kwa kifupi lakini kwa ufasaha mkubwa sana aliposisitiza kwamba Baraza letu tukufu linao wajibu mkubwa katika kuilinda na kuiletea nchi yetu maendeleo. Baraza lina jukumu la kuchochea maendeleo na pia lina wajibu wa jumla wa kuisimamia serikali. Hivyo, Baraza litapotekeleza wajibu wake vizuri ndivyo jinsi serikali itavyoweza kutekeleza wajibu wake kwa mafanikio zaidi.

Pili amesisitiza kwamba, kwa kuwa Baraza hili limeundwa kwa mchanganyiko mzuri baina ya wazoefu na vijana, na kwa kuwa Baraza lina idadi kubwa ya zaidi ya wanawake kuliko Baraza lolote lililopita, na kwa kuwa utendaji wake utaendana na dhamira ya kuleta umoja wa kitaifa ana matumaini makubwa kwamba Baraza litatoa mawazo yaliyo bora zaidi kwa faida ya nchi yetu na wananchi wake.

Tatu Mhe. Rais amesisitiza kwamba serikali ya awamu ya saba itaongozwa kwa misingi ya katiba, sheria na taratibu zilizopo za kufanya kazi kwa kuonesha mfano na maadili mema na kuweka mbele maslahi ya Wazanzibari wote.
Mwisho alielezea umuhimu kwamba itakuwa ndio dira ya utendaji wa kazi wa Serikali ya Mapinduzi ya Awamu ya Saba.

Mhe. Spika, kwa kweli nimejitahidi kwa haraka haraka kufanya majumuisho haya, lakini nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri kwa kuwa hoja nyingi walizoulizia waheshimiwa, walizotuelekeza tumezisikia na nakuahidi Mhe. Spika, tutashirikiana pamoja na waheshimiwa kufanikisha haya tuliyoagizwa kwa manufaa ya nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wa Dimani ambao nawashukuru sana kwa kunirejesha tena basi naunga mkono hoja hii na naomba nimalizie kwa kusema naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Nakushukuru sana Mhe. Waziri kwa majumuisho hayo. Sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaoafiki hoja hii na kuikubali rasmi hotuba ya Mhe. Rais wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujamaliza kabisa shughuli zetu kwa jioni hii naomba niwakumbushe tu kwamba, kesho ile semina inayohusiana na Mswada wa Utumishi wa Umma itakuwepo katika Hoteli ya *Ocean View* kuanzia saa mbili asubuhi. Nyote mnaombwa kuhudhuria semina hiyo. Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni sana kwa mashirikiano makubwa ya kuendesha shughuli zetu za Baraza na kwa kuipokea rasmi hotuba ya Mhe. Rais ambayo sasa itakuwa inafanyiwa kazi rasmi na serikali.

Baada ya hayo sasa niahirishe kikao hiki hadi siku ya Jumatatu tarehe 24 saa tatu asubuhi.

(Saa 1:45 Baraza liliahirishwa hadi tarehe 24 Januari, 2011saa 3:00 asubuhi)